# UHAKIKI WA VISAASILI KATIKA FASIHI SIMULIZI: UCHAMBUZI WA VISAASILI VYA WAKIKUYU

JANE WANJIRA NGURU,    M.A.

EGERTON UNIVERSITY,JULY 1996

# UHAKIKI WA VISAASILI KATIKA FASIHI SIMULIZI:

# UCHAMBUZI WA VISAASILI VYA WAKIKUYU

Tasnifu hii imetolewa kama sehemu mojawapo ya mahitaji ya shahada ya

MASTER OF ARTS katika Chuo Kikuu cha Egerton.

NA

JANE WANJIRA NGURU

JULY, 1996

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

YALIYOMO UKURASA

Ungamo ........................................ (iii)
Tabaruku ........................................ (iv)
Shukrani ........................................ (v)
Muhtasari ........................................ (vii)

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi ........................................ 1
1.1 Somo la Utafiti ........................................ 1
1.2 Ufafanuzi wa Istilahi muhimu........................................ 1
1.3 Makisio ya Tasnifu ........................................ 3
1.4 Madhumuni ya Utafiti ........................................ 4
1.5 Upeo wa Tasnifu ........................................ 4
1.6 Sababu za kuchagua Mada ........................................ 5
1.7 Misingi ya Nadharia ........................................ 7
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili ........................................ 8
19 Njia za Utafiti ........................................ 16

SURA YA PILI

2.0 Maana ya Visaasili: Maelezo ya tanzu za hadithi mbalimbali.................. 17
2.1 Utangulizi ........................................ 17
2.2 Utanzu wa hadithi katika Fasihi Simulizi ........................................ 17
2.3 Mighani ........................................ 22
2.4 Epiki ........................................ 24
2.5 Ngano ........................................ 26
2.51 Hekaya ........................................ 29
2.52 Hurafa ........................................ 30
2.53 Ngano za Mazimwi ........................................ 31
2.54 Visaasili........................................ 33
2.6 Utambaji hadithi miongoni mwa Wakikuyu........................................ 34

YALIYOMO UKURASA

2.61 Wakati na Mahali mwa utambaji ..... 34
2.62 Sheria zilizohusu utambaji ..... 35
2.7 Hitimisho ..... 38

SURA YA TATU
3.0 Visaasili: Matumizi yake katika jamii ya Wakikuyu ..... 41
3.1 Utangulizi ..... 41
3.2 Uchambuzi wa visaasili kwa kuonyesha matumizi yake ..... 41
3.3 Visaasili kama kifaa cha kuelimisha jamii ..... 43
3.4 Visaasili kama njia ya kutawala jamii ..... 53
3.5 Visàasili: Kutoa maadili katika jamii ..... 62
3.6 Visaasili: Kuonyesha ufundi miongoni mwa Wakikuyu ..... 69
3.7 Visaasili: Kuburudisha na Kustarehesha watu katika jamii ..... 72
3.8 Hitimisho ..... 76
3.9 Tanbihi ..... 77

SURA YA NNE
4.0 Visaasili: Mbinu za Usanaa ..... 79
4.1 Utangulizi ..... 79
4.2 Mbinu za Usanaa katika visaasili ..... 79
4.3 Hitimisho ..... 93

SURA YA TANO
5.1 Muktasari ..... 95
5.1 Matokeo ya utafiti ..... 96
5.2 Mapendekezo ..... 98

MAREJELEO ..... 100

# UNGAMO

Tasnifu hii ni yangu binafsi na haijawahi kutolewa na yeyote katika Chuo Kikuu chochote kwa madhumuni ya kutahiniwa.

JANE WANJIRA NGURU

Tasnifu hii imeidhinishwa kwa niaba ya Chuo Kikuu cha Egerton na:-

PROF. ROCHA M. CHIMERAH

# TABARUKU

Kwa Mama yangu mpendwa Cecilia Wanjiru Nguru ambaye amenisaidia vilivyo kwa hali na mali maishani mwangu.

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani nyingi kwa wote walionisaidia na kuhakikisha kuwa kazi hii imefaulu. Kazi ya M.A. inahitaji jitihada na kujitolea kwingi. Zaidi ya yote, kazi hii inafanikishwa sana na watu wanaomuhimiza mtahiniwa aongeze bidii katika yote ayafanyao. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wao na misaada ya aina mbalimbali waliyonipa, ama ya kitaaluma au hali au mali au aina nyingine yoyote ya usaidizi. Hata hivyo, kunao wachache ambao ningependa kuwataja kwa majina na kuwatolea shukrani zangu.

Kwanza kabisa, ningependa kumshukuru Mungu Mwenyezi aliyenipa nguvu na uhai hadi nikaweza kukamilisha kazi hii. Kutokana na upendo wake Mungu, niliweza kuwa na moyo wa uvumilivu na ustahimilivu dhidi ya matatizo ya aina mbalimbali yaliyonikumba katika kuyakamilisha masomo haya. Ninaamini Mungu alisikia maombi ya jamaa na marafiki walioniombea ufanisi katika masomo yangu.

Ningependa kumtolea shukrani zisizo kifani Profesa Rocha M. Chimerah kwa juhudi kubwa alizofanya katika kunitolea mwongozo mwafaka. Kama msimamizi wangu, Profesa Rocha M. Chimerah alikuwa mvumilivu na alinikosoa kila nilipokosa, alinitolea ushauri wa kufana na yote hayo aliyafanya kwa moyo mkunjufu. Kama Profesa Chimerah hangejitolea alivyofanya, kazi hii haingefua dafu kwani haingekuwa imeumbika vilivyo. Aidha namshukuru Profesa Chimera kwa kunifunza vyema "Coursework" ya mwaka wa pili, wakati nilipokuwa mwanafunzi mmoja tu darasani. Kwa hayo yote, asante sana Profesa.

Vilevile, ningependa kuwatolea shukrani waalimu katika idara ya lugha na isiimu katika Chuo Kikuu cha Egerton kwa msaada na mawaidha waliyonipa. Ningependa hasa kuwashukuru Mwalimu George Mwaro na Mahiri Mwita kwa mawaidha yao na pia kwa vitabu vingi walivyonipa.

Aidha, kuna wanafunzi wenzangu kama vile David Ongarora, Siteti wa Ngero, Mutuku Kavoi, Jacinta Ndambuki, Sheila Wandera, Vicky Khasandi na Jonathan Choti wote wa idara ya lugha na Isiimu na ambao tulishirikiana kwa mambo mengi sana.

Siwezi kumsahau Jacqueline Muchori wa idara ya Jografia kwa msaada alionipa na hasa nilipokuwa ninaiandika tasnifu hii.

Kundi jingine la muhimu sana ambalo siwezi kulisahau ni la wale walionipasha habari mbalimbali katika utafiti wangu. Kazi hii haingekuwa ilivyo bila ya mchango wa walionipa deta na taarifa kadhaa kuhusiana na masuala yaliyomo humu. Miongoni mwao ni nyanya yangu Mwambuimwe Njoki ambaye hakuchoka kamwe katika kunitambia visaasili chungu nzima.

Ningependa pia kuwashukuru dada yangu Yudita Wambui, Kaka zangu Milton Maina na Patrick Mwaniki kwa msaada na mawaidha muhimu waliyonitolea.

Pia sina budi kumshukuru Evans Ombui ambaye msaada wake katika kufanikisha kazi hii haukuwa na kifani. Zaidi ya wote, ningependa kumtolea shukrani zangu nyingi sana David Moshi ambaye kamwe hakuchoka katika kunitolea nakala za tasnifu hii..

Hatimaye ningependa kumshukuru mhazili Carolyne Inganga ambaye alijitolea vilivyo na kuipiga chapa (taipu) tasnifu hii. Namshukuru Carolyne kwa uvumilivu mwingi aliokuwa nao wa kuirudia kazi hii mara nyingi katika kuihakiki na kuyarekebisha makosa yote. Asante sana Carolyne Inganga.

**MUHTASARI**

Utanzu wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika ulipuuzwa kwa namna fulani na Wataalamu wengi wa kigeni. Wengi wa Wataalamu hao hawakuona chochote chenye manufaa katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Ni dhahiri kuwa kauli hiyo ilitolewa na Wataalamu hao, kama vile Finnegan (1970) na Beuchat (1965), bila ya utafiti wa kutosha kuhusu umuhimu wa Fasihi Simulizi katika muktadha wa kijamii. Uwezekano mwingine ni kuwa Wataalamu hao walifanya uchunguzi wao, huku tayari wakiwa wameshafikia uamuzi wao, ambao bila shaka uliathiri matokeo ya uchunguzi wao. Vile vile hatuwezi kupuuza uwezekano mwingine kuwa, Wataalamu hao walishindwa kubainisha tanzu mbali mbali za Fasihi Simulizi na Umuhimu wa tanzu hizo katika jamii.

Ili kuonyesha umuhimu wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika, tasnifu hii imeingilia vilivyo utanzu wa visaasili. Tasnifu hii imejikita katika kueleza maana, matumizi ya visaasili vya Wakikuyu, na kutizama sifa mbalimbali za usanaa zinazotambulisha visaasili kama utanzu maalum na wenye umuhimu mkubwa katika Fasihi Simulizi. Katika kutekeleza lengo hilo, nimeigawanya tasnifu hii kwenye sura tano maalum ambazo pia zina visehemu mbalimbali ili niweze kushugulikia kikamilifu kila kipengele miongoni mwa hivyo nilivyotaja.

Licha ya kuwa visaasili huburudisha hadhira, visaasili aidha hutekeleza jukumu muhimu zaidi la kuwafunza watoto na vijana au hata watu wazima na kuwaelimisha juu ya mambo mbalimbali yanayohusu maisha ya jamii. Visaasili hutoa mafunzo muhimu kuhusiana na matukio au maumbile ya mambo mbalimbali katika jamii.

Sura ya kwanza ni utangulizi wa jumla kuhusu kile ambacho kimo katika tasnifu nzima. Katika sura hii, somo la utafiti, madhumuni na jinsi ambavyo madhumuni hayo yalivyo, ni miongoni mwa mambo muhimu ambayo yamejadiliwa.

Utanzu wa visaasili ni miongoni mwa tanzu nyingine za hadithi zilizomo katika Fasihi Simulizi. Ili tanzu hizo za hadithi zieleweke vilivyo, sura ya pili imejikita katika kutoa maelezo kuhusu tanzu mbalimbali za hadithi.

Aidha katika sura ya pili kuna mambo muhimu yanayohusiana na utambaji hadithi miongoni mwa Wakikuyu. Wakati na mahali mwa utambaji, na aidha sheria zilizohusu utambaji zimetolewa maelezo.

Katika sura ya tatu, matumizi mbalimbali ya visaasili katika jamii ya Wakikuyu yameelezwa. Kwa mfano, umuhimu wa visaasili umeangaliwa kwa undani sana, huku

mifano ya visaasili au vielelezo vya mafunzo vikitolewa. Kwa upande wa namna ya matumizi ya visaasili katika jamii ya Wakikuyu, kuna maelezo kwa undani ya yale manufaa yanayokusudiwa ama ujumbe unaotarajiwa kuifikia hadhira na hivyo kuinufaisha kwa njia ya kielimu na kijamii (mafunzo ya kitaaluma na kijamii).

Sura ya nne imejadili sifa au mbinu za visaasili vya Wakikuyu katika kueleza usanaa unavyojitokeza katika visaasili mbalimbali vilivyochambuliwa.

Sura ya tano ni hitimisho la tasnifu hii. Katika sura hii, muhtasari wa mambo muhimu yanayobainika katika tanifu nzima umetolewa, kisha msimamo wa tasnifu pamoja na mapendekezo mbalimbali kwa wasomi na wapangaji sera za elimu yametolewa.

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Wakikuyu ni kundi la watu walio katika jamii ya Wabantu. Wao huishi katika nyanda za juu zilizomo katika sehemu ya kati ya Kenya. Katika sehemu ya kaskazini mashariki, Wakikuyu wameenea hadi mlima Kenya, ilhali katika upande wa kaskazini magharibi wamesambaa kwenye milima ya Nyahuhuru(Aberdares). Kwa upande wao wa kusini mashariki kuna mlima Kilimanjaro.

Wakikuyu ni wakulima,wafugaji,na aidha walijulikana sana kote Ulimweguni hasa wakati wa vita vya Mau Mau. Kwa muda mrefu, jamii ya Wakikuyu iliongozwa na mabaraza ya wazee walioheshimika sana na wote katika jamii hiyo.

Wakikuyu wana utamaduni mkomavu sana, ambao hupokezwa kutoka kizazi hadi kingine kwa njia ya methali, vitendawili, visaasili, mighani, ushairi na nyimbo ambazo huimbwa hasa wakati wa mbalamwezi (Njau na Mulaki, 1984).

Katika tasnifu yetu, tumechunguza jinsi ambavyo jamii ya Wakikuyu iliunda na kuthamini visaasili vyake, na jinsi ambavyo utamaduni wa Wakikuyu ulijengeka katika misingi ya visaasili katika mtaala wa Fasihi-Simulizi.

### 1.1 SOMO LA UTAFITI

Tasnifu hii imeshughulikia uhakiki wa visaasili katika Fasihi Simulizi kwa kuvichambua visaalili vya Wakikuyu. Tasnifu hii imeupigia mbizi utanzu wa visaasili kwa lengo la kugundua na kuonyesha jinsi utanzu huo unavyodumisha jamii, utamaduni na sanaa. Hayo yamefanikishwa kupitia uchambuzi wa asili au chanzo, maana, matumizi na usanifu wa visaasili miongoni mwa Wakikuyu.

### 1.2 UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU.

#### UHAKIKI

Kuna fafanuzi nyingi kuhusu istilahi ya "uhakiki" kama walivyo wahakiki wenyewe. Katika tasnifu hii hatujaingilia mijadala kuhusu ufafanuzi wa istilahi ya "uhakiki". Badala yake tumejikita na kuzingatia ufafanuzi uliotolewa katika kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981:73):

"Kuhakiki ni kutoa uhakika au ukweli wa jambo, peleleza, chungua. Soma maandishi kwa kuyachambua na kufafanua mambo mbalimbali yaliyomo".

## UCHAMBUZI

Katika tasnifu hii tumetumia istilahi "uchambuzi" kwa kumaanisha kutenga vitu vilivyoshikana au vilivyochanganyika pamoja baina ya kifaacho na kisichofaa. Kisha kutengeneza tayari kwa kutoa uchafu;yaani kusafisha au kuhakiki katika mtaala wa fasihi. Maana hii ya uchambuzi imo katika kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981:73).

## VISAASILI

Visaalili, kama istilahi, imetolewa fafanuzi kadha na wasomi wa taaluma mbalimbali, mathalan wanafasihi, wanahistoria, wanafalsafa, wanaanthropolojia na wanadini. Hata hivyo istilahi ya "visaasili" ni nyeti sana kufafanua. Katika tasnifu hii, istilahi hiyo imetumika kumaanisha aina ya hadithi zinazoeleza asili ya watu au vitu fulani na pengine maendeleo yao ya kale.

Hadithi hizi mara nyingi huwa zinaaminiwa na watu wenyewe ingawa imani hiyo haina ushahidi wa kutosha. Hadithi hizi pia huweza kueleza asili ya mambo kwa mfano asili ya kifo, asili ya tabia fulani (hasa zile za wanyama) na hali fulani au maumbile katika mazingira ya binadamu (Syambo na Mazrui 1992:13). Aidha, katika tasnifu hii, istilahi hii imetumika kwa kuzingatia sifa zake kama zinavyotolewa na mwanafalsafa Olela, (1988:203).

- Visaasili ni kusanyiko la maarifa linaloaminika katika ukamilifu wake au lisiloaminika.
- Hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- Visaasili havihakikiwi katika mitaala ya ushahidi.
- Visaasili havibadilishwi wala kuundwa upya na mtu au kundi la watu. (Olela 1988:203) (Tafsiri ni yetu)

Pia, tunatarajia kufafanua aidha kwa kupunguza au kupanua istilahi hii, iwapo tasnifu hii itakabiliwa na hali hiyo na matarajio ya jamii tutakayoshughulikia.

**FASIHI SIMULIZI**

Hii ni sanaa inayobuniwa, ikawasilishwa na kusambazwa kwa (lugha ya) mdomo. Fasihi hii imekuwa ikihifadhiwa kwa kichwa na kusimuliwa kwa njia ya mdomo, ikipokezanwa kutoka kizazi hadi kizazi. Vyombo vyake vikubwa ni mdomo na sauti ya binadamu katika hali ya kuimba, kusimulia, kuiga, kughani, kutamba, kutega na kadhalika - almuradi yote yanayoelezwa yanatolewa kwa mdomo na ishara za mwili.

**MAANA**

Tumelitumia neno hili la "maana" kuonyesha hasa ujumbe uliotolewa na visaasili.

**MATUMIZI**

Istilahi hii ya "matumizi" tumeitumia kwa minajili ya kuonyesha hasa umuhimu au dhima ya visaasili katika jamii ya Wakikuyu.

**USANAA**

Hii ni njia moja ya kumweleza mtu kitu fulani pamoja na kumfanya awe na hisia fulani juu ya kitu hicho. Kwa mfano muziki, uchoraji au lugha ni sanaa, kwani, kutegemea matumizi yake, vinaweza kutufanya tuhisi furaha au huzuni, tuchamgamke au tukasirike.

## 1.3 MAKISIO YA TASNIFU

Tulikisia kwamba visaasili, kama utanzu muhimu wa fasihi , hutumia mbinu mbalimbali za kisanaa katika uumbaji wake;mfano tashihisi, mafumbo, takriri, onomatopia (tanakali sauti) taharuki, chuku n.k.

Tulikisia pia kuwa utanzu wa visaasili ni utanzu unaojisimamia na uliopewa maana fulani katika jamii ya Wakikuyu.

Vile vile tulikisia kwamba visaasili vina matumizi muhimu katika jamii ya Wakikuyu kama vile kuonya, kukosoa, kukejeli, kuelimisha, kusifu, n.k na ni chombo muhimu cha kufundisha watu katika jamii hiyo.

Aidha, tulikisia kuwa katika jamii ya Wakikuyu, visaasili, viwe vinabeba ukweli au havibebi, huhakikisha maendeleo na uelezaji wa utamaduni kwa kuzingatia hali fulani za kibinadamu ambazo zimeranda kwingi.

## 1.4 MADHUMUNI YA UTAFITI

Tasnifu hii imekusudia kutekeleza malengo manne yafuatayo:-

1. Kubainisha kuwa utanzu wa visaasili ni huru na ni tofauti na tanzu nyingine za fasihi kama vile mighani, epiki, hurafa, hekaya na nyinginezo.
2. Kuvifasiri visaasili vya Wakikuyu zaidi kwa wengine wasioielewa lugha hiyo.
3. Kuonyesha kuwa jamii ya Wakikuyu, kama zilivyo jamii nyingi za Kiafrika, ina uwezo wa kuviumba, kuvihifadhi na kuvithamini visaasili vyake vilivyo.
4. Kuonyesha kuwa visaasili vya Wakikuyu ni hai na vimekamilika vilivyo katika maana, matumizi na pia katika usanaa.

## 1.5 UPEO WA TASNIFU

Tumeshughulikia visaasili peke yake kama utanzu muhimu wa fasihi. Hatukushughulikia uchambuzi wa tanzu nyingine kama vile epiki, mighani, vitendawili, n.k. Tanzu nyingine za fasihi zimetajwa tu pale zilipokuwa zinachangia utanzu wa visaasili.

Visaasili ambavyo tumechambua tumevikusanya kutoka katika kabila la Wakikuyu waishio katika mkoa wa kati nchini Kenya. Tumekusanya visaasili kutoka wilaya za Nyeri, Murang'a, Kirinyaga, Kiambu, Thika na Nyandarua. Sababu ya kukusanya visaasili kutoka wilaya hizi ni kwamba tulitaka kupata visaasili vilivyowakilisha aghalabu jamii pana ya Wakikuyu, ili tusije tukalaumiwa kwa mfano, kwa kuzungumzia visaasili vya Wakikuyu wa tarafa ya Ndia wilayani Kirinyanga, kisha tukavitumia kama kiwakilishi cha Wakikuyu wa mkoa wa kati. Aidha, tulijikita tu katika mkoa wa kati na si kwingineko waishiko Wakikuyu kwa sababu tulikisia Wakikuyu wa mkoa wa kati ni wahifadhina sana wa utamaduni wao kwa sababu hawajaingiliwa sana na athari ya tamaduni zingine.

## 1.6 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Visaasili ni zao la jamii linalotokana na utamaduni na mazingira kwa minajili ya kutimiza shabaha maalum. Kuibuka na kuendelea kudumu kwa visaasili katika jamii ni thibitisho tosha kuwa utanzu huu una umuhimu si haba. Umuhimu na manufaa ya visaasili ukitambuliwa, visaasili vitaweza kupewa nafasi ambayo vinastahili, hasa katika kuelimisha jamii. Kwa kufanya hivyo, visaasili vitathaminiwa na kutumiwa kama amali muhimu na yenye manufaa tuliyorithi kutoka kwa mababu zetu.

Katika jamii nyingi za Kiafrika zamani, elimu ya shuleni na vyuoni haikujulikana. Visaasili vilikuwa mojawapo ya tanzu muhimu sana katika Fasihi Simulizi ambazo zilitekeleza wajibu muhimu; mfano kuikuza jamii kwenye maadili kwa kutoa mafunzo mbali mbali juu ya maisha.

Masuala mbali mbali ya utamaduni na historia, masuala mbali mbali ya utamaduni wa jamii, pamoja na uhusiano wa mazingira yalipata kufundishwa; kwa mfano kuelimisha jamii kuhusiana na asili ya jamii, asili ya maumbile na tabia za watu na wanyama, yote yalitolewa katika visaasili.

Iwapo tunataka kujenga msingi thabiti wa elimu ya kisasa kwa vijana, itatubidi kuangalia urithi wa wavyele wetu; na ikiwa tutafanya hivyo, umuhimu na wajibu kama huo wa visaasili upo hadi leo. Kwa kufanya tafiti mbalimbali katika jamii zetu na kutambua majukumu yawezayo kutekelezwa na amali mbalimbali za kiasili kwa manufaa ya vizazi vya leo, hapo itakuwa ni hatua muhimu kutekeleza lengo hilo.

Kwa kuvitambua na kuvithamini visaasili kama amali muhimu ya jamii, itakuwa sio tu kuviendeleza bali pia kuvihifadhi. Vyombo vya starehe kama vile televisheni, redio,sinema, pamoja na mambo ya kielimu kama vile kusoma maktabani na shuleni, pia kusoma magazeti na majarida ni hali ambazo zimebadilisha kabisa hali na miktadha ya zamani iliyohusu vikao vya utambaji hadithi vikiwemo visaasili. Kuna wataalam mbali mbali kama vile Kirumbi (1975) na Junod (1938) wanaolalamikia kuangamizwa kwa tanzu za Fasihi Simulizi kwa jumla. Kipury (1983) ana maoni kuwa ni jukumu la jamii kuhifadhi Fasihi Simulizi kabla haijakufa kabisa.

Omari na wenzake, (1975). wanasema :-

"Tumeshaona kuwa tusipofanya hivyo kwa wakati huu tulio na watu walio na kumbukumbu hizo, tuna hatari ya kuupoteza urithi huo. Nao vijana wetu,

wanaosoma shule za Msingi na Sekondari au Vyuo vikuu, watapoteza nafasi ya maana."(1975:33)

Iwapo tutakubaliana na mawazo hayo ya Omari, basi kuna haja kubwa sana ya kufanya uchunguzi katika tanzu zote za Fasihi Simulizi, na kuzihifadhi, sio tu kwa njia ya maandishi, bali pia kwa vinasa sauti ili vizazi vya sasa na vijavyo visinyimwe amali hiyo. Kwa hivyo, utafiti wetu utatekeleza wajibu muhimu kwa visaasili.

Katika mfumo wetu wa elimu, aina ya fasihi ambayo hufunzwa na kusisitizwa ni Fasihi andishi. Fasihi Simulizi imekuwa ikipuuza sana hadi hivi karibuni. Kutokana na hali hiyo, kuna upungufu wa vitabu vya somo la Fasihi Simulizi. Kwa sababu hii, twaona kuwa kuna pengo la kiakademia katika somo hilo. Tuna imani kuwa tafiti za namna hii zikifanywa kwa wingi, zitatoa mchango mkubwa sana katika kuliziba pengo hilo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa hatujengi tu misingi imara ya elimu kwa vijana wa shule bali pia tutakuwa tunajenga uhai wa taifa.

Kwa kuchambua visaasili vya Wakikuyu, tutakuwa tumepiga hatua katika kuielewa jamii hiyo kupita kwa misingi ya kifasihi. Ili tuweze kuilewa jamii fulani, hatuna budi kuwaelewa watu wa jamii hiyo. Maoni haya yanaugwa mkono na Akivaga na Odaga (1982:2) kuwa:

"Jamii hutoa fikira zake, njia ya maisha, amali na falsafa maishani kutokana na utamaduni wao. Kusoma Fasihi Simulizi ni njia muhimu ya kurudi kwenye mizizi ya utamaduni wetu. Kuelewa kwetu mambo yanayothaminiwa na jamii nyingine tunazohusiana nazo ni njia mwafaka ya kujielewa sisi wenyewe ... sharti tujue sisi ni nani ndipo tuweze kujua namna ya kukabiliana na jamii zenye tamaduni tofauti".Olela (1981:42) ana maoni yanayokaribiana na yale ya Gotesky anaposema;

"Kila utamaduni huunda na kuthamini visaasili, sio kwa sababu utamaduni huo unaweza kutofautisha kati ya ukweli na uwongo, bali kwa sababu visaasili hivyo hudumisha na kulinda utamaduni usiingiliwe na kuharibiwa. Aidha, hudumisha asasi na mifanyiko ya kiasasi".

(Tafsiri ni yetu)

Hakuna shaka kuwa utafiti kama huu utakuwa ni kichochezi mwafaka kwa wasomi wengine kujitolea na kufanya uchunguzi/utafiti katika tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi, kuhusu makabila mbalimbali kuhusiana na tamaduni tofauti tofauti humu nchini.

Kumekuwa na maoni potofu na uonevu mwingi kuhusiana na Fasihi Simulizi ya Kiafrika kutoka kwa wataalam wengi. Finnegan, (1970:110) ana maoni kuwa tanzu za epiki na visaasili hazipatikani katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Baadhi ya wasomi wa kizungu walikuwa watawala wa kikoloni na hivyo hawakuipa Fasihi Simulizi mahala pake, sababu ikiwa kwamba Serikali za kikoloni zilikuwa na jukumu la kuwastaarabisha Waafrika. Wasomi hao walionelea kuwa, kulingana na vijelezi vyao kuhusiana na tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi, tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiafrika zinaupungufu mkubwa. Kwa kupuuza tanzu hizo, wageni hao waliipuuza Fasihi Simulizi ya Kiafrika kwa jumla. Katika somo letu, tunanuia kuuweka wazi ukweli kuwa fasihi hiyo ina uhai fulani. Kwa kuchungua hasa maana, matumizi na usanaa wa visaasili vya Wakikuyu, tutakuwa tunaionea fahari fasihi hiyo na kuipa hadhi inayostahili.

## 1.7. <u>MISINGI YA NADHARIA</u>

Nadharia ni utaratibu unaotumiwa kama dira ili kuzipa mwelekeo fikira za kitaaluma. <u>Kamusi ya Kiswahili Sanifu</u> (1981) yaeleza nadharia kama mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Nadharia ni utaratibu maalumu unaomwongoza na kumwelekeza mtunzi au mhakiki wa kazi ya fasihi. Wanafasihi mbalimbali wamewahi kuzitumia nadharia tofauti katika kuzihakiki kazi mbalimbali.

Baada ya kuzipitia baadhi ya nadharia za fasihi, tuliona kuwa ni bora tutumie nadharia ya utendaji kazi (Functionalism). Nadharia ya utendaji kazi huhakiki majukumu ambayo mfumo wa kijamii huwa nayo kwa ujumla na aidha huangalia jinsi majukumu hayo yanavyosaidia katika ujenzi na ukuaji wa jamii hiyo.

Brown (1935), aliyekuwa mwanaathropolojia kutoka Uingereza, alichangia sana nadharia hii. Yeye alionelea kuwa nadharia ya tabia za kijamii za mwanadamu ndio hasa msingi wa nadharia ya utendaji kazi. Hii ni kwa sababu, Brown alionelea kuwa mifumo tofauti ya tabia za binadamu huendeleza mfumo wa jamii, mbali na kutosheleza mahitaji ya watu binafsi katika jamii hiyo. Kwa maoni yake, mfumo wa kijamii katika jamii yoyote ile ndio hasa msingi wa kuwepo kwa jamii hiyo. Brown alisisitiza pia kuwa na jamii ambayo huwa na jukumu la kujeleza mambo yote katika maisha. Aidha, jamii ndiyo inayoamua tabia ya wanajamii, iwapo ni tabia kuhusu, kwa mfano, mambo ya kidini, mazingaombwe

na kadhalika. Aidha jamii yoyote ile haiwezi kuendelea vilivyo kama wanajamii wake hawatajifunza jinsi ya kuishi na pia namna ya kueleza hisia zao vilivyo. Hivyo, ni muhimu kwa wanajamii kuwa na hisia zinazofaa ili kuendeleza jamii yao vilivyo.

Okpewho (1983), ana maoni kuwa nadharia ya utendaji kazi ni nadharia inayoamua mfumo wa mahitaji katika jamii yoyote ile, na jinsi mfumo huo unavyohakikisha utoshelezaji na uendelezaji wa mfumo wa jamii. Katika maneno ya Malinowski (1926), ambaye ameichangia sana nadharia hii, nadharia yenyewe huweza ikaitwa nadharia ya mahitaji ya kimsingi inayotosheleza majukumu kadha katika jamii yoyote ile.

Kulingana na madhumuni yetu, nadharia ya utafiti ilitusaidia katika utafiti huu kwani ilitupatia mwongozo wa yale tuliyokuwa tunahakiki na kuchambua kwani tuna imani kuwa visaasili vina jukumu, umuhimu, na maaana fulani katika jamii ya Wakikuyu, na hivyo basi itatusaidia kuendeleza Fasihi Simulizi kama somo kwa jumla.

## 1.8. YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kazi nyingi zimewahi kuandikwa kuhusu visaasili kwa ujumla katika fasihi. Tutaangalia yaliyoandikwa kuhusu visaasili Ulimwenguni, kuhusu visaasili katika Fasihi Simulizi ya Kiswahili na pia kuhusu visaasili vya Wakikuyu.

### YALIYOANDIKWA NA WATAALAMU MBALI MBALI ULIMWENGUNI

Hamilton (1953), ameandika mengi kuhusiana na visaasili vya Wagiriki na Waroma kuonyesha njia au jinsi wanadamu walivyofikiria au kuishi miaka mingi iliyopita. Kulingana na maoni ya Hamilton, visaasili vya Wagiriki na Waroma vilikuwa zao la washairi mashuhuri na vilihusu mambo ya kidhahania. Kulingana na Hamilton, visaasili ni sayansi kongwe, na ni matokeo ya jitihada za wanadamu kujaribu kueleza yale waliyoyaona. Maoni ya Hamilton yalitufaa sana katika kuelewa maana ya visaasili. Hii ni kwa sababu Hamilton ashikilia visaasili humwezesha mwanadamu kueleza yale anayoyaona.

Eliade (1957) asema kuwa, katika karne ya kumi na tisa, visaasili vilimaanisha chochote kilichopingana na ukweli. Hata hivyo, maoni hayo yamebadilika sana kwani jamii nyingi huvichukulia kama msingi wa maisha ya kijamii na utamaduni. Upungufu uliopo katika mawazo ya Eliade hasa wahusiana na kutueleza umuhimu wa visaasili katika jamii. Aidha, maelezo yake kuhusiana na visaasili yanapingana na yetu kwani, katika somo hili, tunachukulia kijelezi cha visaasili kuwa visa au hadithi zinazoeleza asili au chanzo cha

matukio fulani katika maisha. Visaasili, kwa hivyo, twavichukulia vyahusu ukweli ilihali Eliade alionelea kuwa visaasili vilimaanisha chochote kilichopingana na ukweli.

Cunnigham (1973), asema kuwa, visaasili kwa ujumla, huweza kuwa vya kuelimisha, kutukuza, kukemea na kutumbuiza. Asema visaasili huwa ni kuhusu mambo ya wakati uliopo. Visaasili, asema Cunnigham, huwa ni nguvu za kitamaduni zilizo hai.

Cunnigham ana maoni kuwa:

.........Kisaasili kila mara huhusiana na uumbaji, hutuambia jinsi kitu fulani kilivyopata asili yake, au jinsi ruwaza ya tabia, asasi, au namna ufanyaji kazi ulivyoanzishwa (Cunnigham 1973:63) (Tasfsiri ni yetu)

Maoni ya Cunnigham yalitusaidia sana katika utafiti wetu hasa tulipokuwa tunachunguza matumizi ya visaasili katika jamii. Aidha maelezo aliyoyatoa yalituongoza katika kueleza maana ya visaasili.

Stewart (1989), ana maoni kuwa visaasili vina misingi yake katika Fasihi Simulizi. Yeye asema kwamba visaasili ni aina ya hadithi zinazopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo (simulizi). Hadithi hizo hupitishwa au kuwasilishwa na watambaji kwa lengo la kutekeleza majukumu mbalimbali. Stewart asema kwamba visaasili vingi vya kitamaduni hutufikia kwa njia ya kifasihi, na visaasili hivyo ni mpaka wa Fasihi Simulizi, Fasihi Andishi na Historia. Stewart ametufaidi katika kutuonyesha jinsi visaasili vinavyoumbwa, kuwasilishwa na aidha kusambazwa katika jamii.

Kerenyi na Jung (1951), wanashikilia maoni kuwa visaasili huwa hai kwani hueleza asili fulani, ukweli na hali ya sasa ya maisha, na hutoa maadili na mwelekeo fulani wa matendo ya binadamu. Visaasili ni jiwe la msingi la Ulimwengu, kwani kila mtu Ulimwenguni huvitegemea.

Kerenyi na Jung (1951) wasema kuwa mwanafalsafa hujaribu kupenya Ulimwengu wa matukio ili aweze kusema hali halisi ya mambo, ilhali mtambaji wa visaasili hujaribu kutueleza hasa jinsi asili ya mambo ilivyokuwa. Tunakubaliana na maoni ya Kerenyi na Jung kuhusu hasa visaasili kama maelezo yatolewayo kueleza asili ya mambo tofauti Ulimweguni. Aidha maoni yao kuhusu mafunzo ya maadili yatolewayo na visaasili ni ya manufaa kwani yanaunga mkono somo letu kuwa visaasili vinatekeleza jukumu muhimu sana katika jamii.

Niyi Osundare amenukuliwa na Jones (1988), akisema kuwa visaasili na ushairi huhusiana sana tangu zamani. Katika enzi ya kale, ushairi ulionekana kama gari la visaasili.

Hivyo basi leo, kazi za akina Homer, Vigil, Ovid, Euripides na wengine, sio tu aina ya mashairi mashuhuri, bali pia ni msingi wa visaasili vya Wagiriki na Waroma. Jones asema kuwa visaasili na ushairi huhusiana sana kupita kwa lugha. Lugha humwezesha mwanadamu kueleza fikra na hisia zake. Lugha aidha humwezesha mwanadamu kuumba visaasili na pia kuitumia lugha hiyo hiyo katika kueleza uasili wa visaasili kwa kuhusiana na mambo mengine muhimu ya kiisimu. Visaasili ni tokeo la mawasiliano ya namna fulani ambayo huwezeshwa au kufanikishwa na utamaduni wa binadamu na kuendelezwa na lugha. Maoni ya Jones yametufaidi sana kwani, tofauti na wataalamu wengine mbalimbali, yeye ametuonyesha uhusiano kati ya lugha na visaasili. Katika uhusiano huo, bila shaka upo usanaa wa lugha ambao hutumiwa katika uumbaji wa visaasili.

Wellek na Warren (1949), pia wameshughulikia visaasili. Wana maoni kuwa visaasili ni mazao ya jamii. Waendelea kusema kuwa katika enzi ya kisasa, ni rahisi kwetu kutambua wasanii au baadhi ya wasanii wa visaasili. Hata hivyo, kulingana na maoni ya Wellek na Warren, visaasili bado huwa na umuhimu fulani katika jamii, hata kama wasanii wa visaasili hivyo wamesahilika. Maoni ya Wellek na Warren yana umuhimu kwetu kwa vile wametambua umuhimu wa visaasili katika jamii kwa kuona kuwa visaasili hutekeleza jukumu muhimu katika jamii.

Ruthven (1976), katika maoni yake asema kuwa visaasili ni utanzu ulio huru na ulio na haki zake. Aendelea kusema kuwa haki hizo hazijatambuliwa vilivyo katika mifumo mingi ya elimu. Aidha, asema kuwa kuna uhusiano fulani kati ya visaasili na miviga (rituals). Uhusiano huo hutokea kwa vile takriban visaasili vyote huwa na asili yake kutoka kwa miviga ingawa ni muhimu kutaja kuwa miviga haina asili yake katika visaasili. Maoni haya ameyanukuu Ruthven kutoka kwa Robertson (1989).

Maoni ya Ruthven yalikuwa ya manufaa kwetu hasa katika kuonyesha uhuru uliopo baina ya visaasili na tanzu nyinginezo za Fasihi Simulizi. Aidha Ruthven alitufaidi katika kuonyesha usanaa uliopo katika visaasili kwani, kwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya miviga na visaasili, yeye atetea hoja kuwa visaasili ni sanaa za maonyesho sambamba na miviga. Ruthven, bila shaka, anatambua kuwepo kwa mbinu za sanaa katika uumbaji na uwasilizaji wa visaasili.

Olela(1981:42), amemnukuu Gotesky akisema kuwa kila utamaduni huunda na kuthamini visaasili vyake kwa vile visaasili hivyo hudumisha na kulinda utamaduni usiingiliwe na kuharibiwa. Visaasili, kulingana na Gotesky, hulinda wanajamii dhidi ya

kuhangaika na kughadhabika. Aidha hudumisha asasi na mifanyiko ya kiasasi. Maoni ya Gotesky yametufaidi sana katika somo letu, kwani, baadhi ya makisio yetu ni kuwa visaasili hutekeleza jukumu muhimu sana katika jamii. Gotesky amevipa visaasili mahala pake katika jamii na kuvipa hadhi istahiliyo. Kulingana na Gotesky, visaasili huwa ni kifaa muhimu katika kukuza, kueneza na kuhifadhi utamaduni wa jamii yoyote ile. Aidha kuna maoni kuwa visaasili hudumu kwa vizazi vingi bila kubadilika sana. Hata iwapo vinabadilika, mabadiliko hayo huwa ni ya polepole hivi kwamba visaasili havionekani kama vinabadilika.

## YALIYOANDIKWA KUHUSU VISAASILI KATIKA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI

Olela (1988), anashikilia kuwa utamaduni hujengeka katika maswala ya visaasili. Yeye ana maoni kuwa jamii zimejengeka katika visaasili ambavyo hufahamika na wajamii. Kwa mfano, katika nchi kama vile Uchina, Ugiriki na bara Afrika, visaasili huwa na mahala maalum. Hivyo, visaasili ,kama njia mojawapo ya kueleza maswala fulani katika jamii, hutegemewa sana. Kulingana na Olela, maana ya maisha, asili/chanzo cha vitu na matukio fulani, swala la kifo, elimu, ukweli na hata lugha ni baadhi ya mambo yanayoelezwa kivisaasili. Makisio kuhusu maswala haya yanahitaji maelezo ambayo hupatikana katika visaasili. Tunakubaliana na maoni ya Olela kuhusu maana ya visaasili, kwani kijelezi chetu katika somo hili, licha ya vijelezi vingi tofauti vilivyotolewa kuhusu visaasili, ni kuwa visaasili ni hadithi za asili au chanzo cha vitu na matukio mbalimbali katika maisha. Ni muhimu kutaja kuwa Olela ameona umuhimu wa visaasili katika jamii, hasa katika kueleza na kuendeleza utamaduni. Hiyo basi, maoni yake yametufaidi katika uchambuzi wa matumizi ya visaasili katika jamii.

Syambo na Mazrui (1992), wameandika mambo kadha kuhusiana na visaasili. Wana maoni kuwa sanaa ya Fasihi-Simulizi ina tanzu zake ambazo ni tofauti na zile za Fasihi Andishi. Wametaja tanzu kadha za Fasihi Simulizi nazo ni ngano (au hadithi) nyimbo/mashairi, methali na vitendawili. Kuhusu ngano, wana maoni kuwa kuna aina tofauti tofauti kama vile ngano za usuli au visaasili, ngano za ushujaa, hekaya na hurafa.

Ngano za usuli, ambazo pia ni visaasili kulingana na Syambo na Mazrui, ni zile zinazoeleza asili ya watu fulani na pengine maendeleo yao ya kale. Ngano za usuli pia zinaweza kueleza asili ya mambo mengine, kwa mfano, asili ya bahari kupwa au kujaa.

Syambo na Mazrui wametoa mifano ya visaasili, kwa mfano asili ya Wabajuni, na asili ya mwezi kupatwa. Maoni yao, Syambo na Mazrui, yalitufaidi sana katika kueleza maana ya visaasili.

Odaga (1984) ana maoni kuwa katika visaasili, wakati mwingine mambo hutendeka kwa njia ambayo haieleweki kwa binadamu. Visaasili, kulingana na Odaga, ni hadithi zinazojaribu kueleza asili na sababu ya kuwepo kwa matukio fulani. Wahusika katika visaasili huwa binadamu, Wanyama, pepo, miungu, na viumbe vingine vyenye uhai na visiyo na uhai. Wakati mwingi, visaasili huelezwa kama hadithi za kidini, kwa vile mara nyingi huwa vina miungu au viumbe vilivyo na nguvu zisizo za kawaida kama wahusika. Visaasili vingine hueleza kuwepo kwa mito, maziwa, mawe, miamba na kadhalika. Odaga ametoa mifano ya visaasili, kama vile kisaasili cha Waluo kinachoeleza asili ya kifo. Pia ameeleza kisa cha "Kwa nini Wakuria hawali nyama ya ndovu".

Knappert (1971) amechangia utanzu wa visaasili. Yeye amekusanya mighani na visaasili vya watu wa makabila ya Bakongo, Nkundo, Woyo, Makere, Ngbandi, Azande, Mayumbe, Bwana na Kasai wote kutoka nchi ya Zaire. Mifano ya Visaasili alivyoeleza ni; kwa nini bundi huangalia chini, asili ya maisha, na vinginevyo. Ingawa Knappert ametutolea orodha ya visaasili vya makabila tofauti ya Zaire, yeye hajapiga hatua na kutuonyesha umuhimu wa visaasili hivyo, na aidha matumizi ya mbinu za kisanaa katika visaasili hivyo.

Mtaalamu Herskovits (1958), kama alivyofanya Knappert, ametutolea tu mifano ya visaasili kutoka Dahomey. Visaasili alivyokusanya ni vya asili ya kifo, kwa nini kobe huishi mwituni, kwa nini wanyama hawazungumzi, kwa nini kuna wadanganyifu,wazinzi na wezi, kwa nini wanawake hawafai kuambiwa siri, na vinginevyo.

Warner (1986), amekusanya visaasili kadha vya Wabantu; mfano visaasili vya asili ya maisha na hasa uhai wa kabila la Herero kutoka nchi ya Namibia, Kusini mwa Afrika. Aidha ameandikwa mengi kuhusu asili ya kifo miongoni mwa Wazulu, kuhusu mila, imani na tamaduni za wabantu, kuonyesha kuwa kila tukio huaminika kuwa na sababu fulani au asili fulani; -mfano ukame, ugonjwa, mafuriko na kadhalika. Warner ana maoni kuwa visaasili ni muhimu kuendeleza utamaduni wa jamii.

Okpewho (1983), naye ameandika mengi kuhusiana na visaasili. Ana maoni kuwa visaasili sio kama aina yoyote ile ya hadithi, bali ni aina ya visa ambavyo hueleza uwezo wa akili ya mwanadamu katika viwango tofauti tofauti. Okpewho, katika utafiti wake,

amechunguza yale anayoyaona muhimu katika utamaduni wa Mwafrika kifasihi. Kwa kuchambua visaasili kadha kutoka kwa mataifa kadha ya Afrika, anaonyesha jinsi visaasili vilivyo asili au msingi wa fikra ambazo hukuza thamani za kitamaduni kwa jumla. Okpewho aidha amejadili nadharia muhimu za Fasihi-Simulizi, nadharia ambazo zatoa mwangaza zaidi kuhusu visaasili kama vile nadharia ya utendaji kazi. Okpewho ana maoni kuwa visaasili ni sanaa muhimu sana katika jamii ambayo hutekeleza majukumu muhimu katika jamii yoyote ile. Tunakubaliana na maoni ya Okpewho kuwa visaasili huonyesha maendeleo ya akili ya binadamu, hueleza asili ya mambo mbalimbali, na vile vile hutekeleza majukumu muhimu katika jamii nyingi za Kiafrika.

Okpewho (1979), pia ana maoni kadha kuhusiana na visaasili. Yeye asema kuna mbinu tofauti za kisanaa kama vile takriri na onomatopia katika visaasili. Mbinu hizo huonekana sana kutokana na maneno yanavyotumiwa. Huwa kuna mdundo fulani au mpigo fulani wa kimziki katika baadhi ya maneno yanayotumiwa, mfano kusema "Bande Bana Bantu" yaani "Mbande tajiri amefariki" katika lugha ya Yoruba; Nigeria. Mara nyingi maneno ambayo hayana maana iliyo wazi hutumiwa kuonyesha utajiri wa kiisimu wa lugha fulani. Utamu wa maneno yenye mdundo fulani hupatikana, hasa maneno hayo yawapo karibu; na jambo hili hutokea sana katika visaasili, kwani visaasili hivyo hutekeleza jukumu fulani katika jamii. Maoni ya Okpewho yalitusaidia katika kueleza usanaa uliopo katika visaasili.

Mlama (1981), katika Makala ya Semina ya Fasihi Simulizi ana maoni kuhusu usanaa wa hadithi vikiwemo visaasili. Yeye (Mlama) anasema kuwa utambaji hadithi ni sawa na sanaa za maonyesho. Mlama atoa mwongozo hasa wa maendeleo ya sanaa, na binadamu huwa anatafuta mbinu za kukabiliana na mazingira yake. Na kwa vile haelewi mambo kama vile kifo, ngurumo, mafuruko yanasababishwa na nini, anaamini kuna miungu. Ili kuifanya miungu imwokoe kutokana na majanga ya kifo, ngurumo na mafuriko, anaifanyia vitendo na shughuli za kisanii kama vile ngoma, maigizo na kadhalika. Hatimaye, vitendo hivi vinawekwa pamoja kuwa miviga (ritual). Pia hadithi zinatokea kuelezea mambo kadhaa kuhusu miviga hiyo kama vile matendo ya miungu inayohusika. Ili kuingiza matendo haya, sanaa ya utendaji inatumika.

Jamii inapoendelea na kutupilia mbali miviga kwa sababu sasa inaelewa kisayansi mambo yanasababishwa na nini, inaendeleza hadithi zilizokwenda pamoja na miviga hiyo.

Hadithi hizi zinatendeka peke yake kwa madhumuni ya kisanii, na ufundi wa kiutendaji unaogezeka kufikia kukamilishwa kwa sanaa za maonyesho.

Mlama ametufaidi katika kueleza usanaa wa visaasili na aidha katika kueleza umuhimu wa visaasili katika jamii kwani hayo ni baadhi ya mambo aliyoeleza.

## YALIYOANDIKWA KUHUSU VISAASILI VYA WAKIKUYU

Kuna kazi kadha zilizoandikwa kuhusiana na visaasili vya Wakikuyu.

Bottignole (1984), ameandika mambo kadha kuhusu visaasili vya Wakikuyu. Yeye ameeleza asili ya kabila la Agikuyu. Aendelea kusema kuwa jamii hiyo huwa na misingi yake katika visaasili fulani. Visaasili vya Wakikuyu, asemavyo Bottignole, huwa na umuhimu usio haba katika jamii. Kwa jamii yoyote kwa ujumla, visaasili hutoa maelezo ya matukio fulani, tamaduni mbalimbali, hutumbuiza na pia hutoa maadili kwa jamii.

Bottignole asema kuwa Visaasili huwa ni njia ya kuunganisha watu mbalimbali, kwani watu katika vikao vya utambaji huzungumza, hucheka, hukejeli na hukosoana. Vikao vya utambaji mara nyingine huwa na maigizo, muziki na nyimbo ambapo washiriki hupaza sauti, hupiga makofi, hushangilia, huuliza na kujibu maswali. Kwa mtambaji au msanii wa visaasili, yeye hupata fursa ya kuonyesha ufundi na ustadi wake wa kutamba, na huwa na imani kuwa anapotamba, huwasiliana na watu wanaoishi, na aidha wavyele. Jambo la muhimu ni kuwa visaasili vya Wakikuyu hutokana na maisha ya Wakikuyu; visaasili ni amali ya jamii. Visaasili, hivyo, kwa kupitishwa kutoka kwa kizazi hadi kingine, huendeleza ukuaji wa utamadini na jamii kwa jumla. Maoni ya Bottignole yametufaidi sana katika kueleza majukumu au umuhimu wa visaasili katika jamii.

Kenyatta (1938), naye pia ameeleza mambo kadha kuhusiana na jamii ya Wakikuyu. Yeye ameeleza kisaasili kinachohusiana na asili ya kabila na utawala katika jamii ya Wakikuyu, asili ya koo mbalimbali za Wakikuyu miongoni mwa mambo mengine. Kenyatta ametutolea kijelezi tunachokabuliana nacho, kinachosema kuwa visaasili ni hadithi zinazoeleza asili au chanzo cha maisha, kabila, matukio kama vile kifo, mafuriko, ugonjwa miongoni mwa mambo mengine.

Njururi (1966), amekusanya visaasili miongoni mwa jamii ya Wakikuyu; visaasili ambayo vinatoa mafunzo fulani katika jamii. Aidha amekusanya aina tofauti tofauti za hadithi kama vile ngano za mashaka. Kuhusu visaasili, ametutolea kisa kuhusiana na jua na mwezi na chanzo cha uhasama uliokuwepo baina ya viwili hivyo. Uhasama huo ndio

ulisababisha jua kuangaza mchana na mwezi kuchomoza usiku, kwani jua na mwezi ni maadui wakuu. Pia ametueleza kisaasili kuhusiana na asili ya mito na ukame miongoni mwa Wakikuyu. Visaasili hivi vinatutolea mafunzo fulani kama vile umuhimu wa utiifu, umuhimu wa kuheshimiana na kusaidiana miongoni mwa mafunzo mengine.

Kabira (1983), naye pia ameandika mambo kadha kuhusiana na visaasili vya Wakikuyu. Yeye amekusanya hadithi za Wakikuyu, zikiwemo ngano za mazimwi, mighani, hurafa na visaasili. Hadithi zilizokusanywa na Kabira, kwa jumla, zinatoa matumizi kama vile kutoa mafunzo, kuonya, kukemea, kuelimisha, kukashifu, na kusifu. Katika uhakiki wa hadithi hizo, Kabira anatuonyesha jamii inavyomtarajia kila mtu binafsi awe nguli mwenye haki zake. Kabira anamuonea fahari msanii wa hadithi, kwani anaona kuwa msanii huwa na jukumu la kupitisha ujumbe fulani kwa jamii kupitia kwa hadithi zake.

Njau na Mulaki (1984), aidha wameshughulikia utanzu wa ngano za Wakikuyu. Miongoni mwa ngano walizotaja ni hurafa, mighani, hekaya na visaasili.Katika ngano walizoshughulikia, wao wanatufahamisha maana na pia umuhimu wa tanzu hizo mbali mbali katika jamii, umuhimu ambao hasa huzunguka mafunzo fulani muhimu katika jamii.

Mwangi (1976), amekusanya hadithi za Wakikuyu na kuziangalia kama sehemu mojawapo ya maisha ya jamii katika hadithi zake, vikiwemo visaasili. Mwangi ameangazia historia ya Wakikuyu, sheria zao, na hali tofauti za utambaji hadithi hizo. Aidha amezungumzia aina za hadithi, mitindo, na pia wahusika katika hadithi hizo. Yeye amesisitiza kuwa hadithi ndio vifaa mwafaka zaidi vya kuelimisha jamii.

Kutokana na yaliyoandikwa kuhusu visaasili katika Fasihi Simulizi ya Kiswahili na visaasili vya Wakikuyu tunapata kujua kuwa:

i. Jamii nyingi za Afrika huwa zimetambua utanzu wa visaasili kama aina muhimu ya hadithi na hivyo basi zina maana fulani kuhusu hadithi hizo. Maana hiyo hasa yakubali kuwa visaasili ni aina ya hadithi zinazoeleza asili ya matukio fulani, matendo fulani, maumbile fulani na pia maendeleo yake.

ii. Utanzi wa visaasili, kama tanzu nyingine za Fasihi Simulizi, una dhima muhimu katika jamii. Visaasili vina matumizi mwafaka katika jamii.

iii. Utanzu wa visaasili, ili ukamilike vyema na kutekeleza wajibu wake vilivyo, huwa na matumizi ya mbinu za kisanaa.

Wataalamu tuliorejelea hapa wametutolea maana, mbinu za usanaa, na pia, visaasili katika jamii.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI

Tulitumia njia mbili muhimu katika utafiti wetu. Kwanza, kwa vile utafiti wowote ule huanzia maktabaani na kumalizikia maktabani, tulijikita katika utafiti wa kimaktaba. Njia hii imetumika kwa sababu tunaamini kuwa kuna mengi yaliyowahi kuandikwa na wataalamu wengi ambayo yatakuwa ya manufaa kwa utafiti wetu. Tuliyasoma na kuyazingatia yaliyowahi kuandikwa kuhusu utanzu wa visaasili na Fasihi Simulizi hasa ya Wakikuyu kwa ujumla.

Aidha tulifanya utafiti wa nyanjani. Utafiti huo wa nyanjani ulifanywa katika viwango viwili. Kwanza, utafiti huu ulihusika na kuwahoji watu kwa minajili ya kutambua wakwasi wa visaasili ambao tulizingatia katika uhojaji wetu. Katika kiwango hiki, nia yetu ilikuwa ni kutambua mastadi wa visaasili katika jamii ya Wakikuyu.

Kiwango cha pili cha utafiti huu wa nyanjani kilihusu kuwahoji wanajamii na vile vile kuhudhuria sherehe mbalimbali ambazo zilitusaidia kupata deta mwafaka kuhusiana na visaasili. Katika ukusanyaji deta, tulivikusanya visaasili kutoka kwa jamii ya Wakikuyu katika lugha ya Kikikuyu. Visaasili tulivyokusanya ni vile vinavyotoa mafunzo fulani kwa hadhira kwa ujumla.

Tuliweza kuvichambua visaasili hivyo kutoka kwa lugha ya Kikikuyu na kuvieleza kwa lugha ya Kiswahili.

Aidha tulivichambua visaasili hivyo katika viwango vitatu muhimu ambavyo ni:-

a) Maana yake

b) Matumizi yake

c) Matumizi ya mbinu za kisanaa katika visaasili hivyo.

# SURA YA PILI

## MAANA YA VISAASILI: MAELEZO YA TANZU MBALIMBALI ZA HADITHI

### 2.1 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunajikita katika kujaribu kuyaweka wazi maswala mbalimbali yanayowakinza watu wengi. Hivyo basi, tutapiga hatua na kujaribu kueleza hasa tanzu za Fasihi Simulizi zinazoingiliana sana na utanzu wa visaasili. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeyaweka wazi maswala, hasa yanayohusiana na mwingiliano wa tanzu hizo.

Katika sura hii, tunanuia kuonyesha kuwa utanzu wa visaasili ni utanzu ulio huru na unaojisimamia kivyake. Utanzu wa visaasili umekamilika vilivyo na una haki zake, zikiwemo haki za kuweza kuhakikiwa au kuchambuliwa kivyake kama tutakavyofanya katika kazi yetu. Hivyo basi, katika sura hii, tutatoa maelezo mbalimbali kuhusiana na hadithi na aina tofauti za hadithi. Tutafanya hivyo kwa sababu utanzu wa visaasili ambao tutashughulikia ni aina ya hadithi. Tutatoa maelezo kuhusiana na hadithi, na aina tofauti za hadithi; mathalani mighani, epiki, ngano, hekaya, hurafa na hatimaye visaasili. Lengo letu la kueleza tanzu hizo mbalimbali ni kwa sababu kuna watu wengi ambao hukanganywa sana na aina tofauti za hadithi na huona mwingiliano mkubwa uliopo. Hata ingawa mwingiliano huo upo katika tanzu mbalimbali za hadithi, ni muhimu sana kuelewa mwingiliano uliopo na hivyo basi kuweza kueleza sifa mbalimbali za tanzu hizo.

Vile vile katika sura hii, tutatoa maelezo mengine muhimu kuhusiana na utanzu wa hadithi kwa ujumla miongoni mwa jamii ya Wakikuyu. Miongoni mwa mambo tutakayoeleza ni kama vile, mahali na wakati wa utambaji hadithi, na aidha kuhusu sheria mbalimbali zinazotawala utambaji hadithi katika jamii ya Wakikuyu.

### 2.2 UTANZU WA HADITHI KATIKA FASIHI SIMULIZI

Katika kuanza sura hii, labda ni jambo la busara kujaribu na kueleza hasa iwapo ngano na hadithi katika jamii ni kitu kimoja katika istilahi mbili. Katika kufafanua hoja hii, tutaanza kwa kueleza hadithi hasa ni nini katika muktadha wa Fasihi Simulizi.

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) imeangalia hadithi katika sura tatu:

1) Habari za mambo yaliyotukia; mtungo wa habari; kisa, ngano, masimulizi, hekaya.
2) Habari za kubuni, riwaya.
3) Nasaha ya Mtume Muhammad kuhusu mambo ya maisha ya mwanadamu.

Kulingana na kijelezi cha kwanza, inaonekana hakuna tofauti baina ya hadithi, kisa, ngano, masimulizi au hekaya. Katika kijelezi cha pili kuna kipengele cha ubunifu kinachobainisha hadithi ya masimulizi au ya ngano na riwaya. Hali kadhalika kijelezi cha tatu kinaeleza mawaidha, mashauri au mwongozo kuhusu maisha yaliyokuwa yakitolewa na mtume Muhammad. Kutokana na vijelezi hivi vitatu, bila shaka kijelezi ambacho kingekaribia matakwa yetu ni cha kwanza. Hata hivyo, kijelezi hiki ni tata kwa sababu mambo yaliyotukia yanaweza kuwa historia. Je, katika hali hiyo, historia tutaiita hadithi? Ukweli ni kwamba historia na hadithi ni mambo mawili tofauti. Utata zaidi wajitokeza uelezapo hadithi kama mtungo wa habari. Mtungo huu ni wa aina gani na hupitishwa kwa hadhira kwa njia gani? Labda kijelezi cha Hamad (1981) kitatufaa zaidi. Anarejeleza hadithi kama masimulizi ya kinathari (si ya kishairi). Hamad amejaribu kuziba pengo lililoachwa na Kamusi Sanifu la jinsi habari hii inavyowasilishwa kwa nathari au kishairi.

Msokile (1992), aeleza hadithi kama kazi ya sanaa inayotumia lugha. Kwa hivyo hadithi yaweza kuwa masimulizi ya kubuni ama ya kweli yaliyo katika nathari. Sanaa hiyo ya hadithi ni kazi ya mtu yenye mwigo na uyakinifu uliofungamana na wakati, mazingira na mfumo wa jamii. Kwa sababu hii, utanzu huu unaweza kupatikana katika fasihi zote zilizopo katika jamii: Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.

Aidha Msokile ameeleza hadithi kama masimulizi ya kubuni yaliyo katika nathari. Msokile amepiga hatua zaidi na kuongeza kipengele cha ubunifu katika hadithi. Lakini je, ubunifu ulio katika riwaya ni sawa na ubinifu wa hadithi? Kwa upande mmoja tunaweza kusema ubunifu ulio katika hadithi ya masimulizi mara nyingi huwa si wake mtambaji kwani kile mtambaji anachohitaji ni kuunda hadithi upya. Hatuwezi kuelezea

ni nani aliyeitamba mwanzo, lakini katika riwaya tunaweza kueleza ubunifu husika ni wa nani.

Hadithi huwa na wahusika ambao huzungumza katika hadithi hizo. Matendo wanayoyatenda wahusika hao hujenga mtiririko wa vituko unaokamilisha hadithi hiyo. Wahusika katika hadithi wanaweza kuwa ni wanadamu au viumbe vyovyote vilivyopewa sifa na uwezo wa kibinadamu; mathalani wanyama, mawe, miti, mazimwi, mashetani. Viumbe hivi huchaguliwa kutokana na tabia zao; kwa mfano, mnyama kama simba huwakilisha dhana ya ukali, sungura huwakilisha dhana ya ujanja, naye fisi, ulafi. Pia zimwi na shetani hutoa dhana ya viumbe vinavyotisha na hata huwa vina uwezo kuliko mwanadamu.

Hadithi hasa hushughulika na mada tofauti. Baadhi yake ni matukio ya historia, na maendeleo ya watu, ilihali zingine hujaribu kueleza asili ya vitu fulani. Pia kuna zingine ambazo hufurahisha huku zikiwachekesha watu hadi kuwaliza. Hali kadhalika mada nyingine hugusia mila za watu. Hadithi huwa na jukumu kubwa la kutekeleza kwa jamii; mathalani kupitisha utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Pia torathi za jamii husika huhifadhiwa (Odaga, 1984).

Ujumi na sifa zingine za kisanaa huzifanya hadithi kuvutia, hali ambayo huzitofautisha na matukio ya kawaida tu. Mbinu za usanaa, matumizi ya lugha, maudhui na uhusika hupima kiwango cha hadithi.

Kuainisha hadithi katika mafungu tofauti imekuwa si kazi rahisi. Ugumu huu unaonekana na Okpewho (1992:181) asemapo kwamba:

> "Kugawanya hadithi za kisimulizi ni tatizo lenye historia yake.
> Hali hii huonyesha unyeti uliopo katika kugawanya na kuwekea mipaka aina mbalimbali za hadithi."

Hata hivyo Okpewho (1992), anaorodhesha njia nne za kuainisha hadithi. Njia moja kuu ni matumizi ya wahusika; hivyo basi kuwa na hadithi za wanyama, za binadamu na za mazimwi. Katika muainisho huu kuna tatizo kwa sababu kutenganisha wanyama ambao wana tabia zifananazo na za binadamu ni vigumu. Hali kadhalika, kuna mwingiliano wa wahusika wa wanyama, mazimwi na watu. Je, hadithi ambayo ina

wahusika wa aina zote tatu itawekwa katika kitengo gani? Hali kama hii ndiyo inayosababisha ugumu wa kuainisha hadithi mbalimbali.

Njia ya pili ni ya kutumia kigezo cha nia au kusudi la hadithi kutokana na ujumbe au maudhui yanayojitokeza, yawe dhahiri au fiche. Hadithi za aina hii ni za kimaadili. Takriban katika hadithi za aina hii, maadili yanatolewa na mtambaji mwisho wa hadithi. Anaweza kusisitiza uzuri au ubaya kulingana na yale yanayoelezwa na hadithi.

Esenwein (1909), kwa kufuata muainisho huu, amegawanya hadithi katika mafungu matatu, yaani hadithi-adilishi, hadithi-furahishi, na mseto wa hadithi-adilishi na hadithi-furahishi. Mgawanyo huu ni wa jumla mno; - hali ambayo inaufanya ukose wafuasi wengi. Wataalam wengi wameupuuza muainisho huu.

Muainisho wa tatu unaweza kuelezwa kutokana na sifa za hadithi yenyewe. Muainisho huu hasa ndio mpana zaidi na hutumiwa na wataalamu wengi kuainisha hadithi. Kitengo hiki huwa na ukuruba mkubwa na kitengo cha pili kwani huingiza kipengele cha maudhui katika kuainisha hadithi. Njia hii huibuka na hadithi za ujanja na hadithi za mashaka ambazo huishia na swali au tatizo la kimjadala ambalo lahitaji utatuzi baina ya msimulizi na hadhira yake.

Hata hivyo, utoaji wa jawabu hilo unahitaji akili pevu na yenye ujuzi wa mfumo mzima wa kitamaduni na kiitikadi. Masimulizi hayo huweza kuwa mafupi au marefu. Wataalamu kama vile Beuchat (1965), Robert na Dundes (1963) wanayaita masimulizi haya,"tata" ("problem au conundrum"). Mfano mzuri umetolewa na Doke (1947) katika masimulizi yafuatayo:

> Mtu mmoja aliishi na mkewe, mamake na mamamkwe kwenye ng'ambo ya mto. Shamba lake lilikuwa kwenye ng'ambo ya pili ya mto huo naye ilimbidi kutumia ngalawa kila asubuhi kuwavusha mkewe na hao mama wawili hadi ng'ambo ya pili ili wakafanye kazi kisha akawarejesha tena kila jioni. Lakini ngalawa hiyo ilikuwa ndogo sana hivi kwamba ingeweza tu kumvusha mtu mmoja kwa wakati mmoja. Siku moja walipokuwa shambani walivamiwa na genge la majangili.

Walipogutuka tu walitimua mbio kuelekea kwenye ngalawa yao, huku hao majangili wakifuata kwa karibu sana. Muda uliokuwapo wa kujinusuru kabla ya genge hilo kuwasili ni kwa huyo bwana kumvusha tu mmoja kati ya hao wanawake watatu na kuwaacha wengine wakiuliwa. Je, angemvusha yupi? (1947:90)

Hali kadhalika kuna hadithi za kihistoria ambazo hugawika katika makundi kadhaa. Miongoni mwa hizi, kuna mighani ambazo huhusishwa na tajriba za nguli wa kihistoria au matukio ya mtu fulani katika jamii aliye na upekee fulani. Aidha kuna kundi la visaasili ambalo hueleza hasa chanzo cha ukoo au mtawala fulani, kuna vinavyoeleza asili ya vita na matukio mbalimbali yapatikanayo katika jamii. Fauka ya vikundi hivi, kuna epiki ambazo huelezea sifa za kiajabuajabu za nguli fulani katika jamii ambaye hutenda mambo ambayo wakati mwingine hayawezi kuaminika.

Pia kuna hadithi za asili ambazo kwa njia fulani zina uhusiano na hadithi za kihistoria. Hadithi hizi hueleza asili ya watu au mambo mbalimbali katika jamii (kwa mfano, moto, ibada, ukulima n.k.) na pia huelezea mambo ya kimaumbile (radi, kifo, n.k.). Ikiwa hadithi za asili zinaelezea juu ya asili ya watu fulani, hali kadhalika zitaitwa mighani kwa sababu zinagusia juu ya matukio kumbukizi na watu walio na upekee fulani katika jamii. Ikiwa zitaelezea elementi za maumbile au utamaduni, mara nyingi huitwa visaasili. Visaasili mara nyingi vina misingi ya uunguungu. Muainisho huu ndio hasa ambao ni maarufu sana na hutumiwa na wataalamu wengi kuainisha hadithi. Mathalani, Kipury, Akivaga na Odaga, Hamad na Syambo na Mazrui, japo kuna tofauti kidogo hapa na pale.

Njia ya nne na ya mwisho katika kuainisha hadithi huzingatia muktadha na wakati hadithi husika inapotambwa. Kwa mfano, hadithi za mwezi ambazo hutolewa wakati wa mbalamwezi. Kimsingi hadithi hizi ambazo hutambwa wakati huu zinaweza kuwa zozote kutoka mafungu yoyote ambayo tumeshayajadili. Pia kuna hadithi za wawindaji ambazo hutolewa au hutambwa wakati wawindaji wanapopumzika. Hadithi zao huwa zinazingatia mapambano yao na wanyama, mazimwi na pepo.

Kufikia hapa, ni jambo la busara kutaja kuwa miongoni mwa miainisho hii, muainisho wa tatu ambao huzingatia sifa za hadithi, na ambao huwa na ufungamano na muainisho wa pili ambao huzingatia maudhui, ndio maarufu zaidi miongoni mwa wataalamu. Ingawa wataalamu hawa wanatofautiana kidogo, wao wanafuata mkondo mmoja. Tofauti iliyopo baina ya wataalamu hawa (Okpewho, Taban Lo Lyong, Odaga, Akivaga na Odaga, Nandwa na Bukenya, Lusweti, Kipury, Hamad, Mazrui na Syambo) ni idadi ya mafungu. Aidha mmoja anaweza kuwa na mafungu mengi zaidi ya mwingine. Hata hivyo, kimsingi wana makundi matatu makuu ya hadithi ambayo ni visaasili, mighani na ngano. Wataalamu hawa hawatofautiani wanapoainisha visaasili na mighani ijapokuwa mafungu hayo yanaingiliana wakati mwingine. Tofauti za kiidadi zinazuka wanapoanisha ngano tu. Tutaendelea na kueleza mafungu muhimu ya hadithi ambayo ni mighani, epiki na ngano.

## 2.3 <u>MIGHANI</u>

Hamad (1981), anaelezea mighani kama aina ya hadithi ambazo hueleza historia ya matukio fulani. Matukio hayo huwa ni ya kweli ila yamewekwa katika mtindo wa hadithi. Wahusika wake hasa huwa ni mashujaa au nguli waliotajika kwa umaarufu wao na kutenda mambo yasiyoweza kuaminika. Vitendo hivi vya kihistoria huwa na ukweli fulani. Mighani hukaribiana sana na visaasili, ndiposa Akivaga na Odaga (1983) wanaona uainisho wa aina hizi mbili za hadithi huweza kuleta utata. Wanaeleza:-

> Mighani au hadithi ya kishujaa ni sawa na visaasili, kwamba huzungumzia juu ya mtu au matukio ya wakati uliopita (1983:30).

Walakini, wanaainisha kwamba visaasili huenda hadi mwanzo wa kila kitu au hujaribu kueleza matukio yasiyoeleweka bayana, kwa mfano kifo, maisha baada ya kifo, n.k. Mighani, kwa upande wake, ni masimulizi yanayorejelea wahusika wa kihistoria, ingawa wahusika hawa hupewa sifa za kiunguungu. Ni kweli kwamba visaasili na mighani huweza kuwa na misingi fulani kihistoria, lakini kulingana na vile vinavyotambwa, katika mapito ya nyakati, hutiwa chuku kutokana na ubunifu wa mtunzi na, wakati mwingine, hupata chembechembe za kidhahania. Kinachojitokeza hapa ni

kwamba mighani ni mara nyingi, masimulizi ya mambo yaliyotokea na yana ukweli wa kihistoria, ilihali visaasili ni visa ambavyo vinaelezea asili ya mambo mbalimbali katika jamii. Bukenya na Nandwa (1983:47) wanapiga hatua zaidi na kutofautisha ngano, visaasili na mighani. Wanasema ngano huchukuliwa na wale wazitambao kama tungo za kibunifu ambazo hazina ukweli wowote, ilihali visaasili na mighani huchukuliwa kama ukweli. Mighani na visaasili vinapozingatiwa kutoka jamii moja hadi nyingine, huenda vikageuka na kuwa ngano. Lusweti (1984:96) naye aendelea na kueleza kuwa mighani zingine hueleza hasa utamaduni na historia ya kundi fulani la watu.

Mighani hupatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Sankan (1971) ametutolea mighani kadha za Wamaasai. Miongoni mwa mighani alizoeleza ni kuhusu Senteu na Olonana waliokuwa ndugu wa kambo waliooneana wivu na kupangiana njama, hadi aliyekuwa mdogo, Olonana, akaweza kupokea baraka za baba yao Mbatiany aliyekuwa mzee sana karibu kufa. Mighani hiyo bila shaka inalingana sana na hadithi ya Esau na Yakobo katika bibilia ya agano la kale. Mighani bila shaka zina mafunzo fulani,mfano katika mighani ya Senteu na Olonana. Sankan (1971) huenda ana nia ya kuonyesha uovu uliopo katika wivu.

Onyango na Roscoe (1974), nao wametutolea mighani maarufu sana ya Lwanda Magere miongoni mwa Waluo. Mighani yenyewe yaeleza jinsi Lwanda Magere alivyokuwa na uwezo wa kipekee kwani iliaminika kuwa mwili wake uliumbwa kwa jiwe. Magere, hivyo basi, angeweza kuwashinda maadui wote kwani, vitani, yeyote aliyejaribu kumdunga kwa mkuki, mshale, au silaha yoyote ile, alishindwa kwani alidunga jiwe kwa hivyo silaha yake ingevunjika. Baadaye Magere alipangiwa njama na kundi jirani la watu waliojulikana kama Walang'o. Magere aliozwa msichana mrembo wa Lang'o na, baada ya kuishi naye kwa muda mrefu, aliweza kuvumbuliwa siri ya nguvu zake. Alimwambia msichana huyo akate kivuli chake na kukitia dawa kwani yeye (Magere) alikuwa mgonjwa sana. Msichana Mlang'o alifurahi sana kwa kujua siri ile; na mara tu alikimbilia kwao na kuwaeleza watu wa kwao siri hiyo. Wote walishangaa, na walipopigana na Waluo tena, mmoja wao alijitahidi sana kudunga kivuli cha Magere kwa mkuki wake; na hapo hapo Lwanda Magere alianguka na kufariki. Alipoanguka Magere tu, mwili wake, ambao ulikuwa jiwe, uliweza kuwa palepale hadi leo. Hii ndio

sababu, katika jamii ya Waluo, kuna imani kuwa yeyote yule anayekinoa kisu au mkuki au silaha yoyote ile kwenye mwamba uliokuwa mwili wa Magere, huweza kupata ushindi au ufanisi katika jambo lolote lile afanyalo. Waluo, hivyo basi, wametunga nyimbo nyingi za kumsifu na kumtukuza Magere kwani alikuwa nguli katika jamii hiyo.

## 2.4 EPIKI

Baadhi ya wataalamu, mathalani Finnegan (1970:108) wametilia shaka kama Fasihi Simulizi ya Kiafrika ina epiki. Lengo letu katika tasnifu hii wakati huu si kujitia katika mjadala wa kuwepo au kutokuwepo utanzu huu, bali ni kufafanua maana yake na kuchunguza iwapo kuna tofauti kati yake na visaasili, ambayo ndiyo hasa mada yetu ya tasnifu.

Epiki hueleza sifa zisizo za kawaida za mashujaa mbalimbali katika jamii fulani; mfano Sundiata kutoka Mali, Shaka wa Afrika Kusini au Fumo Liyongo kisiwani Pate, Kenya.

Kimsingi epiki ni mtungo mrefu unaoeleza sifa za mashujaa. Mashujaa hawa huwa na sifa zisizo za kawaida. Ushujaa huu hasa hutegemea jamii mahsusi kwani shujaa katika jamii moja huenda asiwe shujaa katika jamii nyingine. Iwapo tutatazama tanzu za epiki na mighani kwa kijuujuu, tutaona kuwa hakuna tofauti baina yazo kwani zote mbili huzungumzia juu ya mashujaa walio na sifa za kiajabuajabu katika jamii husika. Kimsingi, utungo wa mighani ni mfupi kuliko wa epiki. Aidha, katika mighani, wahusika huwa ni watu walioishi, ambao kuishi kwao kunaweza kuthibitishwa, ilihali katika epiki, wengi wa mashujaa hawa hatuwezi kuthibitisha kuishi kwao. Jamii nyingi huamini kuwa mashujaa hao waliishi ingawa mara nyingi hakuna ithibati kamili. Kwa kutumia kigezo cha wakati, huenda mighani ibadilike na kuwa epiki baada ya kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa muda mrefu. Watu wa jamii husika huamini tu kulikuwa na shujaa fulani, na ifikiapo hatua hii, huwa si mighani tena bali ni epiki.

Mbele (1977), Okpewho (1977) na Biebuyck (1978) ni miongoni mwa wataalamu waliotetea hoja ya kuwepo kwa epiki katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Mbele haingilii sana mjadala huu bali anachukulia tu kwamba utenzi wa Sundiata wa Wamalinke wa Afrika Magharibi ni epiki. Okpewho, tofauti na Mbele, anaelemea zaidi

upande wa muundo na fani ya epiki. Anazitazama tenzi za Kambili na Mwindo na kujaribu kubainisha sifa za kimuundo, kisanaa na kiutendaji (performance) za tenzi hizo, kuzilinganisha na sifa za tenzi za mataifa mengine, na kuhitimisha kuwa tungo hizi pia ni epiki. Baadhi ya sifa alizozitaja ni: - formula, visifa (epithets), theme (topos), uhusisho (association), takriri (marudiorudio), malumbano ya wahusika, uchepuo (digression), n.k.

Biebuyck katika Oinas (1978:336ff) anaungana na Mbele na Okpewho kuthibitisha kuwa katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika kuna utenzi wa epiki. Anaonelea kuwa kauli ya Finnegan kuwa hamna epiki katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika ilisababishwa na upungufu wa data, na kuendelea "kutuchorea ramani ya epiki" katika Afrika. Ramani hiyo inaonyesha kuwa epiki hupatikana miongoni mwa Wamande, Waswahili, Waghana na pia miongoni mwa watu wa Afrika Kusini. Biebuyck anaendelea na kusema kuwa tungo za epiki ni zenye sifa za kiulimwengu na vile vile sifa za pekee za utanzu huo katika eneo linalohusika.

Mpaka hapa, mjadala wetu umetuonyesha mambo yafuatayo: Kwanza, tumeonyesha kwamba utanzu wa epiki ni utanzu halisi wenye sifa za kifani na kimaudhui. Sifa hizo ni pamoja na muundo wa kimantiki, visa vinavyoshabihiana na kuhusiana; vituko vya kitenzi hasa migorogoro na usuluhishi wake; lugha ya kishairi; urefu wa kutosha, na maudhui ya kitenzi; matukio ya ushujaa na migongano ya kiutawala inayo sawiriwa.

Pili, tumeona kuwa utanzu huohuo, kwa mujibu wa maudhui yake, umetokana na migogoro halisi ya kijamii.

Tatu, tunaona kuwa utanzu wa epiki si wa kipekee sana duniani bali ni matokeo ya maendeleo ya kijamii na kisanaa ya kiulimwengu; na kwamba, kimaudhui na kifani, takriban epiki zote hufanana. Kadhalika, epiki zina sifa zake maalum ambazo zinatokana na utamaduni, mazingira na tabia maalum ya lugha au kabila husika. Mfano, utenzi wa Fumo Liyongo umetawaliwa na maswala ya utamaduni wa Pate.

Jahadhmy (1975) ni baadhi ya waandishi walioelezea utendi wa Liyongo. Liyongo alipangiwa njama Pate, na Wapate walijaribu yote waliyoweza kulingana na mazingira na utamaduni wao ili kumtia mbaroni Liyongo. Jahadhmy aeleza:

........... Liyongo akatambuwa huzengeya kuuawa pale Patekayepuwa barani akitembeya.

Mfalume changaliya mwituni mekimbiliya Wasanye aliwazengeya na Wadahalo pamoya ......

Siku moya wakanena na tuleni waungwana kikoa ni tamu
sana karamu isotindikiya (42-61).

Miongoni mwa Wapate mlikuwa na sherehe ya kula 'kikoa' ambamo kila aliyeshiriki katika sherehe hizo alihitajika kupanda mti na kuangusha au kuchuma makoma.

Epiki ya Liyongo hasa yaonyesha jinsi utenzi huo ulivyo na matokeo ya maendeleo ya jamii husika. Sifa za ushujaa za Liyongo aidha zatokezwa wazi katika utendi wa Liyongo. Mfano:

Ni mwana mume sahihi kama simba una zihi, usiku na asubuhi kutembea ni mamoya.

Ghafula kikutokeya mkojo hukupoteya, tapo likakujiliya
ukatapa na kuliya.

Liyongo kenda Muyini akipita mlangoni, panda katiya kanwani kivuzia kapasuwa.

Kufikia hapa, tumeonyesha dhahiri kuwa utanzu wa epiki upo katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika na pia tumejaribu kuangalia mwingiliano wa utanzu huo na ule wa mighani.

## 2.5 NGANO

Wataalamu mbalimbali wanajaribu kuelezea ngano ni nini na hali kadhalika kuziainisha katika makundi mbalimbali.

Msokile (1992), anaelezea ngano kama hadithi fupi katika Fasihi Simulizi. Anaendelea kusema kuwa ngano huhifadhiwa kichwani na kutolewa kimasimulizi kutoka

kizazi hadi kingine. Syambo na Mazrui (1993), Hamad (1981) na Senkoro (1982) hawatofautiani na Msokile kwani wanaiona ngano kama aina ya hadithi ambayo husimuliwa kwa njia ya kinathari. Naye Esenwein (1909) anasema yafuatayo kuhusu ngano:

> Ngano ni masimulizi yaliyorahisishwa, ni mafupi na yasiyo na muundo kama wa hadithi za kawaida. Masimulizi hayo hutumia wahusika bapa na hutegemea matakwa ya fanani katika kujenga vitendo mbalimbali kuliko muundo katika kuwajenga wahusika. Wahusika bapa watajwao katika dondoo hili, ni wahusika wasiokua, wala wasiobadilika kimatendo na huwakilisha tabia mbaya au tabia nzuri.(1909:109)

Muhando na Balisidya (1976), wanasema ngano ni aina maalum ya hadithi ya jamii yetu, fasihi ambayo ilitumia zaidi akili na ubongo wa binadamu kwa kuhifadhiwa kwake. Wanaelezea muundo wa ngano na maudhui yake:

> Ngano nyingi aghalabu ni fupi na, kutokana na ufupi huo, hizi si hadithi zinazoingilia mambo ya undani sana. Hadithi huingia moja kwa moja katika kulitoa wazo kuu, na kila kipengele kijengacho ngano; wahusika, vielelezo na mizungu mingineyo huelemea katika wazo hilo.(1976:75)

Hapa, waandishi wanajaribu kutuelezea kuwa mada zinazoshughulikiwa na ngano huwa hazizami ndani, na vipengele vyote viundavyo ngano huzunguka mada hii. Msokile (1992), anaendelea kuelezea kuwa ngano simulizi zinapewa uzito wa kisanaa kwa sauti na matendo. Hali kadhalika wahusika wa ngano sio lazima wawe wa kuaminika, na mhusika mkuu ndiye kiungo cha hadithi nzima.

Senkoro (1982:69) anapiga hatua zaidi alinganishapo ngano na hadithi fupi ya kisasa. Kulingana na Senkoro, ngano ni utanzu wa Kifasihi Simulizi ambao ulipitishwa toka kizazi hadi kingine kwa njia ya mdomo. Anaendelea kueleza kuwa utunzi wa ngano, kinyume na wa hadithi za siku hizi, haujulikani wala hauelezwi kuwa ni wa mtu huyu ama yule. Fauka ya haya, ubinafsi wa kiutungaji pamoja na umuhimu wa ufahari wa mtungaji haukuwa na uzito tuuonao leo katika Fasihi Andishi. Hapa umuhimu na uzito uliwekwa zaidi katika maadili na mwenendo wa jamii ilimotungwa ngano ambayo ilitetea amali za kijamii na kila mtu alikuwa huru kusimulia. Senkoro, kwa kuchangia zaidi anasema ngano, ikilinganishwa na hadithi fupi, wahusika wake ikiwa si bapa huwa wawakilishi tu wa tabia ama mwenendo fulani; pia huwa ni wachache na, aghalabu,

mhusika mkuu wa ngano ndiye hasa anayebeba elimu kubwa na maudhui ya ngano hiyo. Mara kwa mara, katika ngano, kuna wahusika wema kabisa na wabaya kabisa. Lengo letu kufikia hapa hasa ni kufafanua istilahi hii "ngano". Ni wazi kuwa Esenwein, Senkoro, Msokile, Muhando na Balisidya wana maoni kuwa ngano ni aina maalumu ya hadithi ambayo ilihifadhiwa akilini au ubongoni mwa binadamu na ilipitishwa kutoka kizazi hadi kingine kwa njia ya mdomo.

Ngano, kama tanzu nyingine za Fasihi Simulizi, zilikuwa na matumizi yake maalumu na, hata kufikia sasa, majukumu haya yangali yapo. Bascom (1954), anasema kuwa ngano zilikuwa na jukumu kubwa katika jamii; ameyaainisha majukumu manne muhimu yatekelezwayo na ngano au masimulizi katika jamii. Majukumu hayo ni:

- Kuburudisha.
- Kuendeleza utamaduni kwa njia ya kutoa mfumo maalum wa mila.- Kuelimisha - kupitia kwa kupongeza tabia njema na kukashifu tabia mbaya.- Kujibu maswali kuhusu chanzo cha mambo mbalimbali ya kijamii na visaasili.

Katika mchango kuhusu majukumu ya ngano, Crowley (1969), ana maoni kwamba masimulizi, kama vile ngano, yanaelezea na kuendeleza hadhi ya imani za kidini na mashaka ya "miviga" na kusaidia kuendeleza umoja wa kijamii.

Kama ilivyo hadithi, ngano nazo zinagawika katika mafungu kadhaa. Wataalamu mbalimbali wamejaribu kuanisha ngano, lakini migao hii mara nyingi hairidhishi. Esenwein (1909) alijaribu kuainisha ngano, hasa kwa misingi ya maudhui na jukumu. Kutokana na muainisho huu, aliibuka na aina tatu za ngano. Aina hizo ni ngano-adilishi, ngano-furahishi na mseto wa ngano-adilishi na ngano-furahishi. Mgawanyo huu ni wa jumla mno na kwa hivyo hauelezi aina tofauti za ngano vilivyo.

Finnegan (1990), naye alizigawanya ngano katika makundi ya jumla mawili kufuatana na wahusika wanaotumika - wahusika watu na wahusika wanyama. Finnegan anasema kijumla na kifupi kuwa ngano za wahusika wanyama ni fupi, zinasisimua na zinakejeli. Ngano zinazotumia wahusika-watu ni nyingi na huwa, kwa kawaida, ni ndefu

kidogo kuliko zile za wahusika-wanyama. Hata hivyo mfano huu ni wa kijumla sana kwani ni vigumu kuainisha ngano zilizo na wahusika wanyama pamoja na wanadamu. Okpewho (1992), alipokuwa akifafanua njia mbalimbali za kuainisha hadithi, alidokeza kuwa muainisho wa kufuata kigezo cha wahusika una utata wake. Hali hii husababishwa na ukweli kwamba tabia za kibinadamu ambazo hupewa wanyama, huleta shida tunapojaribu kuwekea mipaka wanyama na binadamu.

Miongoni mwa miainisho hii, tumeonelea kuwa tutajikita katika muainisho unaozingatia hasa maudhui ukichanganya na sifa za ngano husika. Hii ndiyo njia ya tatu inayoelezewa na Okpewho (1992), ambayo hutumika kuainisha hadithi kama tulivyokuwa tumetangulia kueleza. Ingawa muainisho huu ni mpana sana, ndio unaozingatiwa na wataalamu wengi, mathalan Okpewho, Taban Lo Lyong, Odaga, Akivaga na Odaga, Lusweti, Nandwa na Bukenya, Kipury, Hamad, Syambo na Mazrui.

Kama tulivyokuwa tumeshataja hapo awali, tofauti baina ya wataalamu hawa si kubwa sana. Tofauti hiyo husababishwa na idadi ya mafungu ambayo kila mtaalamu huibuka nayo baada ya kuainisha ngano. Hali kadhalika, itafaa kutaja kwamba muainisho unaopendekezwa na Esenwein (1909), ambao huzingatia maudhui, utatufaa sana, tunapouunganisha pamoja na muainisho wa Okpewho (1992). Kimsingi, ngano zimegawika katika hekaya, hurafa, febo, ngano za mashaka, mazimwi na pepo.

### 2.51 <u>HEKAYA</u>

Hekaya, kwa kawaida, ni kisa kifupi kilichokusudiwa kubaini hekima au funzo fulani. Wahusika wanaotawala hekaya ni binadamu. Ngano hizi huelezea visa vya binadamu wa kawaida au pia vinaweza kuwa ni visa vya ajabu. Syambo na Mazrui (1992) wanadokeza kwamba hekaya zinazojulikana Uswahilini ni zile za Abunuwasi. Kuna visa vingi ambavyo vinaweza kuelezea hekaya hasa ni nini. Mathalani, miongoni mwa jamii ya Wakikuyu, mna hekaya kuhusu kijana mmoja aliyeitwa Maara. Maara alikuwa kijana wa pekee wa mzee mmoja aliyekuwa maskini sana. Mzee huyo alikuwa na mke mmoja tu aliyekuwa mamaake Maara. Mzee huyo alipata riziki yake kutoka kwa uwindaji. Mamaake Maara hakufanya kazi yoyote; na, siku moja alipatwa na ugonjwa na akafariki. Maara na babake waliuchukua mwili wa mama huyo na kuutupa

msituni uliwe na fisi, kwani siku hizo mazishi yalikuwa hayajulikani. Babaake Maara naye alizidi kuzeeka na kudhoofika siku baada ya siku. Hivyo basi ilimlazimu Maara kwenda kuwinda ili amtafutie babaake chakula. Wakati mwingine, wao wawili hawakupata chakula kwani uwindaji ulikuwa kazi ngumu sana. Maara kila mara alikuwa na huzuni kwani aliona kwamba hakuwa na chochote cha kurithi kutoka kwa babaake..

Siku moja Maara aliamka asubuhi na akamkuta babaake amefariki. Alifiriki kwa háraka sana la kufanya. Hivyo basi fikra ilimjia na kumwonyesha kuwa ni bora auchukue mwili wa babaake na kuuweka kando ya barabara ambapo kila asubuhi ngombe walipitishwa kwenda malishoni. Maara alisimama mbali ambapo hangeweza kuonekana na, kwa vile mahali hapo palikuwa mlimani, ng'ombe hao walimkanyagaka-
nyaga babaake Maara, jambo ambalo lilimfanya Maara atoke mafichoni mwake huku akilia kuwa babaake ameuawa na ng'ombe. Wachungaji wa ng'ombe hao walishtuka sana na kumbembeleza Maara asiwachukulie hatua kali ya kwenda kwa mganga kama alivyokuwa amewatisha. Wachungaji hao walimlipa Maara kifo cha babaake kwa ng'ombe wengi ambao walimuwezesha kuoa wake wengi sana na kuwa tajiri mkubwa kabisa kijijini. Watu wa kijiji hicho waligundua baadaye ujanja wa Maara lakini hakuna jambo walilotenda; kwani Maara tayari alikuwa tajiri mkubwa sana.

Hekima iliyomo katika hekaya hii yaonyesha kuwa mtu huweza akatajirika kwa urahisi sana iwapo ataitumia akili yake vilivyo. Hekaya, hivyo basi kwa ujumla, huwa za aina hii, fupi na zenye hekima.

## 2.52 HURAFA

Hurafa ni ngano ambazo wahusika wake ni wanyama ingawa wanyama wenyewe, kwa kawaida, huwa na tabia za kibinadamu. Ngano za aina hii zimeenea sana miongoni mwa jamii nyingi za Kiafrika (Syambo na Mazrui, 1992). Hurafa zinaweza kugawika katika sehemu mbili:

1). Zile zinazojaribu kueleza asili ya tabia fulani ya wanyama au sura zao au hali zao za kimaumbile. Katika ngano za aina hii lazima kuwe na sababu na matokeo ya kitendo chenyewe. Hueleza tabia za baadhi ya wanyama hadi kufikia leo. Mathalan, katika kisa cha Mwewe na Kuku. Katika kisa hiki ambacho kilitokea hapo zamani za kale, Kuku alienda kumwazima Mwewe sindano lakini, kwa bahati mbaya akaipoteza. Kwa sababu

ya kitendo hiki, ili kufidia gharama ya sindano, Mwewe kila mara anawavamia vifaranga wa Kuku. Hata kufikia leo, Kuku angali anachakurachakura huku akitafuta sindano ya Mwewe. Hali hii ya mambo yaeleza ni kwa nini kila mara Kuku huwa anachakura na pia ni kwa nini Mwewe anawavamia vifaranga wa Kuku. Ngano hii inatutahadharisha tuwe waangalifu kwa chochote tukifanyacho na hasa tuazimapo vyombo kutoka kwa wenzetu.

2). Pia, kuna hurafa ambazo ni za ujanja tu. Wahusika wa ngano hizi mara nyingi huwa ni wanyama. Wakati mwingine mnyama anayedanganya mara nyingi hafanikiwi. Matokeo ya mnyama aliyejaribu kudanganya wakati mwingine yanaweza kumdhuru. Tukichukua kama mfano, Waswahili wana kisa kinachoeleza ujanja wa Mamba dhidi ya Tumbiri. Siku moja Mamba alimlalamikia Tumbiri kwamba yeye ndiye aliyekuwa akimtembelea kila mara. Tumbiri alitoa sababu za kutojua kuogelea lakini Mamba aliahidi kumbeba. Hata hivyo, nia ya Mamba ilikuwa ni kumfanya chakula. Walipofika katikati ya mto, Mamba alimwambia Tumbiri kuwa, kulingana na mila za kwao, mnyama akiwa na rafiki ampendaye, lazima ampatie moyo wake. Kwa hali hii Tumbiri angekuwa na wajibu wa kumpa Mamba moyo wake. Tumbiri alitambua mara moja ujanja wa Mamba na kumjibu kuwa, mnyama yeyote akienda kumtembelea rafiki anayempenda sana haubebi moyo wake. Hivyo basi Mamba aliamua kumrudisha Tumbiri akauchukue moyo wake. Walipofika, Tumbiri alipanda mwembeni na kutunda embe ambalo alimtupia Mamba, lakini Mamba hakuliona kwani lilikuwa limeingia matopeni kabisa. Ndiposa hadi leo, Mamba huzama majini huku akitafuta moyo wa Tumbiri.

Ngano hii ni mfano wa aina ya hurafa ya ujanja lakini pia inaelezea ni kwa nini Mamba huzama majini kila mara. Mamba alijaribu kutumia ujanja kumla "rafiki" lakini Tumbiri naye alitumia ujanja huohuo kujisalimisha kutokana na huyu rafiki mwongo aliyetaka kumwangamiza.

### 2.53 NGANO ZA MAZIMWI

Zimwi ni kiumbe ambaye si binadamu wala mnyama; ni kiumbe aliyebuniwa tu katika fikra za binadamu lakini hana akili kama binadamu. Kwa kawaida zimwi ana uwezo zaidi ya binadamu. Huwa anatisha kwa sura na ni mwovu wa matendo. Ngano hizi Waluhya huziita `amanani', hali Wakikuyu huziita ngano za `marimu' na Wakamba

wana ngano za `maimu'. Hata hivyo kuna mazimwi ambayo huwa yamejigeuza na kuwa na sura nzuri za kibinadamu. Hayo hufanya hivi yakiwa na nia mbaya ya kumwangamiza binadamu.

Ngano za mazimwi huwa na mafunzo tofauti katika jamii. Hata katika jamii, jukumu la ngano hizo hutegemea nia ya mtambaji. Bila shaka ngano hizo huwa na lengo la kuadilisha watu katika jamii na hivyo basi ni jukumu la mtambaji kuona kuwa funzo la ngano hizo limelenga ndipo.

Mbali na kuadilisha jamii, ngano za mazimwi aidha husaidia kuonyesha sifa tofauti za lugha na pia kuifurahisha hadhira. Ngano hizi hutambwa mara kwa mara katika jamii na huwa na mabadiliko mbalimbali kulingana na nia au lengo la mtambaji. Nia kubwa ya ngano hizi huwa ni kuwaburudisha watu.

Katika jamii ya Wakikuyu, ngano za mazimwi huwa nyingi sana na kila mara huwa na mafunzo fulani. Kuna ngano ambayo huonyesha umuhimu wa kuwaheshimu watu wote hata wasio na uwezo mkubwa kwani hata hao mara nyingine huweza kuwa wenye maarifa makubwa. Katika ngano kama hiyo, kuna mhunzi aliyeamua kwenda kwenye uhunzi huku akimuacha nyumbani mkewe mjamzito. Zimwi alipojua hivyo, alikuja kila siku kwa mama huyo, akapika chakula na kula bila kumpa mama huyo hata kidogo. Mama huyo mjamzito alidhoofika sana kwa ukosefu wa chakula. Wakati wa kujifungua ulipowadia, Zimwi yule alimsaidia mama huyo lakini hakumpa chakula chochote kama kawaida. Ilifika wakati ambapo mama huyo alianika mbegu za kutengenezea mafuta, na hapo ndege mmoja alikuja na kula mbegu hizo. Kila siku ndege yule alikuja na kula mbegu hizo. Siku moja yule mama alimwuliza ndege iwapo huyo angeweza kumtuma kwa vile yeye hula mbegu zake kila siku. Ndege alikubali na mama huyo alimtuma kwenye uhunzi na kumfunza wimbo atakaoimba afikapo uhunzini. Ndege alipofika aliimba:

Mhunzi, mhunzi unayetengeza chuma, fanya kazi yako haraka, mkeo amejifungua huku akisaidiwa na zimwi.

Mara ya kwanza wahunzi walimpuuza na kumfukuza ndege huyo. Hata hivyo, huyo ndege aliendelea kuimba, na hatimaye wahunzi walipomsikiza vizuri, waliona kuwa alikuwa na ujumbe muhimu. Mhunzi aliyekuwa amemwacha mkewe akiwa mja mzito

alifunga virago vyake na kuharakisha kwenda nyumbani. Alipofika na kuona jinsi mkewe alivyokuwa amedhoofu, alikasirika sana; na siku hiyo hiyo aliweza kumwua Zimwi alipokuja jioni na, hivyo basi, akaokoa maisha ya mkewe na mwanawe mchanga. Ngano hii yaonyesha kuwa heshima yafaa sana kwani hakuna ajuaye atakayemsaidia kwa vile hata kiumbe duni huweza kutoa msaada fulani, kama vile ndege alivyomwokoa mama huyo na mwanawe.

Mbali na ngano za mazimwi, kuna ngano za pepo. Ngano hizi hufanana sana na za mazimwi kwani, kama mazimwi, pepo hao wakati mwingine hujigeuza na kuchukua sura za binadamu. Wakati mwingine wanaweza kujitokeza katika ndoto au kusikika tu kama sauti. Mazimwi, hali kadhalika, huchukua muundo huu. Kwa hali hii, ngano za pepo tutazichukulia sawa na za mazimwi.

## 2.54 VISAASILI

Katika sura hii, hatutaingilia kwa undani sana maelezo ya visaasili. Hii ni kwa sababu katika sura ya kwanza, tumetoa maana na sifa mbalimbali za visaasili. Kwa vile tayari tuna ufahamu wa utanzu tunaouita visaasili kutokana na maelezo hayo ya awali, tutakuwa tunayarudia tuliyoeleza; jambo ambalo halitafaidi sana kazi yetu. Sura hii ya pili hasa inanuia kuingilia maelezo mafupi kuhusiana na tanzu mbalimbali ili kuonyesha kuwa tanzu hizo ni huru na tofauti, ukiwemo utanzu wa visaasili.

Visaasili, katika kazi yetu, tutavichukulia kama aina ya hadithi za asili; yaani zinazoeleza asili ya mambo na matukio mbalimbali Ulimwenguni. Kama tulivyokwisha eleza hapo awali, visaasili huchukuliwa kama matukio ya kweli yaliyotendeka kale. Visaasili mara nyingi huaminiwa; na mara nyingine huchukuliwa kuwa na sifa za uunguungu na 'utakatifu' (sacred). Visaasili hueleza mambo mbalimbali yanayohusiana na binadamu, asili ya ulimwengu, asili ya kifo, sifa mbalimbali za wanyama na ndege, au asili ya maumbile ya dunia kama vile mito, milima, misitu n.k. (Lusweti 1984:124).

Okpewho (1982:69) anasema kuwa visaasili hueleza ubunifu na uwezo wa kufikiria alionao binadamu. Okpewho aidha amemnukuu Chase (1949:59) asemaye kuwa visaasili ni fasihi na hivyo basi huhusiana hasa na tajriba na uwezo wa ubunifu wa mwanadamu. Akichangia dhana ya visaasili, Kipury (1983:18) anasema kuwa visaasili

hutegemea imani ya hadhira, hii ni kwa sababu iwapo watu wana imani na visaasili vyao bila shaka watashikilia kuwa visaasili vyote wasikiavyo vinaeleza mambo yaliyowahi kutokea, na hivyo yaliyo ya kweli.

Ni muhimu, kufikia hapa, kutaja kuwa hata ingawa tumeeleza tanzu mbalimbali za hadithi katika sura hii, wakati mwingine huwa ni vigumu kutofautisha tanzu hizo. Hii ni kwa sababu visaasili, kwa mfano, katika jamii moja, huweza kuchukuliwa kama mighani au epiki katika jamii nyingine. Hivyo basi, kutokana na mwingiliano huo, iwapo jamii moja itachukulia 'epiki ya jamii nyingine kuwa mighani', haifai jamii hiyo kukosolewa au kudunishwa, kwani kila jamii ina imani na ufahamu wake ambao ni muhimu. Jambo muhimu, hata hivyo, ni kuwa tanzu hizo zote zinasaidia katika maendeleo ya Fasihi Simulizi vilivyo,na fasihi kwa ujumla, na aidha tanzu hizo bila shaka huwa na matumizi muhimu katika jamii husika.

## 2.6 UTAMBAJI HADITHI MIONGONI MWA WAKIKIYU

Hadithi za Wakikuyu huwa na msingi wake katika matukio ya siku baada ya siku. Kwa sababu hiyo, hadithi hizo huwa na uhusiano wa karibu sana na maisha hivi kwamba mambo mengi ya kijamii na elimu kwa ujumla hutoka kwa hadithi hizo.

Jamii ya Wakikuyu ilisifu sana muungano wa jamii, ufanyaji kazi kwa bidii na pia uaminifu miongoni mwa watu. Hivyo basi, mara nyingi hadithi zilikuwa na malengo ya kuelimisha jamii vilivyo.

## 2.61 WAKATI NA MAHALI MWA UTAMBAJI

Hadithi wakati wote zilitambwa jioni au usiku, na wakati mwingine zilitambwa kama upeo wa matendo mengine kama vile uchezaji ngoma na michezo ya kuigiza. Wakati wa jioni ulikuwa mwafaka kwani kila mtu angekuwa nyumbani baada ya shughuli nyingi za mchana. Wakati wa jioni aidha ni wakati uliofaa wa michezo, kutembeleana na wakati huo hakuna yeyote ambaye angekemewa kuwa mvivu.

Katika jamii ya Wakikuyu, mlikuwa na mahali tofauti mwa kutambia hadithi. Mara nyingi jamaa ingekuwa nyumbani katika chumba kimoja na kutambiana hadithi. Wakati mwingine nyanya angewatambia watoto wadogo hadithi hizo. Iwapo nyanya hakuwa anawatambia watoto hao hadithi, yeye angewaarifu kuhusiana na imani, matumaini na kwa ujumla utamaduni wa jamii hiyo. Masomo hayo yalikuwa muhimu sana kwani watoto walitarajiwa kuwa watu waliokubalika na ambao wangeweza kutegemewa maishani. Watoto walifunzwa umuhimu wa bidii kazini, umuhimu wa kuwaheshimu na kuwasaidia wagonjwa na wasiojiweza katika jamii, na aidha walionywa kuwa uvunjaji wa sheria za jamii ungedhuru jamaa hiyo na pia kabila lote kwa jumla. Mlikuwa na hadithi za kueleza yote hayo; na kwa vile zilivyowaburudisha watu, zilihimiza hadhira kutokuwa kama wahusika wa hadithi hizo. Mara nyingine, hadithi za jioni zilikuwa sahili na zilifaa kwa hadhira, lakini mara tu watoto miongoni mwa hadhira walipolala, hadithi tata na ngumu zaidi zilitambiwa watu wazima. Wakati mwingine pia, vijana walihudhuria sherehe za ngoma na nyimbo, huku wakitambiana hadithi zilizowafaa.

Mna wakati ambamo hadithi zilitambwa nje. Vijana hasa walifurahia sana kuketi nje, huku wakiuzunguka moto mkubwa, wakitambiana hadithi na kucheza, wakati huohuo wakichoma mahindi, mihogo na ndizi. Ni katika vikao hivyo ambamo nyimbo mpya, hadithi na ngoma zilibadilishwa kati ya vijana wa kijiji kimoja na kingine. Aliyetamba hadithi kwa mara ya kwanza ndiye aliyemiliki hadithi hiyo; lakini baadaye mlikuwa na uhuru wa kuuhamisha umilikaji huo kwa mtu mwingine aliyeitamba hadithi hiyo kivyake.

## 2.62 SHERIA ZILIZOHUSU UTAMBAJI

Bila shaka, utambaji hadithi ulifurahiwa sana katika jamii ya Wakikuyu. Hata hivyo, utambaji huo ulihitaji kuwepo kwa hadhira iliyokuwa tayari kufurahia na kufaidika kutoka kwa hadithi hizo. Kwa sababu hiyo, kulikuwa na sheria zilizofuatwa ili kuhakikisha kuwa raha ya utambaji haiharibiwi na watu wachache waliopenda kuvunja sheria hizo.

Sheria moja ilihusu upigaji marufuku utambaji wa hadithi mchana. Iliaminika kuwa iwapo sheria hii ingekiukwa, basi ng'ombe, kondoo na mbuzi wote wangetoweka ghafla na hivyo basi kuifanya jamaa husika maskini. Sheria hii hasa ilinuia kuwazuia watu kuacha kazi zao za mchana na kutambiana hadithi.

Utambaji wa hadithi hasa ulifanywa kimpango hivi kwamba, iwapo kundi fulani liliketi katika duara, kila mmoja angetamba kulingana na vile alivyokuwa ameketi katika duara hiyo. Jambo au sheria hii ilihakikisha kuwa kila mtu alimakinika sana, na, pia kuhakikisha kuwa hadithi iliyotambwa haijatambwa na mtu mwingine. Sheria hii aidha iliikataza hadhira kuingilia hadithi kama mtambaji yungali anatamba, isipokuwa ikiwa hadhira inahitajika kushiriki, mfano katika kuimba wimbo fulani.

Sheria zilitekeleza majukumu tofauti ndani na nje ya hadithi. Sheria hizo ziliifunza hadhira, na hasa watoto, umuhimu wa kuwa na mpango na pia kuwa na adabu. Wanajamii waliona raha ya hadithi haingepatikana bila kuwepo kwa sheria. Aidha ukweli kwamba kila mtu katika hadhira alipewa fursa ya kutamba iliwafanya wafikirie kwa haraka sana na kwa busara huku wakikuza uwezo wao wa kukumbuka hadithi walizotamba. Sheria hizo, aidha ziliifanya hadhira iwe na uangalifu zaidi na kukuza hisia zao, na basi uwezo wa utambaji ulikua. Kwa kujishirikisha na wahusika na hali mbalimbali katika hadithi tofauti, hadhira pamoja na watambaji waliweza kuishi vyema. Hadhira iliweza kustahimili hali mbalimbali katika hadithi tofauti mfano huzuni, furaha, woga n.k.

Jinsi utamaduni ulivyoitawala hadhira ndivyo pia ulivyoitawala hadithi yenyewe. Lililokuwa muhimu ni jinsi utambaji ulivyoanza na pia kumalizika, na wala siyo mtu aliyeanza utambaji.

"Ugai itha", ndiyo maneno mawili yaliopendekezwa kwa kuanzia hadithi. Maneno hayo mawili yaliiarifu hadhira kuwa, utambaji ulikuwa karibu kuanza na hivyo basi kuifanya imakinike katika utambaji. Utaratibu huu wa kuanzisha hadithi ni muhimu kama mtindo wa Waswahili usemao:

Mtambaji: Paukwa! Hadhira : Pakawa!

Mtambaji : Paukwa!

Hadhira : Pakawa!

Mtambaji: Hapo zamani za kale paliondokea ....

Au baada ya majibizano ya "paukwa _ pakawa!"mtambaji anaweza kuendeleza hivi:

Mtambaji: Paliondokea chanjagaa,
kajenga nyumba kakaa,
mwanangu mwanasiti,
kijino kama tikiti,
kakujengea kikuta,
na kilango cha kupita.
Hapo zamani za kale .............

Mtindo wa kumalizia hadithi miongoni mwa Wakikuyu huwa: "Rukirika" neno linalomaanisha kuwa "hadithi imemalizika." Mtindo huu ulionyesha kuwa hadithi imekamilika na hivyo basi hadhira ilikuwa na uhuru wa kuyatoa maoni na mapendekezo yao. Maoni hayo yalihusu wahusika na hadithi; mfano hadhira ingesema:

"fisi mjinga vipi", au "mtambaji hodari" na kadhalika. Aidha maoni hayo yalionyesha kuwa maadili ya hadithi hayakupotea tu katika hadithi bali kuwa maadili haya yalifuatwa na kutekelezwa vilivyo hata kama yalikuwa tata vipi. Wakati mwingine hadithi zingemalizika na hapo mtambaji angeongezea maneno yake ya "laana" ili kuwahimiza wengine wapende utambaji hadithi. Mfano mtambaji angesema:
"Uria ataganaga arorio ciara ciake cia maguru na moko ni mbia". Kumaanisha "heri yule asiyependa kutamba aliwe vidole vyake vya miguu na mikono na panya." Maneno kama hayo yangewafanya watu wote wajitahidi vilivyo katika utambaji ili wasije wakapatwa na laana zozote zile.

## 2.7 HITIMISHO:

Tumejaribu kutaja mambo muhimu kuhusiana na utanzu wa hadithi kwa ujumla. Tumeangalia maswala ya hadithi na ngano na kueleza maana ya tanzu hizo. Kulingana na misingi ya Fasihi Simulizi ya Kiafrika, kuna tofauti finyu baina ya ngano na hadithi kiasi kwamba ni vigumu kuwekea mipaka utambulisho huu. Kwa vile nia yetu si kuingilia kwa undani sana uhusiano wa ngano na hadithi, tuliweza kueleza kuwa kimsingi, maudhui ya ngano na hadithi yalikuwa yanahitajika yatoe funzo fulani na wakati huo huo kuburudisha. (Taban Lo Lyong, 1972:1).

Aidha tuliingilia maswala ya kujaribu kueleza tanzu tofauti za hadithi kama vile mighani, epiki, visaasili, hekaya, hurafa, na kuonyesha uhusiano uliopo katika tanzu hizo unaowakanganya watu wengi sana. Tuliona kuwa uhusiano huo upo. Hata hivyo, utanzu mmoja katika jamii fulani huweza kubadilika na kuwa mwingine katika jamii nyingine kulingana na imani za wanajamii husika.

Kuna hali ya tanzu na fani mbalimbali za Fasihi Simulizi kuingiliana au kutumika kwa pamoja. Tanzu za Fasihi Simulizi hushirikiana na kuingiliana katika matumizi ya mbinu mbalimbali zinazozijenga. Ushirikiano na mwingiliano huu ndio unaoleta swala la ugiligili (mwingiliano) wa fasihi na tanzu katika uwasilishaji wa mada zake katika Fasihi Simulizi. Mwingiliano huu ni wa kiasi kikubwa sana kiasi kwamba wakati mwingi inakuwa vigumu kutenga mipaka kati ya baadhi ya tanzu/fani za Fasihi Simulizi.

Si ajabu kupata tanzu kadhaa za Fasihi Simulizi zikizungumzia tukio au jambo moja. Pakawa na ngano, nyimbo, mashairi, masimulizi, tenzi, epiki, mighani na hata semi zilizozungumzia tukio moja katika historia ya jamii moja au jamii nyingi. Hii inatokana na ukweli kwamba, maudhui ya Fasihi Simulizi huibuka kutokana na utamaduni wa jamii inayohusika; huibuliwa kutokana na shughuli za watu, imani zao, mifumo yao na sera zao za kiuchumi, kisiasa, kijamii n.k. Katika hali hii, kila utungo unaotokea katika jamii fulani, katika wakati fulani mahsusi utakuwa na maudhui yanayoibuka kutokana na hali halisi ya maisha ya watu hao wakati huo.

Utenzi wa Fumo Liyongo ni mfano mzuri wa hali hii. Fumo Liyongo, kwa ushujaa wake na sifa zake kubwa, ameshughulikiwa sana katika fani na tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi. Kuhusu ushairi, kwa mfano, kuna kichwa :-

Ushairi: Utenzi wa Fumo Liyongo

Kuhusu nyimbo za Liyongo kuna maelezo :-

Nyimbo: Liyongo pia alitungiwa nyimbo ambazo ziliimbwa kwenye ngoma na sherehe mbalimbali.

Kuhusu hadithi za Liyongo tumeelezwa :-

Hadithi: Yamkini kuna hadithi za Liyongo katika jamii mbalimbali za Waswahili.

Vile vile kuna mwingiliano baina ya mbinu zinazotumika katika utunzi na uwasilishaji. Takriban kila utanzu una mwingiliano, huvikwa mfano katika uwasilishaji wa ngoma ambamo aghalabu kuna matumizi ya nyimbo, matumizi ya ushairi, matumizi ya maigizo, methali, vitendawili na misemo.

Mwingiliano huu wa tanzu na fani za Fasihi Simulizi unaleta ugumu wa kuainisha fani na kuzibainisha katika jamii nyingi. Jamii ya Wakikuyu, kwa mfano, ina jina moja tu "ng'ano" la kueleza utanzu wa hadithi na fani zake katika ngano, mighani, visaasili n.k. Katika jamii nyingi, ni vigumu kubainisha tendi, tenzi/ushairi, kwani mara nyingi tenzi na ushairi huchukuliwa kuwa kitu kimoja. Ni muhimu kutambua ugiligili huu. Hata hivyo maoni yetu ni kuwa mwingiliano huu ni wa kufaana.

Nia yetu hasa, kwa kueleza tanzu mbalimbali za hadithi, ni kuonyesha kuwa utanzu wa visaasili ni huru na una haki zake kama vile tanzu nyingine za hadithi zilivyo. Kwa vile kazi yetu inahusu uhakiki na uchambuzi wa visaasili, bila shaka sura hii imeonyesha kuwa visaasili vinaweza kuhakikiwa kwa vile ni utanzu muhimu wa hadithi kama vile tanzu nyingine zozote zile.

Tumehitimisha sura hii kwa kueleza mambo yaliyo muhimu sana katika utambaji wa hadithi miongoni mwa Wakikuyu. Mambo hayo yameangaza hali ya utambaji hadithi miongoni mwa Wakikuyu, mathalan wakati na mahali mwa utambaji na pia sheria zinazowaongoza watambaji na hadhira katika vipindi vyote vya utambaji.

Hata hivyo, ni muhimu ikumbukwe kuwa jamii ya Wakikuyu imekumbwa na mabadiliko mengi na kwa haraka mno. Mfumo wa kikoloni ulibadilisha mambo mengi ya kiasili. Maendeleo na usasa wa baada ya uhuru vile vile umetoa mchango wake kuupiga kumbo mfumo wa kiasili wa Wakikuyu. Si ajabu kuwa ni nadra sana kupata vikao asilia vya kutamba hadithi, vikiwemo visaasili, na vivyo hazizingatiwi kwa makini sana siku hizi. Kumekuwa na mabadiliko mengi ya kimazingira na kitamaduni vile vile hivi kwamba, kutokana na hayo, watu wengi, na hasa walioelimika, hawatilii maanani visaasili. Aidha, asili ya matukio tofauti huhusishwa na sayansi.

# SURA YA TATU

## 3.0 VISAASILI: MATUMIZI YAKE KATIKA JAMII YA WAKIKUYU

### 3.1 UTANGULIZI

Visaasili ni utanzu wa Fasihi Simulizi na hutekeleza wajibu maalum na muhimu katika jamii. Kwa hivyo, visaasili vimeweza kudumu katika jamii jinsi tanzu nyingine muhimu zinavyozidi kudumu. Tanzu kama vile methali, nyimbo, vitendawili na nyinginezo zimeweza kudumu kutokana na umuhimu wake katika jamii.

Katika umbo la utanzu huo, tumepata kujua kuwa visaasili huhusiana na mambo ya kweli. Visaasili hasa hujaribu kueleza asili na chanzo cha mambo mbalimbali, mengi ambayo huonekana wazi katika jamii. Katika kuvichambua visaasili vya Wakikuyu na kuangalia matumizi yake, tunaweza kuonyesha hasa umuhimu uliopo katika visaasili hivyo. Ni dhahiri kuwa visaasili vina nafasi muhimu katika jamii ya Wakikuyu kama vilivyo katika jamii nyingi za Kiafrika.

Kupitia kwa visaasili, mambo mbalimbali yanayohusika na utamaduni na jamii ya Wakikuyu kwa jumla hupata kufunzwa.

### 3.2. UCHAMBUZI WA VISAASILI KWA KUONYESHA MATUMIZI YAKE

Fasihi Simulizi huwa na umuhimu usio kifani katika jamii nyingi za Kiafrika. Tanzu tofauti za Fasihi Simulizi huwa na majukumu tofauti katika jamii yoyote ile.

Mtaalamu kutoka Marekani, Daktari Joseph Campbell, alinukuliwa katika jarida la Time (January 1972) akisema kuwa visaasili hutekeleza majukumu manne muhimu.

Kwanza, kulingana na Campbell, kupitia kwa jazanda, visaasili huweza kuibua na kudumisha, katika binadamu, hisia za kushangaza (kushtua) na wala sio woga kuhusiana na matukio ya kutisha yapatikanayo Ulimwenguni. Katika jukumu hili la kwanza kulingana na Campbell, twaona kuwa yeye ashikilia kuwa visaasili sio utanzu wa kuogofya binadamu bali hasa huwa na lengo la kuonyesha maajabu ya Ulimwengu. Binadamu hivyo basi hupewa ile hisia ya kuweza kuyakubali maajabu hayo na wala sio kuyaona kama yalivyo na nia ya kuangamiza.

Jukumu la pili muhimu kulingana na Campbell lasema kuwa visaasili humwezesha mwanadamu kupata picha au maono anayoyaelewa kuhusiana na Ulimwengu na hasa kuhusiana na ujuzi wa kisayansi uliopo. Kupitia kwa picha au ishara mbalimbali, visaasili

humweleza binadamu mambo mengi muhimu kuhusu Ulimwengu. Kuhusiana na jukumu hilo la pili, Campbell anajaribu kutoa maoni kuwa visaasili hasa humweleza mwanadamu sababu za matukio mbalimbali ya Ulimwengu.

Jukumu la tatu lililotolewa na Campbell ni kuwa, utanzu huo huendeleza mifumo ya kijamii kupitia kwa sheria za mifumo hiyo na miviga ambayo hasa huwafurahisha na kuwakuza vijana. Kwa mfano nchini India, visaasili hueleza nguvu au uwezo wa makundi fulani yajulikanayo kama "Castes". Ndiposa nchini humo kundi la Brahma huaminika na kukubalika kuwa lenye uwezo zaidi kwa wote kuanzia utotoni. Jukumu hilo, kulingana na Campbell, hasa lahusu mfumo na sheria tofauti za jamii zilizopo. Visaasili hapa hukuza na kudumisha jamii vilivyo.

Campbell pia alitoa jukumu la nne kama kumwongoza mwanadamu hatua kwa hatua maishani, kupitia kwa mifumo ya kisaikolojia isiyoweza kuepukika. Campbell ashikilia kuwa mara nyingi visaasili hutoa mwongozo kwa mwanadamu. Maoni ya Campbell, hivyo basi, yatuonyesha msimamo wake kuhusiana na visaasili kwa ujumla. Kulingana naye, aonelea kuwa wana visaasili hawazui au kutunga visaasili vipya, lakini jambo la muhimu wanalofanya ni kuonyesha kuwa kuna upungufu fulani pasipokuwa na visaasili. Wataalamu hao wa visaasili wana maoni kuwa "mtu wa kisasa" hawezi akaepuka visaasili mradi ana matumaini, imani na hisia za hali ya juu kuliko wanyama wengineo wote.

Kulingana na Campbell, visaasili ni sehemu muhimu sana katika maisha, na bila visaasili hivyo, basi maisha yatakuwa hayajakamilika vilivyo. Visaasili ni vifaa muhimu sana katika kuendeleza maisha ya mwanadamu.

Visaasili, kama tulivyotangulia kusema hapo awali, ni utanzu unaotekeleza majukumu muhimu sana katika jamii yoyote ile vipatikanamo.

Ni muhimu kutaja pia kuwa tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi huweza zikawa na majukumu yanayolingana. Mfano, mtu anaweza kutumia hadithi, vitendawili, au methali miongoni mwa tanzu nyingine za Fasihi Simulizi, katika kujieleza. Hivyo basi, visaasili huenda vikawa na majukumu sawa na utanzu mwingine katika jamii; kwa mfano nyimbo. Hata hivyo jambo muhimu ni kuwa, hata iwapo majukumu hayo yanaweza kulingana, kila utanzu huweza kutekeleza majukumu yake vilivyo na hivyo basi kuweza kuendelea ipasavyo. Kwa hivyo majukumu tutakayojadili ya visaasili huenda yakawa yanalingana na majukumu ya tanzu nyingine za Fasihi Simulizi. Hakuna utanzu wa Fasihi Simulizi unaoeweza kudai uwezo

wa kutekeleza majukumu fulani katika jamii, kwani mwingiliano wa tanzu hizo vilevile huonyesha mwingiliano kati ya majukumu yake.

Katika kujadili majukumu yanayotekelezwa na visaasili katika jamii ya Wakikuyu, tutayapanga (majukumu hayo) katika vijisura tofauti huku tukieleza kisaasili kama thibitisho la jukumu tutakalokuwa tunajadili.

## 3.3. VISAASILI KAMA KIFAA CHA KUELIMISHA JAMII

Kabla kuanzishwa kwa mifumo ya elimu ya magharibi, Wazungu wengi walidhani kuwa jamii za Kiafrika hazikuwa na elimu yoyote. Wazungu hao walihusisha elimu na ujuaji wa kusoma na kuandika na, kwa vile Waafrika hawakujua kuandika au kusoma, walichukuliwa kuwa hawakuwa na elimu. Hoja hiyo, bila shaka, ilikuwa ya kupotosha kama vile Wazungu wenyewe walivyogundua baadaye.

Jamii nyingi za Kiafrika zilikuwa na njia za kuelimisha wanajamii kuhusiana na mambo tofauti tofauti. Visaasili vilivyotambwa katika jamii ya Wakikuyu viliweza kufahamisha na kuwaelimisha kuhusiana na asili yao, asili ya kifo, asili ya upinde wa mvua na kadhalika.

Watoto wa Kiafrika walifanywa kuamini kuwa visaasili na tanzu nyingine zikaribianazo navyo, kama vile mighani, huwa ni habari za kweli au habari ambazo hudhaniwa kuwa za kweli.

Tukishughulikia kisaasili kihusianacho na asili ya Wakikuyu kama mfano, twaona kuwa kisa hicho huwaangazia wanajamii mambo muhimu yanayowasaidia katika kuielewa jamii yao vilivyo.

Kulingana na kisaasili hicho, twaelezwa kuwa wakati wa mwanzo wa Ulimwengu, Gikuyu, aliyekuwa mwanzilishi wa kabila hilo, aliitwa na Mugai au Murungu. Mugai alimpa Gikuyu sehemu yake ya ardhi, mabonde, mito, misitu, wanyama na mambo mengine mengi yaliyopatikana Ulimwenguni.

Wakati huo huo Mugai aliumba mlima mkubwa sana na kuuita Kiri-Nyaga (Mlima wa Murungu). Mlima huo ulikuwa kiti cha Mugai, alichokitumia kupumzikia alipokuwa matembezeni ya kuukagua Ulimwengu.

Mugai alimwita Gikuyu mlimani ili amuonyeshe vitu vyote alivyokuwa ameumba. Gikuyu akiwa juu ya mlima, Mugai alimwonyesha miti fulani (Mikuyu) katikati mwa nchi.

Hapo alimuamuru Gikuyu ashuke mlimani na kujenga makao yake katika mahali alipomwonyesha na Gikuyu alipaita mahali hapo Mukurwe-Wa-Gathanga.

Mugai alimwambia Gikuyu kuwa kila mara alipokuwa na mahitaji yoyote angepaswa kufanya kafara, na kuinua mikono yake kuelekea Kiri-Nyaga. Mugai alimwahidi Gikuyu kuwa akiabudu na kutoa kafara mahitaji yake yangetekelezwa. Mugai pia alimletea Gikuyu msichana mrembo wa kuoa aliyeitwa Mumbi. Gikuyu na Mumbi waliishi pamoja na kupata wasichana tisa. Gikuyu alimwomba Mugai na kutoa kafara huku akiomba apewe wanaume tisa wa kuwaoa wasichana wake. Mugai alimtekelezea hoja, na basi kutoka kwa moto aliokuwa ameuwasha Gikuyu wakati wa kutoa kafara, mlitokea wanaume tisa ambao walikaribishwa kwa furaha kubwa. Hivyo basi wasichana wa Gikuyu na Mumbi waliokuwa Wanjiru, Wambui, Wanjiku, Wangari, Waceera, Wairimu, Wangui, Wangechi, Waithera na Mwethaga au Warigia wote walipata waume.

Gikuyu, Mumbi na watoto wao waliishi raha mustarehe kwenye nchi waliyopewa na Mugai. Gikuyu na Mumbi walipoaga dunia baadaye, kila binti pamoja na watoto wake aliunda ukoo chini ya jina lake. Kwa njia hiyo, koo tisa za Agikuyu ziliundwa. Koo zote tisa ziliungana na kuishi kwa amani, na hivyo kundi lote hilo lilipewa jina "Ruriri rwa Mbari ya Mumbi" au kama lijulikanavyo leo kama "Nyumba ya Mumbi", kwa maana kuwa kabila lote la Wakikuyu lingepata urithi wake kupitia kwa upande wa mama.

Wakati wowote Wakikuyu walipotaka kuomba, walielekeza nyuso zao Mlimani Kirinyaga, wakainua mikono yao juu na kutamka maneno matakatifu;
"Thaai thathaiya Ngai thaai".

Baada ya hivyo wangeendeleza sala zao kwa kusema:

Watoto thaai uthaai
Mvua thaii uthaii
Ng'ombe thaii uthaii
Mbuzi thaii uthaii
Thaai thathaiya Ngai thaai

Maneno hayo yalitamkwa kumaanisha kuwa viumbe vyote vilivyotoka kwa Mungu, kwa mfano watoto, ng'ombe mbuzi na kadhalika, vilikuwa vitakatifu.

Hapo wangetaja mahitaji yao mfano kama ni mvua, mavuno, baraka na kutamka tena maneno hayo matakatifu. Kila mara baada ya sala, walitarajia kupata majibu yake ama siku hiyo au siku chache baadaye.

Kisaasili hiki kinatekeleza majukumu muhimu sana ya kuelimisha jamii ya Wakikuyu. Hii ni kwa sababu kinaeleza jinsi kabila la Wakikuyu lilivyoanzishwa na kuendelea hadi lilivyo leo. Vile vile, kisaasili hiki kinatetea umilikaji wa ardhi katika kabila la Wakikuyu kwani, kulingana na kisaasili chenyewe, Mungu (Mugai) ndiye aliyemwita Gikuyu na kumwonyesha nchi yake, ambayo baadaye ilimilikiwa na vizazi vyake. Jambo hili ni muhimu sana hasa iwapo tuna haja ya kueleza mambo ya kuwepo kwa mashamba miongoni mwa Wakikiyu. Wakikuyu, hivyo, kwa vile wana imani kuwa walipewa ardhi yao na muumba wao, si ajabu kwamba kila mara huwa tayari kabisa kupigania nchi yao na kutetea ardhi hiyo vilivyo, kwani kwao hiyo ni haki yao.

Katika kisaasili hicho pia twapata kujua asili ya jina la kabila hilo. Jina "Mbari ya Mumbi" yaani "ukoo wa Mumbi" ni jina ambalo hutumiwa sana kueleza Wakikuyu. Aidha kabila hilo lilijulikana kama Agikuyu kutokana na jina Gikuyu, aliyekuwa mwanzilishi wao. Gikuyu alilipatia kabila hilo jina lake kwani yeye ndiye aliyekuwa" baba" ya watu wa kabila hilo. Kutokana na hali ya kuwaita Wakikuyu jina la baba yao, twapata kujua kuwa hapo ndipo mfumo wa upeanaji majina miongoni mwa Wakikuyu ulipotoka. Twaona kuwa hata sasa, Wakikuyu huwaita watoto wao wa kwanza majina ya baba na mama zao ili kuendeleza mtindo walionzishiwa na Gikuyu na Mumbi.

Jambo jingine muhimu linalofunzwa na kisaasili cha asili ya Wakikuyu ni kuhusiana na ibada na utoaji wa kafara. Kulingana na kisaasili hicho, Mugai alimpa Gikuyu amri kadha kuhusiana na jinsi ya kutoa kafara. Gikuyu alipaswa kuchinja kondoo na kumwaga damu ya mnyama huyo katika shina la "Mkuyu"au "Mugumo"; na kisha achome nyama ya mnyama huyo chini ya mti huo ili imfikie Mugai. Aidha, wakati huo huo, Gikuyu alipaswa kuinua mikono yake juu na kuelekea mlima wa Kiri-Nyaga. Hapo tunaona jinsi "Mugumo" au "Mkuyu" ulivyopata umuhimu kama mti mtakatifu miongoni mwa Wakikuyu. Kwa njia hiyo hiyo, twapata kuelewa ni kwa nini Mlima wa Kirinyaga ulionekana kama mahali muhimu, hasa wakati wa ibada na utoaji kafara. "Mugumo" au "Mkuyu"haungekatwa na yeyote, na

kosa la kukata mti huo liliadhibiwa kwa kifo. Ijapokuwa imani hii inaendelea kufifia siku hizi, bado huwa ina mashiko sana miongoni mwa watu fulani, na hasa wazee.

Kisa cha asili ya Wakikuyu pia huelimisha wanajamii hiyo kuhusiana na mifumo ya kijamii. Jamii ya Wakikuyu, kulingana na kisaasili hicho, ilitawaliwa na wanawake. Hii ni kwa sababu Gikuyu na Mumbi waliwazaa wasichana na hawakupata wavulana wowote. Gikuyu aliwaruhusu wanaume alioletewa na Mungu kuwaoa binti zake kwa masharti fulani. Wanaume hao waliambiwa kuwa wangeishi nyumbani mwa Gikuyu, jambo ambalo walikubali bila pingamizi.

Kisaasili hicho, aidha, chatueleza ni kwa nini baadaye jamii ya Wakikuyu ilibadilika na kutawaliwa na wanaume. Mapinduzi hayo yalitokea wakati wanawake, na hasa viongozi wa kike, walipotungwa mimba.

Imani kuwa wazazi wa kwanza wa Wakikuyu walikuwa na mabinti tisa ni thibitisho tosha kuelezea ni kwa nini jamii ya Wakikuyu huwa na koo tisa ambazo huhusishwa na majina ya mabinti tisa wa Gikuyu na Mumbi. Ndiposa kuna koo zijulikanazo kama Anjiru, Ambui, Achera, Anjiku, Angari, Airimu, Angui, Angechi, Aithira na Arigia. Ni dhahiri kwamba majina ya koo hizi yanafanana moja kwa moja na majina ya watu binafsi kama vile Wanjiru, Wanjiku, Wambui na kadhalika.

Aidha kisaasii hiki kinaeleza jinsi jamii ya Wakikuyu inayoelimishwa kuhusu mahali panapozingatiwa au kuaminiwa kama mahali asilia pa watu hao. Kila Mkikuyu hujua au huwa amesikia kuhusu Mukurwe wa Gathanga; kwani, kulingana na kisaasili hiki, mahali hapo ndipo Mugai alipomuamuru Gikuyu ajenge makao yake. Hivyo basi mahali penyewe huchukuliwa kuwa makao asilia ya Wakikuyu. Hapo twaona kuwa Mukurwe wa Gathanga huchukuliwa na Wakikuyu kama mahali patukufu, kwani ndipo palipochaguliwa na Mugai na kupendekezewa Gikuyu. Mahali hapo palipewa jina hilo na Gikuyu na Mumbi waliokuwa wazazi wa kabila la Wakikuyu.

Kisaasili cha chanzo cha kabila la Wakikuyu chaonyesha kuwa Wakikuyu, kama yalivyo makabila mengi ya Kibantu, waliona au huona kabila lao kama kiwakilishi cha maisha ya wanadamu wote. Mtu mmoja, Gikuyu, anachukua mahali pa `Adamu' katika kisaasili cha Wasemitiki, na kuonyesha kama aliyeleta uhai wa watu Ulimwenguni. Gikuyu ndiye mtu wa kwanza na baba wa kabila lote la Wakikuyu; na kulingana na kisaasili chenyewe, mtu ni kiumbe aliyekuwa na uwezo wa kuwasiliana na muumba wake wakati wowote alipokuwa na mahitaji fulani.

Wakati Mugai alipoona kuwa dunia ilihitaji watu wengi zaidi, alimwita Gikuyu na kumpa mke na pia ardhi nzuri iliyokuwa imenawiri. Hapa twaona kuwa, kuanzia mwanzo, Gikuyu anaruhusiwa kuwa na uamuzi huru unaomwezesha kuvitawala vizazi vyake vya baadaye na, hivyo, kuonyesha hali inavyopaswa kuwa kwa mwanamume wa Kikikuyu. Umuhimu wa aina hii ya uumbaji ni kuwa mtu anaibuka katika kisa hiki kama kiumbe muhimu anayejenga jamii na kutengeneza sheria ambazo zinayafaa mahitaji yake. Kwa njia hiyo, kisaasili cha asili ya Wakikuyu kimezungukwa na hisia kuwa Mugai ni mtukufu na ana uwezo usio kifani, na, pia, wakati huo huo, ana uwezo wa kujidunisha hadi kiwango cha kugawa mali baina ya wanadamu. Iwapo Mugai anataka kudumisha utukufu na uwezo wake usio wa kawaida, ni lazima aupoteze ule uhusiano wa karibu sana na mwanadamu na pia aache safari zake za kutembea ardhini aliyompa Gikuyu ili kuikagua. Wakikuyu walijua kuwa Mugai aliishi kwenye mlima wa Kirinyaga na hivyo basi ukweli kuwa wangeweza kumfikia na kuwasiliana naye kila mara uliwafanya wasimuogope au kumtukuza sana kwa vile Mungu huyo alikuwa karibu sana nao. Kwao Wakikuyu, mbingu na dunia zilikuwa ni kama mahali sawa. Jinsi hiyo basi ndiyo inayowafanya Wakikuyu wahusishe kifo na hali ya Mugai kutaka kukatisha uhusiano wa ana kwa ana na wanadamu.

## Visaasili vya Kifo

Visaasili vya kifo miongoni mwa Wakikuyu ni mfano mwafaka wa visa vinavyoelimisha jamii. Kulingana na jamii ya Wakikuyu, kuna visa viwili vielezavyo asili ya kifo.

Inasemekana kuwa miongoni mwa Wakikuyu, watu walifufuka mara tu walipokufa. Siku moja Mungu (Mugai) alimtuma Kinyonga akawaambie watu kuwa hawangekufa tena. Ngai alitaka watu waongezeke na kuujaza Ulimwengu wote. Hivyo basi, Ngai akamwambia Kinyonga:

`Nenda ukawaambie watu kuwa kuanzia sasa hawatakufa tena. Watu hao watapata watoto na dunia itajaa'.

Kinyonga alianza kutembea pole pole sana, na kwa hatua ndogo sana. Yeye hakutaka udongo uporomoke, na hivyo basi, alionelea ni vizuri atembee pole pole. Alipofika duniani aliwakuta watu tayari kabisa kuupokea ujumbe aliowaletea. Kisha, Kinyonga alianza kuwapa watu ujumbe wake na kusema

"Ni-ni-ni lia-a-ambi-mbi-wa-a ......

ni-ni-nilia-a-ambi-mbi-wa-a" ......

Hapo akawa anayarudiarudia maneno hayo bila kueleza ujumbe huku wakingoja kwa hamu ili wapate kuusikia bila kufanikiwa.

Wakati watu walipokuwa bado wanangoja ujumbe wa Kinyonga, Ngai alikasirika sana na kumtuma ndege aendaye kasi sana kama iaminivyo jamii ya Wakikuyu ajulikanaye kama "Nyamindigi". Ndege huyo aliharakisha sana, na alipofika duniani, alimkuta Kinyonga hajamaliza ujumbe wake.

"Nini unachowaambia watu? `Ni-li-ni-li-a-a-a-mbi-wa-a-, mb-ii-wa-a, "kwani watu hawa hawakuambiwa kuwa wataendelea kufa na kutoweka duniani?" ndege aliuliza. Ndege huyo alipoyamaliza maneno yake alipuruka na kwenda zake.

Kinyonga aliachwa huku akiwa na wasiwasi mwingi, na aliona kuwa aliwakosea watu sana kwa kutowapa ujumbe wake haraka ilivyotakikana. Tangu siku hiyo watu walianza kufa na hawakufufuka tena wala kurudi tena duniani.

Watu walipomuona Kinyonga walimdhihaki na kumulaani huku wakisema "Kinyonga, wewe utazidi kukonda na kukonda na sisi tutaendelea kunenepa na kuwa na afya nyingi". Kinyonga, kutokana na laana hiyo, aliendelea kukonda siku baada ya siku na hatimaye akafa. Huo ndio mwisho wa kisaasili hicho.

Kulingana na kisaasili cha pili miongoni mwa Wakikuyu kuhusiana na kifo, Riua (jua) alikuwa mfalme wa Ulimwengu na aliishi juu ya mlima wa Kirinyaga. Siku moja Riua alitembea duniani na kumpata mwana wa kiume wa mfalme akiwa amefariki. Mfalme wa

dunia alimwambia Riua kuwa kifo kilikuwa ni tatizo kubwa sana miongoni mwa watu. Riua, mfalme, alisema:

> "Nipe tarishi nitakayepatia dawa kutoka mlima wa Kirinyaga. Dawa hiyo itawekwa motoni, na watu watakaponusa mvuke wake hawatakufa tena".

Mfalme wa dunia mara moja alimchagua Kindi, na wanawake walipomuona Kindi amejipamba tayari kwenda kwa mfalme Riua, walimshangilia kwa vigelegele:

> "Aririririiii-riii, Aririririii-riii-i"

Kindi alifurahi na kuwajibu "Hii-hii!- Yii!-hi!" na kwenda zake pamoja na mfalme Riua kuelekea Mlima Kirinyaga.

Wakati Kindi alipokuwa anatoka Kirinyaga, huku akiwa amebeba dawa aliyopewa na Mfalme, alikutana na Fisi aliyekuwa akielekea Kirinyaga kuchukua dawa hiyo kwa matumizi yake ya kibinafsi. Alimuona Kindi na kujawa na wivu mkubwa. Hapo basi Fisi alimshambulia Kindi, akamnyang'anya dawa aliyokuwa anabeba na kuitupa katika mto uliokuwa umejaa maji.

Kindi alijawa na wasiwasi, na hapo basi, alirudi tena kwa Mfalme Riua na kumwambia yaliyokuwa yamefanywa na fisi. Mfalme aliposikia hayo, alikasirika sana na kumwambia:

> "Wewe Kindi, ulishindwa kutekeleza wajibu wako vilivyo kwa watu. Kwa hivyo ninakulaani kuwa hutaishi tena na watu bali utaishi shimoni kila mara. Na huyu Fisi, kuanzia sasa amekuwa adui mkubwa wa watu"

Hivyo basi watu waliendelea kufa kwa vile hawakupata dawa ya kujikinga dhidi ya kifo. Hivi ni visa viwili vinavyoeleza jinsi kifo kilivyofika katika nchi ya Wakikuyu.

Katika kisaasili cha kwanza, hatuambiwi ni kwa nini Mugai alibadilisha fikra zake na kumtuma "Nyamindigi" na ujumbe wa kifo. Hisia za Mugai hazieleweki kabisa na tunashangaa ni kwa nini alikosa ustahimilivu zaidi dhidi ya binadamu, aliyekuwa ni mpokezi tu wa ujumbe. Pengine Mugai hakupendelea ongezeko kubwa la watu na hivyo basi akaona kuwa kifo kingepunguza ongezeko hilo.

Ukweli kuwa mwanadamu aliambiwa kuwa atakufa na kutoweka Ulimwenguni kabisa waleta hoja muhimu ya kuzingatia. Fikra kuhusu pepo walio hai wanaohusisha waishio na wafu hutoka wapi? Kama tulivyoona, Wakikuyu waliamini, na bado huamini,

kuwa wafu hawakuwa wamekufa bali walibadilika wakawa pepo na, hivyo basi, walikuwa wanajamii walioshiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii. Ni mwanadamu pekee aliyepata maelezo ya; "Je roho ya mtu inaweza kufa wakati mwili umekuwa dhaifu kuweza kuistahimili?" Hili ni jambo ambalo mwanadamu anaonelea haliwezekani. Kwa sababu hiyo, Wakikuyu walifurahi kuamini kuwa pepo au roho za wafu ziliachwa duniani wakati mwili ulipokufa.

Katika kisaasili cha pili kuhusiana na kifo ni Riua (jua) na wala sio Ngai aliyewatawala watu. Yeye (Ruia) kama vile Ngai, aliishi katika Mlima Kirinyaga na alikuwa na dhima ya Mfalme na wala sio mwenye ardhi kama ilivyo katika kisaasili cha kwanza. Ulinganifu uliopo katika visa hivi viwili ni wa kawaida kwani, kwa Wakikuyu, jua ni ishara ya utukufu, kama lilivyo kwa jamii nyingi za Wabantu. Ngai, kama tulivyokwisha kuona, ni mwenye utukufu huo. Kinachoshangaza, hata hivyo, ni kuwa muumba mkarimu wa Ulimwengu anaweza, badala ya kuwapa watu wake uhai, kuwaletea kifo. Au je, huenda mwanadamu alikuwa muovu sana na hivyo akaletewa maafa hayo? Jambo hilo haliwezekani, kwani hatuonyeshwi, katika visa hivyo, wakati wowote mwanadamu alipokosa kumtii muumba wake. Wakati mwanadamu anapokosa kutii, anakosa kuwatii wanadamu wenzake na, hivyo basi, huhukumiwa kwa hayo.

Jambo la kutilia maanani katika kisaasili cha pili ni kuwa kifo tayari kinawamaliza watu duniani wakati usaidizi wa Mfalme unapotafutwa alipokuwa katika safari zake za ukaguzi. Kutokufa si jambo linalopaswa kuchukuliwa kwa urahisi, na Mfalme (Riua) anaonekana tayari sana kuwa na sababu za kuondoa kifo katika jamii. Watu wote wanaadhibiwa; wakosaji na wasiokosa, wanaadhibiwa. Adhabu ya Mfalme inaonekana wazi na, ni thibitisho la hasira yake kwa wanadamu.

Visaasili hivi vinatuelimisha kuwa, haki yafaa kutekelezwa kila mara. Haki hii inafanana na sheria za Wakikuyu ambazo hazijaandikwa zisemazo kuwa maisha yafaa kulipwa kwa maisha mengine. Ni haki isiyopendelea upande wowote na inamwepusha Mungu kabisa kwani katika visaasili hivi mwanadamu anajaribu kujitatulia matatizo yake bila usaidizi wa Mungu. Hali ya tanzia inadunishwa kabisa na inajitokeza tu pale mwanadamu anapokuwa ameshindwa kabisa kuepuka athari fulani zinazomkumba.

Haki yasisitizwa, na, ndiposa twaona kuwa, kwa vile Fisi alivyomkosea Kindi katika kisaasili cha pili, wote wawili wanaadhibiwa vilivyo. Visaasili hivi ni msingi thabiti wa haki

iliyopo hata sasa katika jamii ya Wakikuyu. Kenyatta (1938:304) atoa maelezo yahusuyo adhabu ilivyotolewa kwa wachawi na wauaji kama mfano wa kuonyesha jinsi haki ilivyodumishwa miogoni mwa Wakikuyu. Asema Kenyatta kuwa, iwapo wahalifu hao wangepatikana katika jamii, wangepangiwa siku ya kuuawa. Hivyo basi, siku hiyo ilipoamuliwa, wazee na watu wengine katika jamii wangeungana na kufanya mviringo na kisha muuaji huyo angepelekwa chini ya ulinzi mkubwa wa "njama ya ita". Hapo muuaji angepewa mbuzi mdogo wa kiume kutoka kwa mbuzi wake na kulazimishwa kumuua, ishara ya kuonyesha kifo chake mwenyewe. Muuaji huyo angemwagiwa mwilini damu ya mbuzi huyo huku watu wakiwa kimya kabisa. Wimbo ungeimbwa uliosema kuwa muuaji au mchawi lazima angeuawa jinsi alivyokuwa ameua. Baadaye muuaji angefungwa kwa majani ya ndizi kuanzia kichwani hadi miguuni na moto ungewashwa. Mchawi au muuaji alipowashiwa moto angelindwa hadi achomeke kabisa. Hivyo basi haki ilidumishwa na ingali inadumishwa vilivyo katika jamii ya Wakikuyu wa kuwaadhibu wahalifu vilivyo.

Visaasili vya kifo aidha vinaelimisha jamii kuhusiana na umuhimu wa kuwa na utiifu na kutekeleza wajibu wowote ule haraka iwezekanavyo. Kisaasili cha kwanza hasa chaonyesha hasara itokanayo na uvivu na ulegevu wa mtumwa aliyekuwa Kinyonga. Kinyonga alipotumwa na Mungu alitembea pole pole sana na hakufahamu iwapo ujumbe huo ulikuwa muhimu au la. Alichojali zaidi ya maisha ya mwanadamu ni udongo aliotahadhari asiuporomoshe. Kutokana na kutojali kwake, twaona kuwa hasara kubwa zaidi ilipatikana. Upole na ulegevu wake uliwaletea wanadamu kifo ambacho kwa kweli kinaogopwa na kuwakabili hadi leo. Kinyonga alimkasirisha Mungu sana, ndiposa Mungu akamtuma ndege aliyekuwa na haraka zaidi katika kuyafanya mambo yake. Haraka ya "nyamindigi" ndiyo ilimfanya Mungu abadilishe ujumbe wake kwa kuona kuwa ujumbe huo ungefika haraka ilivyohitajika. Nyamindigi ni mfano mzuri wa jinsi watu wapasavyo kuwa, yaani ni bora kila mara kuwa na jitihada na bidii katika yote tuyafanyayo.

Funzo jingine katika visaasili vya kifo ni umuhimu wa kutokuwa na wivu miongoni mwetu. Katika kisaasila cha pili twaona kuwa wivu wa Fisi ndio hasa uliofanya kifo kudumu katika jamii ya Wakikuyu. Fisi alimuonea Kindi wivu kwa sababu yeye (Fisi) huenda hakuchaguliwa na Mfalme Riua kuwa tarishi wa kuwapelekea wanadamu dawa ya "kufukuza kifo". Iwapo pengine Fisi angechaguliwa kupeleka dawa hiyo, yeye angeifikisha. Kwa vile ni

mkubwa zaidi na ana nguvu zaidi kuliko Kindi, yeye alimdharau sana na kuamua kumshambulia. Hapo basi Fisi aliinyakua dawa aliyokuwa amebeba Kindi na kuirusha kwenye mto. Jambo hilo, bila shaka, lilimkasirisha sana Mfalme Riua na akawalaani Kindi pamoja na Fisi, huku kifo kikiendelea kuwasumbua wanadamu. Ubaya wa wivu wa Fisi ndio unaoendeleza kifo katika jamii. Iwapo Kindi angefika alikotumwa salama na kuifikisha dawa aliyopewa na Mfalme, bila shaka yeye angekuwa mwokozi wa waja kwani kifo kingetoweka kabisa. Wivu baina ya watu katika jamii husababisha majanga mbalimbali, na hivyo basi, kutokana na kisaasili hiki, twaonyeshwa wazi umuhimu wa kuepuka wivu kwani wivu kila mara huandamana na hasara fulani inayotokea baadaye.

Uhusiano baina ya mwanadamu na muumba wake ambaye ni Mungu pia unaangaziwa katika visaasili vya kifo miongoni mwa Wakikuyu. Mungu na mwanadamu inaelekea walikuwa na uhusiano mzuri sana hapo mwanzoni. Ndiposa katika kisaasili cha kwanza twaelezwa kuwa wanadamu walifufuka mara tu walipokufa. Kutokufa kwao ni thibitisho kuwa wao walitenda mambo yaliyomfurahisha Mungu na hivyo basi Mungu akafurahia kuishi kwa mwanadamu Ulimwenguni. Huenda ikawa mwanadamu alianza kutenda maovu yaliyomkasirisha Mungu. Mungu, hapo basi, hakusita kumtuma Kinyonga kwa mwanadamu akiwa na ujumbe kuhusu kutokufa kabisa. Pengine Kinyonga alipokuwa bado anagugumia ujumbe wake, Wanadamu walitenda maovu zaidi yaliyomkasirisha Mungu zaidi na kumfanya amtume ndege "Nyamindigi" na ujumbe wa kifo. Yafaa wanadamu wajihadhari na kuendesha maisha yanayopendeza mbele ya Mungu, kwani yeye anao uwezo wa kufanya jambo lolote. Huenda iwapo wanadamu watampendeza Mungu, yeye (Mungu) atawatumia mjumbe atakayekuja kutangaza mwisho wa kifo, na hivyo basi watu waendelee kuishi daima dawamu.

Aidha, makao ya wanyama na wanadamu, kulingana na visaasili, ni jambo linalozusha mjadala. Kulingana na Kisaasili cha kwanza, Mungu alimtuma Kinyonga duniani. Inasemakana kuwa Kinyonga hakutaka kuporomosha udongo duniani, jambo ambalo lilimlazimu atembee pole pole sana. Ni dhahiri kuwa Nyamindigi alikuwa na mabawa na hakutembea kwa miguu. Hali hiyo ilimwezwsha Nyamindigi kuruka kwa haraka na kufika duniani haraka, jambo ambalo lilimwezesha kumpata Kinyonga kama bado hajawapatia wanadamu ujumbe. Kulingana na kisa hicho, ni wazi kuwa Mungu aliishi pamoja na

wanyama mbinguni ilihali wanadamu waliishi duniani. Katika kisa cha pili, twaona kuwa Kindi alitumwa na Mfalme Riua duniani, na hivyo ni dhahiri kuwa makao yake (Mfalme Ruia) na pia ya wanyama yalikuwa mbinguni. Visa hivi vyaonyesha kuwa, wanyama walikuwa na uhusiano wa karibu zaidi na Mungu, tofauti na uhusiano uliokuwepo baina ya Mungu na wanadamu. Ili wanadamu wapate uhusiano wa karibu na mzuri na Mungu, ingewabidi kuwa na matendo mazuri mbele ya Mungu. Uhusiano kama huo, hivyo, ni muhimu na, iwapo wanadamu wangekuwa watiifu kwa Mungu, basi wao wangekuwa huru kuwasiliana na Mungu.

Kutokana na visaasili tulivyoeleza, ni dhahiri kuwa utanzu huo ni muhimu katika kuelimisha jamii. Visaasili ni muhimu kama zilivyo tanzu nyingine, mfano vitendawili, methali na nyimbo, ambazo mara nyingi hufunzwa ili kuonyesha busara na mafunzo fulani yanayohitajika katika jamii. Mfano, vitendawili huonekana kama muhimu sana katika kufunza thamani za watu. Vivyo hivyo, visaasili vingi vimetambuliwa kama muhimu katika kuwaelimisha watu katika jamii kuhusiana na mambo mbalimbali.

## 3 .4 VISAASILI KAMA NJIA YA KUTAWALA JAMII

Kuna tanzu fulani za Fasihi Simulizi kama vile hadithi na nyingine ambazo husaidia katika ujenzi wa asasi za kijamii na miviga. Tanzu hizo hueleza sherehe, mifumo, miviga na mazingaombwe katika jamii. Visaasili ni utanzu ulio muhimu sana na ambao unaweza kueleza hasa mambo ya kidini na miviga katika jamii yoyote ile. Katika jamii nyingine, visaasili, mighani, na utamaduni hutawala mambo mbalimbali katika jamii kama vile haki za umiliki wa ardhi, utawala, na vyeo katika jamii na vile vile kutetea kuwepo kwa mali baina ya watu katika jamii.

Kulingana na visaasili kadha ambavyo huaminika katika jamii, jamii ya Wakikuyu huweza kutenda mambo fulani kimpango kulingana na visa hivyo. Utanzu huo huweza kuitawala jamii na kuwaongoza waliomo katika kuelewana na kuwa na utaratibu fulani ili waweze kuishi maisha mema.

Kuna kisa miongoni mwa Wakikuyu kinachoeleza asili ya uongozi, na kinalingana sana na kile tulichoeleza cha asili ya Wakikuyu. Inasemekana kuwa wakati wanawake

walipokuwa na vyeo vikubwa katika jamii, wao (wanawake) walikuwa wakali na waliwapiga wanaume bila huruma yoyote. Vile vile hawakuwa waaminifu kwa wanaume na mwanamke mmoja angekuwa na waume wengi. Hata hivyo, wanaume walilazimishwa kuwa waaminifu, na, yeyote aliyepatwa akizini alihukumiwa kifo. Mbali na hukumu ya kifo, wanaume waliteswa sana na kunyimwa haki zao.

Wanaume walikasirishwa sana na utawala wa wanawake. Hivyo basi walipanga mapinduzi dhidi ya utawala wa kiimla wa wanawake. Hata hivyo, wanawake walikuwa na nguvu zaidi kuliko wanaume wakati huo na vile vile walikuwa hodari sana katika upiganaji vita. Wanaume, kwa vile waliogopa mapinduzi hayo, waliamua kuwa wakati mwafaka wa mapinduzi ungekuwa kama wanawake wengi, na hasa viongozi, walipokuwa wajawazito.

Wanaume walifurahia uamuzi huo kwani walikuwa na hamu sana ya mapinduzi hayo. Wanaume walikutana kisiri na kupanga siku ya mapinduzi. Muda mfupi baadaye, wanaume walianza kuwaomba viongozi wanawake waonane nao kimwili. Wanawake walihadaiwa na wakakubali kuonana na wanaume hao kimwili bila ya kujua mpango uliokuwepo wa mapinduzi.

Wanaume, baada ya kumaliza matendo yao, walingojea matokeo. Baada ya miezi sita, wanaume waliona kuwa mpango na matendo yao yalikuwa yamefaulu. Mara moja waliunda vikundi na kisha wakatekeleza mapinduzi yao bila pingamizi lolote. Mapinduzi yalifanikiwa kwa sababu wanawake waliokuwa mashujaa walizirai kutokana na hali yao ya uja uzito. Wanaume walishangilia ufanishi wao, wakachukua utawala na kuwa viongozi wa jamaa zao badala ya wanawake. Bila kusita, wanaume walipiga marufuku mfumo wa wanawake kuwa na waume wengi, na kuanzisha mfumo wa wanaume kuwa na wake wengi.

Wanaume aidha waliamua kubadilisha jina asilia la kabila hilo na pia majina ya mbari zao na kuyaweka chini ya mfumo wa utawala wa wanaume. Hivyo walifaulu katika kubadilisha jina la kabila lao kutoka kwa "Ruriri rwa Mbari ya Mumbi" na kuwa "Ruriri rwa Gikuyu" yaani "Watoto wa Gikuyu". Hilo lilimaanisha kuwa utawala na urithi katika jamii hiyo ungekuwa kwa upande wa wanaume

Walipotaka kubadilisha majina ya mbari, wanawake waliwapinga sana na kuwaambia wanaume kuwa iwapo majina ya mbari yangebadilishwa, wanawake wangekataa kabisa kuzaa watoto zaidi. Aidha, wanawake hao walitisha kuwauwa watoto wote wa kiume waliozaliwa kutokana na njama ya mapinduzi.

Wanaume waliogopa sana uamuzi huo wa wanawake na, ili kuepuka maafa, walikubali majina asilia ya mbari yaendelee kutumika.

Kutokana na kisaasili hiki tunapata kuona mambo kadha yanayojitokeza ili kuweza kudumisha jamii vilivyo. Uamuzi uliofikiwa kuwa mbari zote tisa ziwe chini ya utawala mmoja ni muhimu sana kwani uamuzi huo uliunganisha kabila la Wakikuyu.

Kisaasili hicho aidha chatuangazia kuhusiana na hali asilia ya utawala katika jamii ya Wakikuyu. Hapo twapata kujua kuwa wanawake ndio waliokuwa watawala. Kutokana na utawala wao wa kiimla, walipangiwa njama, wakatungwa mimba na wanaume, na kupinduliwa. Jambo hilo linatuonyesha hasa sababu ya wanawake wengi wa kabila la Wakikuyu kuwa wanyenyekevu kwa waume zao. Kutokana na mapinduzi yaliyotokea, wao walipata kujua kuwa wanaume wana nguvu na uwezo zaidi kuwashinda. Kisaasili hiki kunaitawala jamii ya Wakikuyu, kwani wanawake Wakikuyu walipata kujua nafasi yao katika jamii. Ndiposa twaona kuwa ni hivi karibuni tu wanawake walipoanza kushika hatamu za uongozi katika jamii.

Hata hivyo bado kuna sehemu fulani za Wakikuyu ambamo wanawake hawawezi kushika hatamu za uongozi. Wanawake Wakikuyu, baada ya mapinduzi, walipunguza ukali waliokuwa nao hapo awali na kuwa wanyenyekevu kwa wanaume.

Utawala wa jamii aidha wajitokeza wazi kuhusiana na mfumo wa ndoa. Mwanzoni kabla ya mapinduzi, wanawake walikuwa huru sana na hata waliweza kuwa na wanaume zaidi ya mmoja. Jambo hilo bila shaka lilipingwa na wanaume ambao, kwa wakati huo, hawakuwa na uwezo mwingi. Baada ya mapinduzi kutekelezwa, wanaume bila ya kusita waliupiga marufuku mfumo wa utawala uliokuwepo na kuanzisha mwingine ambapo wao, (wanaume), walikuwa na uhuru wa kuwaoa wanawake zaidi ya mmoja. Tangu wakati huo ni

nadra sana kupata mwanamke aliyeolewa na wanaume zaidi ya mmoja. Jambo hilo ni tofauti kabisa na hali ya wanaume ambao huwa na uhuru wa kuwaoa wanawake idadi yoyote. Mfumo wa mwanamume kuoa wake wengi uliitawala jamii kwani ulizuia matendo maovu; kwa mfano ukahaba, kwani mwanamke aliyekuwa hajaolewa alikuwa na matumaini ya kupata mume kwa kuolewa kama mke wa pili, tatu au wa idadi yoyote ile.

Kisaasili hiki aidha chaendeleza hoja ya umoja na muungano wa kabila la Wakikuyu. Jambo hilo ni dhahiri kutokana na mapinduzi yaliyotokea. Hata baada ya mapinduzi hayo, wanaume walioshikilia hatamu ya uongozi walipendekeza jina la kabila libadilishwe na kuwa `Ruriri rwa Mbari ya Gikuyu'. Badiliko hilo la jina halikuonyesha hali yoyote ya kutengana baina ya wanajamii hiyo. Kwa kubadilisha jina, wanaume walinuia kuonyesha kuwa wanaume ndio waliokuwa watawala na wala sio wanawake.

Hali ya wanaume kukubali utumizi wa majina asilia ya mbari ni dhihirisho kuwa wanawake katika kabila la Wakikuyu wamepewa heshima yao wanayostahili. Kulingana na kisaaasili, wanawake walipotisha kujifunga uzazi kabisa iwapo majina ya mbari yangebadilishwa, wanaume walibadili nia yao. Wanaume walipata kuelewa vilivyo kuwa bila wanawake kutekeleza wajibu wao wa uzazi vilivyo, basi kabila la Wakikuyu lingeweza kuzikwa katika kaburi la sahau. Hali hiyo inatoa utawala mwafaka katika jamii hiyo kwani akina mama, na hasa wakiwa wajawazito, walipewa na bado hupewa heshima na hutunzwa kwa makini sana. Hii ni kwa sababu wanaume huona kuwa, kwa kweli, kama lilivyo jina la mama wa kabila la Wakikuyu, Mumbi, kila mwanamke ni "Mumbi" kwani wao hutekeleza wajibu muhimu wa kuwaumba watu wanaoliendeleza kabila la Wakikuyu. Heshima waliyopewa wanawake (na wanaume) kulingana na kisaasili imedumishwa hadi leo. Wanawake katika hali hiyo huonekana kama walio muhimu katika kutoa mawazo muhimu katika jamii.

Kisaasili chetu aidha chatoa utawala katika jamii, hasa kwa upande wa wanawake. Katika kisaasili hicho,ukosefu wa uangalifu kwa upande wa akina mama ndio uliowafanya wahadaiwe na baadaye watungwe mimba na wanaume. Iwapo wanawake hao hawangetungwa mimba, bila shaka wanaume hawangeweza kutekeleza mipango yao ya mapinduzi. Hali hii yaonyesha udhaifu waliokuwa nao wanawake ; udhaifu ambao baadaye

uliwatia taabani. Kisaasili hiki, hivyo, kilikuwa na bado kina funzo muhimu kuhusiana na uangalifu na kumakinika katika kutenda jambo katika jamii yoyote ile. Mambo yatendwayo kiholela na kwa pupa bila uangalifu mara nyingi huleta matatizo katika jamii hiyo. Uangalifu huzaa matunda mazuri katika jamii na hivyo kisaasili chetu kinaitawala jamii katika kuonyesha umuhimu wa kuwa na uangalifu.

Kisaasili kingine muhimu katika kuonyesha jinsi visaasili vinavyoitawala jamii ni kile kinachohusiana na umilikaji na ugawanyaji ardhi miongoni mwa Wakikuyu.

Kulingana na kisaasili hicho, kama tulivyokwisha kuona hapo awali, Mugai alipoumba Ulimwengu, alianza shughuli za kuvigawa vipande vya ardhi na kuwapa watu wa makabila mbalimbali. Mugai alimpa Gikuyu ardhi nzuri yenye rutuba na kumwamuru ajenge mji katika mahali palipoitwa Mukurwe wa Gathanga. Gikuyu na Mkewe Mumbi walijenga mji wao na kuweza kupata watoto, wajukuu, vitukuu na muda si muda watu waliongezeka na kuwa wengi sana. Jambo hilo lilifanya ardhi ya jamaa hiyo kuwa na watu wengi na hivyo wengine waliamua kuhama na kuelekea upande wa kusini na kujaribu kupata ardhi kutoka kwa watu walioishi misituni.

Katika misitu, mliishi kundi la watu waliojulikana kama Gumba (Wapijini), na ambao walikuwa wawindaji. Wao walikuwa wafupi na wenye nguvu nyingi sana. Nyumba zao zilijengwa chini ya ardhi kwa vile watu hao waliona haya na hivyo hawakupenda kuishi na watu wengine. Ili kukata kabisa uhusiano na watu wengine, Wapijini hao walichimba mitaro iliyounganisha sehemu mbalimbali za vijiji vyao vilivyokuwa chini ya ardhi. Mara tu walipoona wageni, Wapijini wangekimbia na kuingia kwenye mitaro hiyo waliyoifunika kijanja, kisha wangekimbia haraka chini ya ardhi na kutokeza tena katika sehemu nyingine. Wakikuyu walishangazwa sana na kitendo hicho, kwani walidhani kuwa watu hao walitumia uwezo wa kizingaombwe katika "kufungua" ardhi na kupotelea ndani.

Kulingana na kisaasili hicho, hamkuwa na habari wazi kuhusiana na jinsi ardhi ilivyokuwa imegawanywa kati ya Wapijini na Wakikuyu. Inasemekana kuwa Wapijini walipotelea chini ya ardhi na hakuna yeyote aliyejua lolote kuwahusu. Kutoweka kwao ardhini kulihusishwa na mazingaombwe waliyofanya walipokuwa chini ya ardhi. Yasemekana

kuwa siku moja, walishindwa kufanya mazingaombwe hayo na hivyo walitoweka kabisa chini ya ardhi na hawakupata kuonekana tena.

Kutokana na kisaasili hiki, kuna mambo kadha ambayo yanajitokeza wazi kulingana na utawala wa jamii. Kwanza, tunaweza kushikilia kuwa Wapijini walipotelea upande wa Magharibi kuelekea misitu ya Zaire ambamo watu kama hao hupatikana. Hata hivyo, tunapozingatia umbali uliopo kati ya misitu ya Zaire na nchi ya Gikuyu, na aidha, shida ambazo zingewakumba Wapijini katika safari yao, hatuna budi kutilia shaka safari hiyo.

Hivyo basi, njia moja tu iliyobaki ya kueleza kutoweka kwa Wapijini hao ni kuwa waliingiliana na kuoana na Wakikuyu wa hapo awali waliokuwa wameingia msituni. Wakikuyu waliooana na Wapijini pengine walipoteza uhusiano wao na kundi kubwa la Wakikuyu, na hivyo, wakaamua kuishi msituni sawa na Wapijini walivyofanya.

Kisaasali hiki kinaeleza hasa jinsi jamii ya Wakikuyu ilivyoweza kumudu ardhi yao. Yasemekana kuwa Mugai ndiye aliyewapa ardhi yao, jambo ambalo lathibitisha umoja na jitihada za kabila la Wakikuyu katika kupigania ardhi yao. Iwapo Mugai hangetoa ardhi hiyo kwa Wakikuyu, huenda labda kabila hilo lingekuwa legevu sana na lenye kuhamahama kwa kutafuta makao. Huenda pia kabila hilo halingekuwa na bidii kama inavyodhihirika leo katika ukulima, ufugaji, na shughuli nyingine walizo nazo kwa vile hawangekuwa na undugu kati yao, jambo ambalo lingekuwa limesababisha kushambuliwa, kupigwa, na pengine hata kutawanywa na makabila mengine.

Kisaasili hiki aidha kinaeleza asili ya Ndorobo au `aathi' kama wajulikanavyo miongoni mwa Wakikuyu. Yasemekana kuwa, muda mfupi baada ya kutoweka kwa Wapijini basi mlitokea kundi la Wandorobo. Wao walikuwa wengi mno kwa idadi, na wingi huo ungelinganishwa na ule wa kukua kwa uyoga msituni. Walikuwa warefu na yasemekana walikuwa mazao ya kundi la Wakikuyu na Wapijini (Wagumba). Aidha Wandorobo hawakuishi chini ya ardhi bali walijenga nyumba zao ardhini, na nyumba hizo zilikaribiana sana na zile za Wakikuyu. Lugha yao pia ilifanana sana na ya Wakikuyu; hivi kwamba makabila hayo mawili yaliweza kuwasiliana bila matatizo yoyote. Wandorobo walihusiana vizuri sana na Wakikuyu na hata Wakikuyu waliweza kununua mashamba kutoka kwa

Wandorobo. Hii iliwezakana kwa sababu Wandorobo hawakuwa wakulima bali wawindaji. Mashamba yaliyonunuliwa kwa jinsi hiyo yalikuwa mali ya jamii. Mashamba kama hayo ndiyo yaliyoendeleza kabila la Wakikuyu, kwani kabila hilo lilitetea nchi yao kijumla na walipokuwa wanaongea na wageni, wao wangeweza kuita sehemu yao ya nchi "borori wito" au "borori wa Gikuyu" kumaanisha kuwa ardhi hiyo ilikuwa yao au ya Gikuyu. Ukweli hata hivyo ni kuwa kila sehemu ya ardhi ilikuwa na mipaka iliyojulikana, na kila mtu aliheshimu mpaka wa ardhi ya jirani yake. Kisaasili hiki ni kifaa muhimu katika kuitawala jamii kwani, ingawa ardhi yote ya Wakikuyu kwa jumla ilijulikana kama ardhi ya Gikuyu kila mtu alikuwa na konde lake, na hivyo waliheshimiana vilivyo. Kwa njia hiyo, amani ilidumishiwa na heshima ikazidi kukua mingoni mwa Wakikuyu jambo ambalo huonekana wazi hata leo kwani kila mtu huwa na hati yake ya kumiliki shamba, na hawezi kuingilia shamba la mwenziwe. Kuingilia shamba la mwingine ni hatia na huweza kuhukumiwa na sheria ya wazee wa kijiji au na sheria ya nchi.

Miongoni mwa Wakikuyu pia kuna kisaasili kuhusiana na uundaji wa Serikali. Kulingana na kisa hicho, zamani za kale kulikuwa na Mfalme katika nchi ya Wakikuyu aiyejulikana kama Gikuyu, mjukuu wa binti wa kwanza wa mwanzilishi wa kabila hilo. (Miongoni mwa Wakikuyu, watoto wa kwanza hupewa majina ya nyanya au babu zao, ndiposa mwana wa bintiye Gikuyu akaitwa Gikuyu vile vile). Gikuyu aliongoza kwa miaka mingi na alitawala kwa kutumia nguvu. Watu walikatazwa kulima mashamba kwani mfalme alisema kuwa mwanamume yeyote aliyekuwa na nguvu alitakiwa ajiunge na jeshi na awe tayari kuhama kuelekea alikotumwa na Mfalme. Kwa hivyo, watu waliishi maisha ya kuhamahama na, kutokana na ukosefu wa kulima, walikumbwa na baa la njaa. Uliwadia wakati ambapo watu walichoshwa na tabia ya kuhama na wakaamua kutulia. Watu hao walimwendea Mfalme na kumwambia awaruhusu kulima mashamba yao na kujenga makao ya kudumu.

Kutokana na utawala wa kiimla, Mfalme alikataa ombi la watu wake. Watu, kwa hivyo, walikasirishwa sana na hali hiyo ya Mfalme na hivyo basi wakapanga mapinduzi. Kizazi kilichoongoza mapinduzi hayo kilijulikana kama `iregi' (wapinduzi), na kizazi kilichofuata kilichoanza ukulima kikajulikana kama `ndemi' (wakataji), kama kumbu kumbu ya kipindi ambapo Wakikuyu walipoanza kukata misitu na kujitokeza kama wakulima.

Baada ya Mfalme Gikuyu kupinduliwa, Serikali ya nchi hiyo ilibadilishwa kutoka kwa Serikali ya kiimla na kuwa ya kidemokrasia iliyozingatia sana mahitaji ya wananchi. Mapinduzi hayo yanajulikana kama `itwika' kutoka kwa neno `twika', lenye maana ya kuvunjika kutoka kwa utawala wa mabavu na kupata demokrasia. Ufanisi huo ulisherehekewa nchini humo; karamu, ngoma, nyimbo ziliendelezwa kwa muda wa miezi sita mfululizo; iliyotangulia mwongo mpya wa Serikali iliyopendwa na watu. Ili kuendesha Serikali hiyo mpya kwa ufanisi, mlikuwa na katiba na baraza la "njama ya itwika" lililoteuliwa kuongoza katiba. Kila kijiji kiliteua mwakilishi katika baraza hilo na mkutano wa kwanza wa baraza hilo ulifanyika Mukurwe wa Gathanga. Hivyo, sheria, za kuitawala Serikali mpya zilikuwa:-

- Uhuru kamili kwa watu na kuendeleza ardhi chini ya mfumo wa umilikaji wa kijamaa.
- Umoja wa kabila la Wakikuyu na wanachama kamili, ambao ungetambuliwa kutokana na kutahiri wavulana katika miaka ya kumi na sita na kumi na nne; nao wasichana kati ya miaka kumi na kumi na minne.
- Kijamii na kisiasa, wanaume na wanawake wote waliotahiri wangekuwa wanachama sawa katika kabila hilo na hivyo tawala za kifalme zikamalizwa.
- Serikali ingekuwa mikononi mwa baraza la wazee (kiama) lililochaguliwa na wanajamii wote. Wanabaraza hilo wanapaswa kutoka kwa wazee waliostaafu kutoka kwa umri wa upiganaji vita.
- Wanaume wote kati ya miaka kumi na minane na arobaini wangeungana na kuwa kundi la wapiganaji (anake) na wangetakiwa kila mara wawe tayari kupigania nchi yao.
- Wakati wa mahitaji, Serikali ingewaomba watu watoe mbuzi, kondoo na ng'ombe kwa kutolewa kafara za kitaifa na pia katika sherehe nyingine zozote zilizohusu kabila lote.
- Ili kuhakikisha kuwa utawala wa mabavu haurejei tena, Serikali ingebadilishwa mara mwa mara baina ya vizazi viwili yaani cha `Mwangi' na cha `Maina' ambacho pia kilijulikana kama `Irungu'. Uanachama wa vizazi hivyo ungeamuliwa tangu uzazi na iwapo kizazi kimoja ni cha Mwangi watoto wao wangeitwa Maina, nao wajukuu wao wangeitwa Mwangi na

kadhalika. Iliamuliwa kuwa kila kizazi kingeshika hatamu ya uongozi kwa muda wa miaka thelathini hadi arobaini.

- Wanaume na wanawake ni lazima kuoa au kuolewa ili waweze kupata heshima na madaraka katika jamii.
- Sheria kuhusu tabia ya watu katika Serikali pia zilitolewa na wote walitakiwa kuwa watiifu kwa Serikali yao.

Kisaasili hiki, kama kinavyojitokeza, kina mafunzo mengi mno na pia ni muhimu sana katika utawala wa jamii ya Wakikuyu.

Katika kisaaasili hiki, twapata kuelewa heshima iliyotunukiwa wazee miongoni mwa jamii ya Wakikuyu. Wakikuyu waliona, na bado huona wazee kama watu walio na tajriba tofauti na ambao huwa na vyeo vikubwa katika jamii. Ndiposa twaona kuwa, baada ya mapinduzi yaliyotokea, wazee ndio waliochaguliwa katika "njama ya itwika" kuchukua wadhifa wa utawala. Vile vile, twaona kuwa wazee hao wamepewa vyeo vingi katika jamii kama vile kutoa hukumu au uamuzi katika kesi mbalimbali zilizotokea katika jamii.

Vile vile, kisaasili hiki kinaeleza mfumo wa Kisiasa miongoni mwa Wakikuyu hadi wakati Wakoloni walipoingia nchini Kenya na kuvunjilia mbali mifumo ya kisiasa miongoni mwa makabila mengi wakiwemo Wakikuyu. Mfumo huo wa Kisiasa waonyesha dhahiri kuwa, kabila la Wakikuyu halikuwa na nafasi hata kidogo kwa utawala wa nguvu; wao walipendelea haki zao, na hivyo walikuwa tayari kila mara kupigania haki zao. Jambo hilo linadhihirika wazi wakati ambapo watu wa kabila hilo walichoshwa na utawala wa kimabavu wa Mfalme Gikuyu na kupindua Serikali yake, huku wakipiga marufuku bila kusita utawala wa Kifalme katika jamii hiyo.

Kutokana na uchambuzi wa kisaasili hiki, twapata kujua asili ya mambo fulani kitamaduni yaliyokuwa yamepewa umuhimu, kisiasa na kijamii. Kwa mfano, umuhimu wa mambo ya kitamaduni kama vile utahiri umetiliwa maanani, kwani ndio uliokuwa alama ya uanachama halisi katika kabila hilo. Iwapo mtu yeyote hakutahiriwa, basi yeye alikuwa ni kama mgeni katika jamii hiyo na hangekubalika kabisa hadi atahiri. Utahiri aidha ulikuwa ni alama ya kuvuka kutoka utoto na kuingia katika kundi la utu uzima, wakati ambapo mtu

aliruhusiwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii, na aidha kumiliki mali. Ndoa, aidha, ilitiliwa maanani na, kulingana na katiba, ilikuwa ni hatia kwa mwanaume au mwanamke yeyote yule kukosa kuoa au kuolewa. Mtu kama huyo hakupewa heshima aliyostahili, na aidha hangeweza kupata madaraka katika jamii. Mambo ya kidini kama sala na utoaji kafara pia ulitiliwa maanani. Jambo hilo lilikuwa muhimu sana, ndiposa katika katiba kukawa na sheria ya watu kutoa mifugo waliohitajika katika kuendeleza matukio kama hayo ya kidini. Umuhimu wa dini katika jamii ya Wakikuyu ni dhihirisho kuwa Wakikuyu walikuwa wacha Mungu na hata waliamini kuwa kabila lao pia na ardhi yao ilitoka kwa Mungu.

Kisaasili hiki, bila shaka, ni kifaa muhimu cha kutawala jamii ya Wakikuyu kuhusiana na mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika jamii hiyo kama vile utawala, uhusiano wa watu katika jamii, uhusiano wa watu na Mungu na aidha umuhimu wa kuzingatia utamaduni vilivyo.

Kutokana na visaasili tulivyoeleza kama vifaa vya kutawala jamii , ni wazi kuwa visaasili hivyo ni muhimu kwa kutawala jamii. Visaasili hapo twaona vina umuhimu katika jamii kama zilivyo tanzu nyingine za Fasihi Simulizi. Mfano, methali na misemo hutambuliwa kama tanzu zifaazo sana katika kutawala vitendo vya watu katika jamii. Visaasili navyo, havikuachwa nyuma kwani vyaonyesha asili ya vitendo muhimu katika jamii na jinsi vitendo hivyo vinavyopaswa kuzingatiwa na kudumishwa ili kukuza jamii katika mkondo unaofaa. Katika kufanya hivyo, visaasili huwa vinatawala jamii vilivyo.

## 3.5. VISAASILI: KUTOA MAADILI KATIKA JAMII

Visaasili vilitekeleza, na bado hutekeleza wajibu muhimu wa kutoa maadili yanayofaa katika jamii ya Wakikuyu. Kupitia kwa visaasili na tanzu nyingine za Fasihi Simulizi, wanajamii hupata mawazo yatakayowaongoza katika maisha. Wazee nao hukumbushwa mara kwa mara, kuhusiana na sheria na mambo ambayo lazima yawekwe hai kwa manufaa ya wanaokuja baadaye.(Okpewho 1992:115).

Visaasili, kama tulivyotangulia kusema hueleza asili ya maumbile. Hutoa maelezo kuhusu tabia ya sasa inayoonekana ya mtu, mnyama au ndege fulani. Visaasili vya namna hii

mara nyingi huwa na maadili fulani. Tabia ya wanyama au watu hao hutolewa kama funzo la kuwaonya au kuwatahadharisha watu dhidi ya kutenda maovu fulani.

Miongoni mwa Wakikuyu, visaasili vya namna hii ni vingi mno na hutoa mafunzo mengi sana. Kwa mfano, kuna kisaasili cha Kuku na Mwewe. Kisa hiki kinaeleza kuwa zamani sana Kuku alienda kumuazima Mwewe sindano, lakini kwa bahati mbaya, aliyeazima akaipoteza sindano ile. Kwa sababu ya kitendo chake, ili kufidia gharama ya sindano, Mwewe kila mara anawavamia vifaranga wa Kuku. Hata kufika leo Kuku angali anachakurachakura huku akitafuta sindano ya Mwewe. Hali hii ya mambo yaeleza ni kwa nini kila mara kuku huwa anachakurachakura na pia ni kwa nini Mwewe anawavamia vifaranga wa Kuku.

Ingawa kisaasili hiki ni kifupi, kinatutolea mafunzo muhimu sana. Maadili yatolewayo wazi na kisaasili hiki ni kuwa, ni muhimu kila mara tuwe waangalifu kwa chochote tunachofanya na hasa tunapoazima vyombo kutoka kwa wenzetu. Bila shaka, kama Kuku angalikuwa mwangalifu baada ya kuazima sindano kutoka kwa Mwewe, hangepatwa na shida aliyopata. Hadi leo yeye huchakura tu bila ya kujua iwapo ataipata sindano aliyoipoteza, lakini bila shaka ana matumaini ya kuipata siku moja. Aidha, Kuku hangepatwa na majonzi kila mara kwa kuwapoteza vifaranga wake walioliwa na Mwewe. Tabia ya Kuku kutokuwa mwangalifu inawaathiri hata wanawe, kwani vifaranga sio walioipoteza sindano lakini ndio wanaolipa kosa la mama yao. Tunafunzwa, kwa hivyo, kuwa tuwe waangalifu tusije tukawaumiza wengine tunaohusiana nao katika kulipa dhambi zetu.

Maadili mengine yajitokezayo wazi katika kisaasili hiki ni yale ya kulipiza kisasi. Mwewe anapenda sana kulipiza kisasi na ndiposa aliamua kuwavamia vifaranga wa Kuku kila alipopata fursa. Kulipiza kisasi kama tujuavyo si jambo zuri. Kulingana na kisaasili, jambo analofikiria mwewe kila mara ni kuwavamia vifaranga wa Kuku. Yeye humla tu kifaranga ampataye na kuanza tena kusaka mwingine. Kisaasili hiki kinatuonya dhidi ya kupenda kulipiza kisasi na badala yake tujitahidi zaidi katika kufidia tuliyokosewa. Kwa njia hiyo, tutawasaidia waliotukosea (kwani mara nyingi makosa huwa sio makusudi), na pia tuweze kujifaidi kwa kufanya mambo mengi yaliyo ya maana kuliko tu kukimbilia visasi.

Aidha, kuna kisaasili kinachotoa maadili ya ubaya wa kuwaonea wenzetu wivu. Mara nyingi tunapowaonea wenzetu wivu, huwa tunapatwa na matatizo fulani ambayo hutuathiri sana maishani. Wivu ni mbaya kwani hata kuanzia mwanzo wa Ulimwengu kuna visa vya maovu ya wivu mfano jinsi Kaini alivyomwonea wivu nduguye Abeli na hivyo yeye (Kaini) akalaaniwa na Mwenyezi Mungu.

Miongoni mwa Wakikuyu, mna kisa cha Sungura na Buibui kinachoonyesha hali ya wivu. Hapo zamani, Sungura na Buibui walikuwa marafiki wakubwa. Buibui alipeleka posa kwa msichana mrembo aliyetaka kumwoa. Msichana huyo alimpenda Buibui sana na, ingawa hakuwa amemwarifu, alingoja kwa hamu kubwa kuolewa naye.

Siku moja, Buibui alimwambia Sungura, "Njoo rafiki yangu. Nigetaka kukuonyesha mchumba wangu". Sungura alikubali mwaliko wa kwenda kumwona rafiki yake Buibui. Msichana yule mrembo alikuwa anajitayarisha kwenda mtoni wakati Sungura na Buibui walipowasili. Kisha Sungura alimwambia Buibui.

"Mbona usiende mtoni ukateke maji? Msichana huyu atakupenda zaidi ukifanya hivyo". Buibui alikubali na akachukua mtungi na kuelekea mtoni kuteka maji. Mara tu alipoondoka Buibui, Sungura alianza kuzungumza na yule msichana na kumwambia.

"Je, umekubali kuolewa na Buibui? Unawezaje kuolewa na mtu mwenye miguu minane?. Utakuwa unachoka sana kwa sababu itakubidi kuteka mitungi minane ya maji kila siku, kwa vile Buibui hutumia mtungi moja wa maji kuoshea mguu moja".

Msichana aliposikia hayo, aliogopa kazi ya kuteka mitungi minane ya maji kila siku, na hivyo akaamua kutupilia mbali posa ya Buibui. Buibui aliporejea na mtungi wa maji, alifadhaika kusikia kuwa msichana alikuwa amebadili nia. Alienda nyumbani akiwa na huzuni kubwa. Hata hivyo Buibui hakufa moyo na mara alimtafuta msichana mwingine. Lakini alipompeleka huko rafiki yake kumwona msichana yule, Sungura alimhadaa tena na kumfanya msichana akatae posa ya Buibui. Sungura alifanya hivyo kwa muda mrefu na alimuudhi sana rafiki yake Buibui. Uliwadia wakati ambapo Buibui aliona kuwa hataweza kumpata mchumba duniani, na hivyo akaamua kwenda mbinguni kutafuta mchumba. Siku iliyofuata, Buibui alianza safari kwenda mbinguni kutafuta mchumba, huku akitumia utandabui wake. Mara alimuona msichana mrembo kupindukia na kwenda kuzungumza naye. Msichana yule alikubali kuolewa na Buibui, na wakakubaliana kuwa Buibui angeenda

kumchukua baadaye. Buibui aliridhika na kurudi tena duniani na alipofika, aliukunja utandabui wake uliokuwa mrefu sana.

Baada ya muda usiokuwa mrefu, Buibui hakuweza kuvumilia furaha aliyokuwa nayo na kama kawaida, alimwendea rafiki yake Sungura na habari zake nzuri. Sungura aliposikia habari ile, alipatwa na wivu mkubwa na akaanza kupanga hila za kuivunja posa ya Buibui. Sungura hakufurahia wazo la wasichana kumkubali Buibui kila mara.

Siku ya Buibui kwenda kumchukua mkewe iliwadia, na baada ya kufika mbinguni alisahau kuukunja utandabui wake. Sungura alipoona hivyo aliushika utandabui na kuanza kupanda kuelekea mbinguni.

Sungura alihakikisha kuwa alimuona mchumba wa Buibui na kumuonya dhidi ya kuolewa na Buibui, kwani ingembidi kuchota maji mitungi minane kila siku. Mara moja msichana alikataa kuolewa na Buibui na alipomwambia Buibui, Buibui alighadhabika sana. Buibui aliuchukua utandabui wake na kuteremka duniani mara moja na kumwoa msichana mwingine. Alipokuwa anateremka aliukunja utandabui wake ili Sungura ashindwe kurudi chini. Sungura alilia sana kwani hakuwa na matumaini yoyote ya kufika duniani. Mtu mmoja mzee alimuona Sungura akilia na akamwuliza shida yake. Sungura hakusita kumweleza kuwa Buibui aliuchukua utandabui na hivyo hakujua jinsi ya kufika duniani.

Yule mzee aliwaita watu wa kijiji chake na kuwaambia wafume nyuzi mbili ndefu sana. Nyuzi zile zilipokuwa tayari, mzee aliwaambia watu wale wafunge kila moja kwenye masikio ya Sungura. Kisha pole pole, walimteremsha Sungura kuelekea duniani. Sungura aliambiwa kuwa afikapo duniani, atikise nyuzi zile kwa nguvu ili watu wa mbinguni wajue amewasili.

Kila alipoteremshwa, masikio yake yalivutika sana na alihisi maumivu. Alipokuwa karibu kuwasili, Sungura alisahau na kutikisa nyuzi. Watu mbinguni waliachilia nyuzi wakidhani kuwa Sungura alikuwa tayari amefika duniani. Sungura alianguka kwa nguvu puh!puh!, akavunjika mgongo uliopona baada ya miezi miwili lakini masikio yake tangu wakati huo yalibaki marefu sana.

Kulingana na kisaasili hiki twaona kuwa kina maadili kadha. Kisa chenyewe kinatuonya dhidi ya kutoa siri zetu kila mara kwa marafiki zetu. Ni dhahiri kuwa ingawa Sungura alijifanya rafiki wa Buibui, yeye hakumtakia mema, ndiposa kila mara akawa mbioni, kuvunja posa zote za Buibui. Kisa hiki kinatuonyesha kuwa, ni heri tuhifadhi siri zetu na tusiwaambie watu makusudio yetu hadi wakati ambapo mipango imetimia. Iwapo Buibui angepanga ndoa bila ya kumjulisha Sungura, yeye bila shaka angeweza kupata mke kwa urahisi, bila ya kusumbuka alivyosumbuka.

Maadili mengine yatolewayo na kisa hiki ni kuwa tusiwe wepesi wa kusikiza mawaidha ya watu bila ya kuchunguza mambo kwa undani. Twaona kuwa wasichana wote walioposwa na Buibui, ingawa walidai kuwa walimpenda, walikuwa wepesi sana katika kushawishiwa na Sungura. Ingekuwa jambo la busara kwa wasichana hao kuchunguza na kuona iwapo kwa kweli, wangehitajika kuteka mitungi minane ya maji kama alivyodai Sungura. Vile vile, yatupasa kuwa wastahimilivu kabla ya kutenda jambo kwani kukimbilia mambo kwa pupa huenda kukaleta hasara. Pengine wasichana waliovunja posa za Buibui hawakuweza kupata waume baadaye.

Kisaasili hiki vile vile kinatutahadharisha dhidi ya kuwaonea wivu wenzetu. Jambo hili ladhihirika wazi kutokana na yaliyompata Sungura baada ya kumuonea wivu rafiki yake kwa muda mrefu sana. Iwapo Sungura hangekuwa na wivu aliokuwa nao, pengine yeye angesaidiwa na buibui kumpata mchumba, kwani Buibui alikuwa na bahati sana ya kupendwa na wasichana. Twaona kuwa Sungura hakuyafikiria maisha yake kwani, kama angefanya hivyo, angekuwa anajishughulisha na kutafuta mchumba, jinsi rafikiye Buibui alivyofanya.

Kutokana na wivu na uchochezi wake, twaona kuwa wakati unawadia ambapo Buibui anakasirika sana na kuamua kumtesa Sungura kwa kuukunja utandabui wake kutoka mbinguni. Sungura anasumbuka sana na hata baada ya kupata wasaidizi kutoka mbinguni, wasiwasi wake unamdhuru. Hii yaonekana dhahiri anapotikisa nyuzi na kusababisha ziachiliwe huku akiwa bado hajafika duniani. Wasiwasi wake unamfanya avunjike mgongo, lakini jambo baya kabisa linalompata ni kurefuka kwa masikio yake yaliyokuwa yamefungwa kwa nyuzi. Masikio hayo yalibakia marefu na hata leo, Sungura huwa na masikio marefu. Funzo kwa Sungura na kwetu pia ni kuwa, wivu haulipi chochote na pia, mara nyingi wivu

hulipwa na maovu. Sungura aliyemuonea wivu Buibui hakupata chochote ila madhara, ilhali Buibui alibahatika kumpata mke na maisha mazuri ya baadaye. Kisaasili hiki kina makanyo, maonyo dhidi ya bezo na wivu kwa wenzetu.

Maadili mengine yanayotolewa na visaasili ni ubaya wa kuwa na tamaa ya vitu vya wengine. Miongoni mwa jamii ya Wakikuyu, tuna Kisaasili kinachoonya dhidi ya kuwa na tamaa katika jamii. Kulingana na kisaasili hicho, zamani za kale Nyoka na Tandu walikuwa marafiki wakubwa sana. Wao walitembeleana ili kujuliana hali na uhusiano wao ulikuwa mzuri sana. Siku moja, Nyoka alialikwa katika karamu na harusi ya Swara. Kila mara, mnyama aliyealikwa harusini alijipamba sana kwani aliamini kuwa iwapo anapendeza, huenda naye pia akapata bahati ya kupata mchumba humo. Basi Nyoka alikuwa na wasiwasi mkubwa sana kwa vile yeye alikuwa hana macho. Aliweza kufika kokote alikotaka kwa kutumia msaada wa miguu yake kwani alikuwa na miguu mingi sana. Kwa vile alikuwa hajawahi kuwa na macho, alikuwa hajui uzuri wa kuwa nayo. Baada ya kupata mwaliko wake, Nyoka alimwendea rafiki yake Tandu na kumwamsha. Tandu aliposikia kuwa ni rafiki yake Nyoka aliyekuwa anamwita, aliufungua mlango na kumkaribisha ndani. Nyoka alimwelezea mwaliko aliokuwa nao na kusema shida yake iliyokuwa imempeleka kwa Tandu. Tandu hakuwa amepata mwaliko lakini hakuona vibaya. Bila ya kusita, Nyoka alimweleza rafiki yake kuwa alimtaka amwazime macho yake, na akaahidi kuyarejesha baada ya karamu. Tandu, kwa vile alimuamini rafiki yake, alikubali kumpatia macho ili aweze kuendelea na shughuli za usiku ule. Kwa kweli Tandu hakuwa na miguu na aliweza kutambaa kwa kutumia tumbo lake. Nyoka hakusita na mara moja aliitoa miguu yake mingi na kumpa Tandu ambaye naye aliyatoa macho yake na kumpa Nyoka. Nyoka hakuamini uzuri alioona. Ama kweli alikuwa amekosa mambo mazuri sana kwa kukosa macho. Nyoka alimuaga rafiki yake na kuondoka kuenda karamuni. Hata hivyo hakuwa na miguu na hivyo basi ilimbidi atambae jinsi Tandu alivyokuwa akitambaa hapo awali. Nyoka alipofika karamuni alifurahia sana mambo yote aliyoyaona, na baada ya karamu, akaamua kuuvunja urafiki baina yake na Tandu. Jambo hilo lilimaanisha kuwa Nyoka angebaki na macho ya Tandu naye Tandu akae na miguu ya Nyoka. Nyoka aliona kuwa ni heri aweze kuona hata kama hataweza kutembea; hiyo ndiyo sababu ya Nyoka kukosa miguu. Tandu naye alinyimwa macho yake na kwa sababu hii, yeye huwa hana macho lakini ana miguu karibu mia moja aliyopata kutoka kwa Nyoka.

Kutokana na kisaasili hiki, twaona jinsi tamaa ilivyomfanya Nyoka akatae kutimiza ahadi yake bila ya kuijali hali ya rafiki yake. Tamaa ya Nyoka ilimfanya amnyang'anye Tandu macho baada ya kukosa kutimiza ahadi. Nyoka hakujali tena urafiki baina yake na Tandu na hivyo aliamua kuuvuja urafiki huo. Tamaa, hata hivyo, ni mbaya kwani ilimfanya Nyoka akose miguu. Hiyo ndiyo sababu iliyomfanya Nyoka awe anatambaa kila mara kwani alitamani macho ya mwenziwe naye akamuachia miguu yake. Tamaa wakati wote huwa na madhara yake. Kisaasili hiki kinaonyesha hasara itokanayo na tamaa; hasara ambayo aliipata Nyoka ambayo humfanya auawe kwa urahisi na maadui zake kwa vile hana miguu ya kukimbilia. Kisaasili hiki, kwa hivyo, kinatuadilisha kuwa ni bora mtu aridhike na chake alichonacho kwani anayetamani cha mwenziwe hupatwa na hasara fulani. Tamaa ya Nyoka ilimfanya ampoteze rafiki wa dhati. Bila shaka Tandu alimpenda sana nyoka na pia alimwamini kiasi cha kuweza kutoa macho yake na kumwazima. Nyoka, kutokana na tamaa yake, hakuuthamini urafiki huo na jambo hili lilimfanya asipate rafiki mwingine wa dhati kama alivyokuwa Tandu. Nyoka hivi sasa ana maadui wengi sana kwani aliyekuwa rafiki yake wa pekee pia alimwacha na kuwa adui yake.

Kutokana na kisaasili hiki, urafiki ni jambo muhimu sana na yafaa kila mara watu wawe tayari kudumisha urafiki huo. Marafiki huweza kusaidiana na kufaana wakati wa shida na hivyo basi ni bora udumishwe.

Kisaasili cha Nyoka na Tandu kinatuonya kuwa, tusiwe wajanja na wenye kutamani ya wengine kwani tamaa hiyo ikizidi huenda ikatuletea madhara fulani.

Kwa upande wa Tandu, kisaasili hiki kinatuonya dhidi ya kuwaamini marafiki zetu sana. Kama Tandu hangemwamini sana Nyoka, huenda hangemuazima macho yake na bado angalikuwa anaona. Tandu, kutokana na mapenzi yake kwa rafiki yake, aliyatoa macho yake na kumpatia; jambo lililomdhuru baadaye. Ingawa alichukua miguu, Tandu bado hajaridhika kutokana na ukosefu wa macho. Kwa hivyo hili ni funzo kwetu kuwa iwapo tuna marafiki, ni bora kwanza tuchunguze na kuweza kung'amua marafiki tunaoweza kuwaamini bila wasiwasi, kwani wengine huweza kutuletea madhara maishani mwetu. Imani ikikiuka mpaka basi bila shaka hasara huingia na pengine urafiki huwa si wa kweli bali ni ule wa Paka na Panya.

Kutokana na visaasili hivi tulivyoeleza, ni dhahiri kuwa kuwa visaasili hivyo huwa na dhima muhimu katika kutoa maadili yanayofaa katika jamii. Visaasili hutuangazia yaliyo mema na yaliyo maovu katika jamii na kutuonya dhidi ya kujiingiza katika mambo yasiyofaa maishani mwetu.

### 3.6. VISAASILI: KUONYESHA UFUNDI MIONGONI MWA WAKIKUYU

Jamii ya Wakikuyu huwa na vitendo mbalimbali ambavyo vimewapa sifa nyingi sana. Wao hupenda kuvumbua vitu mbalimbali kama makabila mengine yalivyo barani Afrika na kwingineko.

Kuna visaasili katika jamii hiyo vinavyoeleza hasa ujuzi wao ulikotoka au ulivyoweza kuvumbuliwa. Visaasili vya aina hii bila shaka vitakuwa mwafaka katika kueleza matukio mbalimbali yaliyopo katika jamii ya Wakikuyu.

Miongoni mwa visaasili hivyo, ni kile kinachohusu uhunzi ambao uliwatia bidii sana Wakikuyu katika utendaji kazi wao kwani waliweza kufua vyuma vya kutumia. Kwa karne nyingi, Wakikuyu wamekuza ujuzi wa ufuaji vyuma kutoka kwa mchanga, na hivyo basi, matumizi ya zana za vyuma yameimarika katika jamii ya Wakikuyu tangu enzi za mababu.

Kulingana na kisaasili kinachohusu asili ya uhunzi, twaarifiwa kuwa wanyama waligawanywa katika sehemu mbili kwa matumizi ya nyumbani. Mugai alitoa sehemu moja na kuwapa wanaume, na sehemu ya pili akawapa wanawake. Wakati huo, watu hawakuwa na zana zozote za vyuma na walitumia visu na mikuki iliyochongwa kutoka kwa mbao. Wanawake walianza shughuli za kuwachinja baadhi ya wanyama waliopewa ili wapate chakula. Kwa kuchinja, wanawake hao walitumia visu hivyo vya mbao na hivyo basi walichukua muda mrefu sana kuwaua na kuwatoa ngozi wanyama. Kisaasili hiki kinaeleza kuwa, kutokana na uchungu mwingi waliohisi wanyama hao walipokuwa wanachinjwa, wanyama walishindwa kuvumilia zaidi. Usiku mmoja, wanawake walipokuwa wanalala, wanyama wote walikutana na wakaamua kutoroka kutoka kwa binadamu hao wasiokuwa na huruma. Wanyama wote waliokuwa mali ya wanawake walitoroka na wakatapakaa misituni na nyandani. Wakati huo huo, wanyama hao walichagua viongozi miongoni mwao,

ambao wangewalinda wasikamatwe tena na wanadamu. Simba na Chui walichaguliwa kuwa walinzi wa misitu, Ndovu, Nyati na Kifaru walinzi wa vichaka; Kiboko akawa mlinzi wa mito na maziwa na kadhalika. Kuanzia wakati huo, wanyama wote waliokuwa wakimilikiwa na wanawake wakawa wanyama wa mwituni, ilihali wanyama waliomilikiwa na wanaume waliendelea kufugwa nyumbani.

Wanawake walijaribu sana kuwapata wanyama wao kutoka misituni lakini hawakufanikiwa. Hivyo, wanawake walimuomba na kumsihi Mugai awasaidie kuwapata wanyama hao. Mugai hakuwasikiza kwani alisema kuwa wanawake walikuwa wamewatesa sana wanyama hao na hivyo basi yeye Mugai ndiye aliyewawezesha wanyama hao kutoroka. Wanaume walipoona yale yaliowapata wanawake, waliutuma ujumbe kwa Mugai wakimuomba awaeleze njia mwafaka ya kuwatunza wanyama wao. Wajumbe walimwendea Mugai wakiwa na kondoo mweupe na kusema kuwa walitaka kumtolea Mugai kafara ila waliogopa kutumia silaha butu kumuua na kumtoa ngozi mnyama huyo.

Kwa ombi lao, Mugai aliwaambia, "Nyinyi ni watu wenye busara kwa kuwa mmekumbuka kuomba msaada wangu. Naona kuwa mwafahamu niliwapa wanyama hawa na pia nina uwezo wa kuwachukua kutoka kwenu. Kutokana na imani yenu kwangu, nitawapa mawaidha kuhusiana na jinsi ya kupata zana bora, sio tu za kutolea kafara, bali pia za matumizi yenu yote kwa jumla. Nitawafanya watawala wa wanyama wenu kwa zana mpya, lakini nitawaamuru mzitumie pamoja na wanawake walionikosea." Kufikia hapo, Mugai aliwaongoza wanaume hao hadi kando ya mto na kuwambia: " Chukueni mchanga kutoka mahala hapa. Ukausheni kwenye jua, kisha tengenezeni moto na kuutia mchanga huo ndani, na kupitia kwa njia hiyo mtapata chuma. Nitawapatia busara ya kutengeza silaha na zana nzuri zaidi na kwa hivyo hamtatumia silaha butu tena."Tangu wakati huo, Wakikuyu, kwa kufuata maagizo ya Mugai, waliingia katika kipindi cha kutengeza na kufua vyombo vya chuma.

Kisaasili hiki chaonyesha kuwa kutokana na usaidizi wa Mungu (Mugai), wanaume Wakikuyu waliweza kutunukiwa ujuzi wa kufua vyuma. Ujuzi wao wa uhunzi bila shaka unadhihirishwa na zana za chuma na mapambo yao asili ya kabila lao yapatikanayo katika

matendo yote muhimu ya jamii ya Wakikuyu. Zana muhimu za chuma zipatikanazo katika jamii hiyo ni kama vile mikuki, pete, bangili,mashoka, mikasi na vingine vingi.

Yaonekana kuwa Wakikuyu hujivunia ufundi huo kwani haukutokana na ujuzi wa mwanadamu bali wa Mungu wao wamwitaye Mugai. Kutoka kwa Mungu vile vile, Wakikuyu waliweza kupata sheria muhimu zinazoweza kuwasaidia katika mambo mbalimbali ya siku baada ya siku. Kwa mfano, wanaume waliomwendea Mugai wakiomba usaidizi wa kutoa kafara walipata fursa ya kupewa mawaidha kuhusiana na jinsi ya kutengeneza silaha kali ambazo wangetumia katika kuwachinjia wanyama wao.

Vile vile, kuna kisaasili kinachohusiana na ufundi uliopo miongoni mwa kabila la Wakikuyu. Yasemekana kuwa, zamani za kale, watu walikula majani na matunda waliyokusanya mwituni yakiwa mabichi. Watu hao hawakupika vyakula vyao kwani hawakuwa na moto. Siku Moja Mugai alimtokea mtu mmoja na kuomba apewe chakula. Yule Mtu aliyakusanya matunda na majani na kuyaandaa ili Mugai akija apate kuyapokea. Mugai alipotoka safarini mwake, alikuja kwa mtu yule ili apate chakula alichokuwa ameagiza. Mugai alipoona kuwa chakula kilikuwa kibichi, alimwita yule mtu na kumwambia achukue kipande cha mti wa aina ya "Muringa" na kukipasua katikati. Baadaye aliambiwa na Mugai achukue kipande kingine kidogo zaidi cha mti na akisugue kwa nguvu kwenye kipande cha "Muringa". Kutokana na Nguvu nyingi aliyotumia katika kusugua vipande vile vya miti, kijishimo kidogo kilitokea na baadaye moshi ukaaza kuonekana humo kijishimoni. Hapo basi mtu huyo alichukua majani makavu kabisa, na kuyaweka chini ya vijiti hivyo huku akiendelea na usuguaji wake. Moshi uliongezeka na punde si punde, majani yale makavu yakashika moto na kuwaka. Mugai alimwagiza mtu huyo awe anautumia moto ule katika shughuli zake mbalimbali, zikiwemo shughuli za kumtolea Mungu kafara wakati wa ibada. Hapo basi pakawa moto umevumbuliwa na watu wakaanza kupika vyakula vyao na kuacha kuvila vikiwa vibichi.

Kisaasili hiki aidha chaonyesha ufundi mwingine wa Wakikuyu na asili yake. Moto uliweza kuvumbuliwa kutoka kwa Mugai. Yaonekana kuwa mara nyingi Mungu aliwasaidia Wakikuyu sana katika uvumbuzi wa mambo mbalimbali katika jamii.Akili ya Wakikuyu

katika uvumbuzi iliweza kutokana na Mungu, kulingana na visaasili vyao vingi na hivyo, wao kila mara hutenda mambo wakiwa na imani kuwa yatakuwa sawa.

Visaasili hivi na vingine vingi vyaonyesha kuwa Wakikuyu walipata uwezo wao wa kutenda mambo tofauti tofauti kutoka kwa Mungu ambaye, mara nyingi, aliwasaidia kutokana na bidii waliyokuwa nayo.

Jambo muhimu linalofunzwa na visaasili hivi, hata hivyo, linahusiana na umuhimu wa Wakikuyu kumtegemea Mungu katika yote watendayo.Wao waliamini, na bado huamini, kuwa pasipo na usaidizi wake Mungu, basi hawawezi kufaulu katika jitihada zao. Hii ndiyo sababu walikuwa tayari kila mara kumuomba Mungu na kumuomba mawaidha katika kutekeleza mambo mbalimbali katika maisha yao ya kila siku.

Kwa hivyo, kama zilivyo tanzu nyingine za Fasihi Simulizi,visaasili bila shaka ni utanzu ulio na umuhimu usio na kifani na hasa katika kutoa mafunzo muhimu kwa wanajamii na hivyo basi kuwamulikia maisha yao ya siku baada ya siku.

## 3.7 VISAASILI : KUBURUDISHA NA KUSTAREHESHA WATU KATIKA JAMII

Hadithi, vikiwemo visaasili, huburudisha, hufurahisha na kuhuisha jamii. Tuzingatie kwamba, katika jamii za kiasili, hadithi husimuliwa baada ya kazi wakati wa mapumuziko.Hadithi husaidia kujenga fikra na akili kutokana na tafakuri anayoitumia msikilizaji ili kupata maana, ujumbe na uzito wake. "Uburudishaji ndio madhumuni kuu ya watambaji na watambiwa katika hadithi. Mtambaji hujaribu kuwaburudisha wasikilizaji wake bila ya kutumia mbinu tata za mtindo. Mtambaji vile vile hujitahidi sana awafurahishe wasikilizaji wake, kwani asipofanya hivyo, huenda akawachosha akili (Scheub, 1975:165) akinukuliwa na Okpewho (1992:108).

Kwake Scheub, bila shaka, uburudishaji ndio huwa muhimu zaidi katika utambaji.Jambo muhimu pia ni kuwa watambaji wanapoendelea na shughuli zao, wasikilizaji na watazamaji vile vile huweza kujifunza mbinu mbalimbali zinazoweza

kuwasaidia baadaye katika kupiga msasa utambaji wao. Akili za fanani na hadhira hutulizwa kutokana na matatizo mbali mbali ya siku baada ya siku.

Miongoni mwa Wakikuyu, kuna visaasili ambavyo hutambwa kwa madhumuni ya kuwaburudisha hadhira. Kuna kisaasili kinachosema kuwa, zamani za kale wanyama wadogo walipenda kwenda karamuni kwenye nyanda za Makuyu. Mchwa hakuwa na mshipi na basi alimwendea rafiki yake Chawa na kumwazima mshipi wake.Mchwa alipokuwa anajaribu kujifunga mshipi ule rafiki yake alimwambia:"Tutaona ni nani kati yetu wawili ajuaye kucheza ngoma vizuri zaidi".

Baadaye wanyama hawa waliondoka na kwenda mtoni kuoga.Walipomaliza kuoga, waliketi mwambani ili waweze kukauka maji. Pia, walijipaka mafuta ambayo wanyama walijipaka walipokuwa wanaenda kwenye ngoma. Baada ya kujipamba vilivyo, Chawa alimwambia Mchwa,"Hebu tuone jinsi mshipi wako utakavyokuwa pamoja na upanga wako.Hm, nadhani uko sawa lakini hebu ukaze kidogo.Alipoyasikia yale, Mchwa aliukaza mshipi sana na akapata mfuo mpana kwenye kiuno chake.Chawa alicheka sana alipoona jinsi mshipi ulivyokuwa umemkaza Mchwa .Alicheka na kucheka hadi pua yake ikapasuka; na hivyo basi wadudu hao wawili hawangeweza kwenda ngomani.

Kisa hiki kina jukumu la kuburudisha, huku likitoa maelezo kuhusiana na maumbile ya wadudu wanaohusika. Inasemekana kuwa Chawa huwa hana pua ilhali Mchwa huwa ana mfuo mpana kiunoni unaomfanya aonekane kama aliye karibu sana kukatika kiuno.

Kuna kisaasili kuhusiana na chanzo cha Kuku kuishi na watu. Kisaasili hicho chasema kuwa, zamani Kuku waliishi msituni pamoja na wanyama wengine. Kuku waliwambia wanyama wenzao kuwa taji walizonazo vichwani zilitengezwa kwa moto na kuwa, yeyote ambaye angezigusa angechomwa na kufa. Hivyo basi, wanyama waliogopa sana kuvikaribia vichwa vya Kuku.

Siku moja, Chui alihitaji moto nyumbani mwake na hivyo alimtuma mwanaye akaombe moto nyumbani kwa Kuku. Mwana wa Chui alipofika nyumbani mwa Kuku, aliwakuta wote wamelala, na hivyo alirudi nyumbani na kumweleza mamake. Chui alimwambia mwanawe arudi tena nyumbani kwa Kuku akiwa na majani makavu ili awashe tu

moto bila ya kuwaamsha Kuku. Mwana wa Chui alifanya alivyoambiwa lakini alishindwa kuwasha moto kutoka kwa taji la Kuku. Alipomwambia mamake hivyo, Chui alifadhaika sana na kwenda mwenyewe nyumbani kwa kuku. Aliposhindwa kuwasha moto, aliwaamsha Kuku wote na kuwakemea huku akiwaambia kuwa amegundua hadaa zao. Tangu siku hiyo Kuku waliogopa sana kuishi Msituni na hivyo wakatoroka na kwenda nyumbani kwa wanadamu. Chui na wanyama wengine nao waliamua kuwa maadui wa Kuku na wakawa wanawashambulia walipowapata.

Matokeo ya kutamba kisaasili kama hiki ni kuiburudisha hadhira, mbali na kujaribu kutoa maelezo ya sababu ya maumbile au matukio fulani yaliyopo. Visaasili vyenye nia ya kuburudisha mara nyingi hupendwa sana, na hadhira humakinika tangu mwanzo hadi mwisho huku ikiwazia matukio yaliyopo katika visa hivyo. Katika kisaasili cha Kuku na Chui, hadhira inayotambiwa kisa hicho inaweza kushangaa kuhusiana na kutomakinika kwa wanyama wengine. Wanyama hao waliukubali ujanja wa Kuku, walipoambia kuwa sehemu iliyo kama taji kichwani mwake huwa ni moto. Hadhira inaburudishwa kwa vile inashangazwa na upofu wa wanyama hao. Je ikiwa kuku walikuwa wamebeba moto vichwani mwao, mbona wao hawakuteketea? Baada ya ujanja wao kugunduliwa na wenzao, kuku wanashikwa na woga na hivyo basi wanaamua kuishi majumbani mwa watu. Hadhira bila shaka inatumbuizwa vilivyo na ujanja wa kuku ambao ni wanyama wadogo sana miongoni mwa wengine.

Aidha kuna kisaasili miongoni mwa Wakikuyu ambacho huburudisha hadhira sana. Kisaasili hicho hueleza ni kwa nini Fisi huwa na mguu mifupi ya nyuma. Kulingana na kisaasili hicho, siku moja Fisi aliandamana na Njiwa kwenda kutafuta asali msituni. Njiwa alikuwa mjanja sana na alitaka kumtesa rafiki yake kutokana na tabia ya ulafi. Walipoingia msituni, Njiwa alipanda juu ya mti uliokuwa na asali na kumwambia Fisi afungue mdomo wake ili aweze kumrushia asali. Fisi alifanya kama alivyoagiziwa na alifurahi sana. Njiwa hata hivyo alimwambia kuwa, ingembidi afumwe sehemu yake ya makalio ili utamu wa asali usimalizike. Fisi, bila kusita, alikubali na basi Njiwa alikusanya miba kadha na kumshona Fisi sehemu yake ya kwendea choo. Wakati uliwadia ambapo Fisi alipatwa na haja ya kwenda choo asijue la kufanya. Alijaribu marafiki zake kama vile Sungura, Swara, Twiga na wengineo wamfumue sehemu yake ya nyuma lakini wote walikataa wakidai kuwa hawakutaka kuchafuliwa kwa kinyesi. Fisi alipatwa na maumivu mengi tumboni, kwani

lilikuwa limevimba na akawa anagaagaa mchangani kwa uchungu. Hapo karibu, Kunguru alikuwa anapita na akaona jinsi Fisi alivyohangaika. Kunguru alimwuliza shida yake na, bila kusita, Fisi alimuomba kwa huzuni sana amfumue sehemu yake ya nyuma kwani alikuwa yuafa. Kunguru alikubali kumsaidia Fisi na basi akaanza kuiondoa miba iliyokuwa imemfuma Fisi. Mara tu alipoondoa mwiba wa pili, alipigwa na mshangao kwani alikumbwa na kinyesi cheupe kilichomfunika kabisa. Kunguru alishindwa kuondoka alipokuwa na, ni baada ya mvua kunyesha siku tatu baadaye alipooshwa na kuweza kuondoka. Kunguru alikuwa na hasira nyingi sana kwani hakuwa msafi kabisa hata baada ya kunyeshewa; na hiyo ndio sababu yeye huwa na sehemu nyeupe shingoni mwake. Kunguru aliahidi kulipiza kisasi dhidi ya Fisi.

Siku moja Kunguru alisikia kuwa Fisi wote walikuwa na karamu kubwa mno. Kunguru alioga na kujipamba sana kwa marashi na shanga. Fisi walipomuona, walimsalimu na kumkaribisha kwenye karamu yao. Wengine, kutokana ulafi wao, walimuomba Kunguru awape vipande vya nyama alivyokuwa navyo shingoni na miguuni, kwani walidhani kuwa shanga zilikuwa vipande vya nyama. Kunguru aliwaambia kuwa hangeweza kuwapatia vipande hivyo wakati huo kwani vilikuwa tu vya ukoo wake. Hata hivyo, aliahidi kuwapeleka mbinguni ambako wangepata mapande makubwa makubwa ya nyama nono. Kunguru aliwaonyesha mawingu meupe na kuwaambia kuwa hayo yalikuwa mapande ya nyama na humo ndimo angewapeleka.

Fisi wote waliahidi kukutana na Kunguru siku iliyofuata ili wapelekwe mawinguni kwenye nyama. Siku iliyofuata, Fisi wote, wazee, vijana, watoto, na wagonjwa, walikusanyika na kumpata Kunguru tayari kuwapelekea kwenye safari yao. Kunguru aliwaambia wote wapige safu na kukamatana mikia; na aliyekuwa karibu na Kunguru kwenye msitari akaambiwa ayakamate manyoya ya nyuma ya Kunguru. Kisha, Kunguru alipuruka kuelekea mawinguni huku Fisi wote wakimfuata. Kunguru aliendelea kwenda juu na kuwauliza Fisi ikiwa wote walikuwa wametoka ardhini. Walipoitika, Kunguru alitaka kujua iwapo Fisi waliweza kuona chini, nao wakamjibu kuwa waliona giza. Hapo Kunguru alijua kuwa kwa kweli alikuwa mbali sana na ardhi. Mara tu alimwambia Fisi aliyeyakamata manyoya yake ayaache kidogo kwani alipatwa na mwasho fulani. Fisi huyo alikataa kata kata, akidai kuwa kama angeyaacha manyoya yale wote wangeanguka chini na kufa. Kunguru alikuwa amekwisha kuamua kulipiza kisasi, na basi alifutuka kwa nguvu zake zote

na hapo manyoya yake yakatoka. Hapo basi, Fisi wote walianguka chini puh! na kufa. Ni Fisi mmoja tu aliyekuwa mjamzito aliyenusurika, na hivyo, akaweza kuendeleza jamii ya Fisi. Hata hivyo wote waliozaliwa tangu wakati huo walikuwa na miguu mifupi ya nyuma, na hii ndiyo sababu ya Fisi huchechemea wanapotembea.

Kisaasili hiki bila shaka yoyote ni cha kuburudisha na kuchangamsha hadhira. Kwa vile wanyama watumiwao katika visaasili kama hivi hujulikana wazi kwa hadhira, maumbile yao huweza kueleweka vizuri zaidi kwa hadhira kutokana na ujuzi alionao fanani katika kutamba, na vile vile kuigiza mambo katika visa. Ukali wa Simba, urefu wa Twiga, na ukubwa wa Ndovu, yote ni maumbile ambayo huifurahisha hadhira inapotambiwa visa kuyahusu.

Kama tulivyotangulia kusema, uburudishaji wa Fasihi Simulizi huwa muhimu sana ingawa mara nyingi hupuuzwa. Utanzu wowote wa Fasihi Simulizi, mfano ngano, nyimbo, vitendawili ama methali, lazima ulenge kuiburudisha na kuistarehesha hadhira. Iwapo hadithi haiburidishi, basi haitaweza kupendwa na hadhira. Hapo, hadhira haitamakinika wakati wa utambaji wa hadithi hiyo.

Uburudishaji katika Fasihi Simulizi huwa wa aina mbili, kulingana na Lusweti (1984:12). Uburudishaji huo unaweza kutokana na visa au matukio ya kuchekesha. Aidha, uburudishaji unaweza kupatikana kupitia kwa uigizaji na ngoma. Hadithi, methali, vitendawili, mashairi na hata nyimbo huweza kuburudisha kwa kusikizwa tu, lakini kwa kiwango kikubwa, nyimbo huiburudisha hadhira zaidi kupitia kwa densi. Nyimbo za tohara kama vile `nzaiko' miongoni mwa Wakamba, `yatikaet' miongoni mwa Wanandi, `kimienya kie sikhebo' miongoni mwa Wabukusu na `chisimbore' miongoni mwa Wagusii, huwa na dhima kubwa na ni muhimu sana katika kuwatumbuiza wachezaji. Kwa kweli watu wengi huhudhuria sherehe kama hizo wakiwa na lengo la kujiburidisha. Vile vile, watu hutambiana au kuhudhuria vikao vya utambaji hadithi wakiwa na lengo la kujiburudisha na kutuliza akili zao baada ya kazi ngumu za kila siku.

## 3.8. <u>HITIMISHO</u>

Katika sura hii, tumevichambua visaasili kadha katika jamii ya Wakikuyu na kuonyesha matumizi yake katika jamii hiyo.

Baada ya kuvichambua visaasili hivyo, tumeona dhahiri kuwa visaasili vina uzito fulani katika kuendeleza jamii ya Wakikuyu. Ili kuweza kueleza matumizi hayo barabara, tulionelea kuwa ni bora kutoa maelezo kuhusu visaasili husika; yaani tumeviandika visaasili hivyo tulivyovikusanya ili yeyote atakayevisoma apate kuelewa hasa tunachochambua. Jambo hili ni muhimu kwani, mara nyingine, visaasili vya jamii mbalimbali huweza kufanana au kutofautiana kabisa. Sisi tumejikita katika maelezo ya visaasili vya Wakikuyu na hivyo iwapo visaasili hivyo vinatoa mafunzo tofauti katika jamii nyingine; hilo ni jambo linaloruhusiwa, kwani kila jamii huwa na thamani zake ambazo huikuza na kuiendeleza jamii hiyo.

Baadhi ya matumizi tuliyochambua kuhusiana na visaasili vya Wakikuyu ni kuelimisha jamii, kutawala jamii, kutoa madili katika jamii, kuonyesha ufundi wa Wakikuyu na aidha kuwaburudisha na kuwastarehesha watu katika jamii. Bila shaka, kuna matumizi chungu nzima ya visaasili, lakini haya tuliyochambua ndiyo tuliyoona kama muhimu na yanayotumika hata leo katika jamii ya Wakikuyu.

Sura hii kwa hivyo ni thibitisho kamili kuwa utanzu wa visaasilil haupaswi kupuuzwa hata kidogo au kuonekana kama ulio duni. Hii ni kwa sababu, kama tanzu nyingine zozote za Fasihi Simulizi, visaasili ni utanzu ulio na haki, uhuru na ulio na matumizi kemkem katika jamii yoyote ile.

## 3.9. TANBIHI

1. **Kirinyaga**

   Mlima huu uliitwa Kirinyaga kutokana na mwangaza wa theluji iliyopo juu ya mwamba mweusi wa mlima huo. Kutoka kwa mbali huonekana kama wenye mishororo mieupe na mieusi. Ngai, kiongozi wa Ulimwengu, pia hujulikana kama "Mwenenyaga", yaani anayemiliki mishororo ya Kirinyaga.

2. **Mukurwe Wa Gathanga**

   Au Mukurwe wa Nyagathanga huwa katika kata ya Gaturi, tarafa ya Kiharu wilayani Murang'a, karibu kilomita ishirini kutoka Mji wa Murang'a.

3. **Murungu**

Katika sala, Mugai, mwenye uwezo, hujulikana pia kama Murungu `Mwenehiya'. Murungu ndilo jina asili la Mungu kwa makundi mengi ya Kibantu lililoazimwa kutoka kwa jina la mzizi "dungu."

4. Murungu pia hujulikana kama ngai yaani anayegawa.

5. **"Thaai thathaiya Ngai thaai"**

   Ni maneno yaliyotumika sana wakati wa sala na yana maana ya "utukufu kwa Mungu, amani iwe kwetu".

6. **Ndemi** - ni jina litokanalo na `tema' lenye maana kata au `gutema', kukata.

7. **Iregi** - ni jina litokanalo na `rega' lenye maana ya kataa au `kurega', kukataa.

8. **Njama ya itwika** - ni baraza lililoundwa baada ya mapinduzi ya kumng'oa mfalme Gikuyu mamlakani na kuunda Serikali mpya `Itwika' - ni jina litokanalo na `twika' lenye maana ya kukatika.

9. **Muringa** - ni aina ya mti mkubwa sana upatikanao kwa Wakikuyu.

# SURA YA NNE

## 4.0 VISAASILI :MBINU ZA USANAA.

### 4.1 UTANGULIZI

Kile ambacho tumejaribu kufanya katika sura hii, ni kuchunguza utanzu wa visaasili kama fani ya Fasihi Simulizi na kuonyesha jinsi vilivyo na usanii na ubunifu sawa na tanzu nyingine. Sura hii, kwa hivyo, itaonyesha haki za utanzu wa visaasili kama uliokamilika na ulio na usanaa kamili.

Ingawa maneno yatumiwayo katika fasihi ni lugha, matumizi ya lugha hiyo huwa tofauti, kwa mfano, na maongezi ya kawaida. Sifa kuu ya namna ya lugha ya visaasili ni matumizi ya lugha ya tamathali kueleza maswala kadha wa kadha. Matumizi ya lugha kwa njia hiyo (ya tamathali) huwa na makusudio maalum wala sio ya kiholela. Mambo yasiyowezekana hutumiwa tu kama mifano ya kueleza mambo yanayowezekana, na yale yasiyo kweli hutumiwa kueleza yaliyo kweli.

Hii ina maana kuwa, ujuzi ama ufahamu wa maneno ya lugha pekee hautoshi, bali kinachohitajika ni kutambua usanii unaotumika katika visaasili kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe. Kwa njia hii, lugha huwa ndiyo mali ghafi itumiwayo kuumba visaasili.

### 4.2 MBINU ZA USANAA KATIKA VISAASILI

Mbinu hizi ni nyingi na tutajaribu kuonyesha jinsi baadhi ya mbinu hizo zinavyojitokeza katika visaasili tulivyochambua. Miongoni mwa mbinu tutakazozingatia ni:-

- tashihisi au uhaishaji
- chuku
- taharuki
- tanakali - sauti

- takriri
- ucheshi
- metonumia (au taashira)
- dhihaka
- tasifida
- majazi
- taniaba

Katika uchambuzi wetu, tutaeleza hadithi husika na kuonyesha jinsi mbinu mbalimbali za usanaa zinavyojitokeza.

## HADITHI YA ASILI YA WAKIKUYU:

Kisa hiki, kama tulivyokieleza katika sura ya tatu, kinaonyesha mbinu kadha za usanaa kama vile:-

### TANIABA:

Tunaona kuwa kuna matumizi ya mbinu ya taniaba katika kisa hicho. Mbinu hiyo ya taniaba huonyesha kuwa kitu fulani ni badala ya kitu kingine. Kwa mfano Gikuyu anaashiria dhana ya maisha miongoni mwa Wakikuyu. Yeye amechukua mahali pa Adamu katika Agano la kale. Naye Mumbi anachukua dhana ya kuwaumba wakikuyu kwani hata jina lake linatokana na kitendo cha 'kuumba'. Taniaba aidha yajitokeza katika majina ya binti za Mumbi kwani majina hayo hutumiwa kwa niaba ya koo tisa za kabila la Wakikuyu.

### MAJAZI:

Msemo huu huashiria maana ya kitu kizima mara ikitamkwa sehemu tu ya kitu hicho. Majazi ni aina ya istiara, ambapo pia kitu kizima kikitajwa huwakilisha dhana ya sehemu ya kitu hicho. Katika kisa cha asili ya Wakikuyu, tunaelezwa kuwa koo zote tisa za Wakikuyu ziliunganishwa na kujulikana kama "Nyumba ya Mumbi " au "Mbari ya Mumbi". Baadaye tunafahamishwa kwamba koo hizo zilijulikana kama "Nyumba ya Gikuyu" au "Mbari ya Gikuyu". Majazi yanajitokeza kwa vile utajapo tu jina la Gikuyu ambaye ndiye baba wa kabila la Wakikuyu, utakuwa pia unaashiria kabila hilo.

CHUKU:

Katika kisa cha asili ya Wakikuyu, jinsi wanaume tisa walivyoletwa kwa jamii ya Gikuyu na Mumbi yadhihirisha chuku. Tunaarifiwa katika sura ya tatu kuwa, Gikuyu aliarifiwa na Mungu alete vijiti tisa, huku kila kijiti kikiwa na urefu wa binti mmoja wa Gikuyu. Wakati wa ibada, Gikuyu aliwasha moto kwa kutumia vijiti hivyo na hapo palitokea wanaume tisa walioozwa binti za Gikuyu. Kitendo hicho bila shaka kinazusha chuku kwa vile wanaume hao hawakuzaliwa jinsi binti za Gikuyu na Mumbi walivyokuwa wamezaliwa.

TAHARUKI:

Katika kisa hicho, jinsi Mungu (Murungu) alivyoanza kazi yake ya kuumba Ulimwengu inavutia sana. Baada ya Mungu kugawanya Ulimwengu, inasemekana kuwa yeye alimwiita Gikuyu na kumkabidhi sehemu yake ya ardhi. Hadhira bila shaka inaweza kuwa na taharuki ya kutaka kujua jinsi Mungu alivyomtaka Gikuyu aujaze Ulimwengu. Hivyo basi, jinsi Mungu alivyomwongoza Gikuyu hadi mahali paitwapo Mukurwe - wa - Gathangu na kumpa mke ni jambo la kuvutia sana. Kisa hicho aidha kina taharuki kuhusiana na jinsi Gikuyu alivyohitajika kufanya ibada au maombi kwa Mungu. Kisa hicho kwa ujumla kinaiacha hadhira katika taharuki kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hii ni kwa sababu baada ya Mungu kuumba kitu fulani, hadhira hubaki na hamu ya kutaka kujua ni kitu kipi kilitengenezwa baadaye na kwa njia gani.

TAKRIRI:

Kisa cha asili ya Wakikuyu, kinatuarifu jinsi Wakikuyu walivyohitajika kutoa maombi yao kwa Mungu. Baada ya kuutazama mlima wa Kirinyanga, watu hao walitakiwa wainue mikono yao juu na kutamka maneno matakatifu;

"Thaai thathaiya Ngai thaai". Kila baada ya kutaja ombi walisema "uthaai", na mwishowe wakamalizia kwa maneno hayo ya "Thaai thathaiya Ngai thaai". Takriri ya maneno hayo yaonyesha hali ya msisitizo uliohitajika katika sala. Takriri ya neno "thaai" inadhihirisha utukufu na utakatifu wa Mungu. Wakikuyu waliamini kuwa bila msisitizo kama huo kuwepo, basi sala zao hazingeweza kumfikia Mungu.

## HADITHI ZA ASILI YA KIFO:

Kama tulivyotaja katika sura ya tatu, kuna visa viwili kuhusu asili ya kifo miongoni mwa Wakikuyu. Mbinu za usanaa zilizomo katika hadithi hizo ni kama vile:-

TAKRIRI:

Katika kisa cha kwanza kinachoeleza asili ya kifo, Kinyonga alitumwa na Mungu kwenda kuwapa watu ujumbe wa kuishi milele. Twaona kuwa Kinyonga aliyakariri maneno fulani kwa muda mrefu sana. Takriri na kigugumizi chake ndicho kilichosababisha kifo kwani mnyama aliyekuwa na mbio zaidi aliweza kuwasili na ujumbe uliokuwa kinyume kabisa na ule wa Kinyonga.

Wakati Kinyonga alipokuwa anajitahidi kutoa ujumbe alikariri maneno:-

"Ni - ni - ni li - li - lia - a - a - mbi - mbi - wa - a

"Ni - ni - ni li - li - lia - a - a - mbi - mbi - wa - a

Kinyonga aliyakariri tu maneno bila ya kueleza kwa kinaga ubaga ujumbe aliokuwa nao; na kwa hivyo yeye hulaumiwa miongoni mwa Wakikuyu kuwa alisababisha kifo. Takriri ya kinyonga ilinuia hasa katika kutilia mkazo ujumbe aliokuwa nao, lakini yaonekana alikuwa ameusahau ujumbe huo, na basi akawa anayerudiarudia maneno fulani tu.

NIDAA:

Huu ni msemo ambao unaonyesha kushangazwa kwa jambo fulani. Misemo ya aina hii huambatana na matumizi ya alama za mshangao, kukubali jambo, na kuonyesha heshima maalum. Katika hadithi ya pili ya asili ya kifo, Mfalme wa dunia alimchagua Kindi kwenda na Mfalme Ruia mlimani kuleta dawa ya kuzuia kifo. Wanawake walipomuaona Kindi amejipamba na amevaa tayari kuondoka, walimshang-ilia kwa vigelegele:

"Aririririri - riiiii, Aririririri - riii -'.

Naye Kindi alipoona heshima aliyotunukiwa alifurahi na kuwajibu

"Hii - hii ! - Yiii - hiii.

TASHIHISI:

Katika hadithi mbili za Wakikuyu zinazoeleza asili ya kifo, mbinu ya tashihisi imedhihirika sana. Katika mbinu hii vitu au viumbe mbalimbali hupewa sifa na uwezo wa wanadamu.

Katika hadithi ya kwanza, Kinyonga na ndege "Nyamindigi" wote wamepewa sifa ya kuweza kuzungumza. Kwa hivyo viumbe hivyo vinatumwa kwa wanadamu vikiwa na ujumbe muhimu kuhusu kifo. Uwezo huo wa kuzungumza ndio unaomfanya Kinyonga ashindwe kuufikisha ujumbe aliopewa na Mungu vilivyo. Ndege "Nyamindigi", kwa kuweza kuzungumza kwa haraka, anaufikisha ujumbe wake na hapo watu wanaendelea kukabiliwa na tatizo la kifo.

Katika hadithi ya pili ya kifo, wanyama kama vile Kindi na Fisi wamepewa uwezo wa kuzungumza. Aidha jua limehaishwa na kupewa dhima ya ufalme na hivyo basi uwezo wa kibinadamu. Yaelekea kuwa viumbe au wanyama na pia wanadamu katika hadithi hizi mbili wote wana uwezo sawa mbele ya Mungu.

**TAHARUKI**

Hadithi za asili ya kifo zina taharuki kwani hadhira bila shaka inaachwa na hamu ya kutaka kujua hali ilivyokuwa baada ya viumbe au wanyama mbalimbali kutumwa kwa wanadamu. Katika hadithi ya kwanza, kwa mfano, kuna taharuki ya kutaka kujua iwapo Kinyoga aliweza kuufikisha ujumbe aliopewa kwa wakati unaofaa. Aidha kuna taharuki ya kutaka kujua jinsi ndege "Nyamindigi" alivyoweza kuufikisha ujumbe wake.

Pia katika hadithi ya pili, kuna taharuki ya kutaka kujua jinsi Kindi alivyoweza kukabiliana na Fisi aliyemvamia. Pia, jambo Fisi alilofanya na dawa aliyomnyang'anya Kindi, ni jambo linalozua taharuki kubwa.

## MSISITIZO BAYANI:

Hii ni tamathali inayoonyesha ushindani wa mawazo. Ni tamathali inayoisisitiza maana ya sentensi kwa kutumia kinyume. Katika hadithi ya kwanza kuhusu asili ya kifo, tunaona hali ya msisitizo bayani kupitia kwa wahusika wakuu ambao ni Kinyonga na ndege "Nyamindigi". Mbinu hii inajitokeza hasa tunapoona maneno ya wahusika hao. Kinyonga alitumwa kwanza na Mungu akiwa na ujumbe kuwa, watu watafufuka baada ya kufa. Naye ndege "Nyamindigi" ana maneno yaliyo kinyume na hayo ya Kinyonga. Maana ya maneno ya "Nyamindigi" inajitokeza baada ya ndege huyo kusisitiza kinyume cha maneno ya ujumbe tofauti kabisa, kuwa, watu wakifa hawataweza kufufuka tena.

## HADITHI YA ASILI YA UONGOZI.

Hadithi hii kama ilivyo katika sura ya tatu, ina mbinu zifuatazo:-

### CHUKU:

Kulingana na hadithi hii, yasemekana kuwa wanaume walipanga njama na kuamua kuwatunga wanawake wote mimba. Yasemekana kuwa baada ya kutekeleza jambo hilo, wanawake wote walishika mimba kwa wakati mmoja, jambo lililowafanya wadhoofike sana na kuweza kupinduliwa na wanaume. Chuku yadhihirika wazi kwani jambo kama hilo haliwezekani hata kidogo. Haiwezekani, kwa mfano, wanawake wote nchini au katika eneo fulani kuweza kupata mimba kwa wakati mmoja. Hii ni kwa sababu wanawake wote wana nyakati fulani ambamo wanaweza kushika mimba, na wala sio kila wakati, na hizo nyakati zinatofautiana.

### USAMBAMBA

Katika hadithi ya asili ya uongozi, hali ya uongozi inadhihirisha usambamba fulani. Yasemekana kuwa, mwanzoni, wanawake ndio waliokuwa viongozi. Baada ya mapinduzi, uongozi huo ulibadilika na kuwa wa wanaume. Ili uongozi miongoni mwa

jamii ya Wakikuyu ueleweke zaidi, hali ya usambamba uliokuwepo pia yafaa ieleweke vilivyo.

MAJAZI

Katika hadithi hiyo, yasemekana kuwa baada ya mapinduzi, mambo kadha yalibadilishwa. Wanaume waliamua kubadilisha jina asilia la kabila lao na pia majina ya mbari zao na kuyaweka chini ya mfumo wa utawala wa wanaume. Hivyo walifaulu katika kubadilisha jina la kabila lao kutoka kwa "Ruriri rwa Mbari ya Mumbi" na kuwa "Ruriri rwa Gikuyu" yaani "Watoto wa Gikuyu". Mbinu ya majazi inajitokeza wazi katika jina "Gikuyu". Hii ni kwa sababu, hata sasa, jina la "Gikuyu" linapotajwa huwa linaashiria kabila lote la Agikuyu kwa ujumla. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kabila hilo lilipewa jina la mwanzilishi wake aliyekuwa ni Gikuyu.

## HADITHI YA ASILI YA UMILIKAJI NA UGAWANYAJI ARDHI MIONGONI MWA WAKIKUYU.

Katika sura ya tatu, kuna kisa kinachoeleza jinsi ardhi ilivyogawanywa na Mungu baina ya Wakikuyu na makabila mengine. Kisa hicho kinaonyesha mbinu kadha za usanaa:-

CHUKU:

Yasemekana kuwa baada ya Wakikuyu kupewa sehemu ya Mukurwe - wa - Gathanga, wao waliongezeka sana kwa idadi na basi ikawabidi kuhama na kuelekea kwingineko.Wakikuyu walielekea sehemu za msituni na kuwakuta Wapijini. Tunavyoelezwa kuhusu Wapijini walivyoishi kunadhihirisha chuku. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa Wapijini hao walikuwa wamejenga nyumba zao "chini ya ardhi" na basi waliweza "kutokea" na "kutoweka" jinsi walivyotaka. Aidha, kitendo kuhusu kutoweka kabisa kwa Wapijini kinadhihirisha chuku. Chuku hiyo yaonekana kwa vile tunaelezwa kuwa Wapijini walishidwa kufanya mazingaombwe yao na basi wakapotelea kabisa chini ya ardhi. Yamkinika kuwa Wapijini hao walipotea na kwenda Zaire.

TAHARUKI

Kisa hicho kimejaa taharuki. Taharuki hiyo ni kutokana na jinsi inavyoseme-

kana kuwa makabila fulani "yalitoweka" na mengine "yakazuka". Kitendo cha kupotea kabisa kwa Wapijini, kwa mfano, ni cha kushangaza. Hadhira, bila shaka, inaposikiliza hadithi hii ingetaka kujua iwapo kuna makabila mengine yaliyozuka baadaye, na pia jinsi makabila hayo yalivyoweza kuingiliana na Wakikuyu.

TABAINI

Mbinu hii inajitokeza wazi katika hadithi hiyo. Mbinu ya tabaini hasa inajitokeza wakati makabila ya Wakikuyu, Wapijini na Wandorobo yanapolinganishwa. Yasemekana kuwa Wandorobo walitokea baada ya kutoweka kwa Wapijini. Mfano wa tabaini ni kama vile kusema kuwa Wandorobo walikuwa warefu, tofauti na Wapijini walivyokuwa. Wapijini hawakuishi chini ya ardhi bali walijenga nyumba zao ardhini. Pia yasemekana kwamba Wandorobo hawakuwa wakulima kama Wakikuyu, bali walikuwa wawindaji.

Mbinu ya tabaini inaonekana katika hali ya ukinzani katika kuyalinganisha makabila hayo.

TASHIBIHI

Tamathali ya aina hii hutumia mlinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi "kama", "mfano wa", "mithali ya" n.k.

Katika hadithi ya asili ya umilikaji ardhi miongoni mwa Wakikuyu, mbinu ya tashibiha inaokana katika kueleza hali ya makabila mbalimbali ilivyokuwa. Mfano mzuri ni katika kueleza Wandorobo walivyokuwa. Wandorobo, yasemekana, walikuwa wengi mno kwa idadi na ongezeko lao lilikuwa kama "kukua kwa uyoga msituni".

**HADITHI YA KUKU NA MWEWE**

Kama inavyoelezwa katika sura ya tatu, hadithi hii inaeleza ni kwa nini Kuku huchakurachakura, na pia inaeleza sababu ya Mwewe kuwavamia vifaranga wa Kuku. Ingawa hadithi hii ni fupi, inadhihirisha mbinu kadha za usanaa kama vile:-

TASHIHISI

Kuku na Mwewe wamepewa sifa na uwezo wa kibinadamu. Yasemekana kuwa Kuku alimuazima mwewe sindano yake na akaipoteza. Ni dhahiri kuwa Kuku na Mwewe waliweza kuzungumza, jambo ambalo si la kawaida.

Pia, ndege hao walikosana kwa vile Kuku aliipoteza sindano ya Mwewe. Yaelekea ndege hao walikuwa na matumizi fulani ya sindano. Wanadamu ndio viumbe watumiao vifaa kama vile sindano, na hapo basi ndege hao (Kuku na Mwewe) wamepewa sifa za kibinadamu.

TAHARUKI

Kisa hiki kinadhihirisha taharuki, kwani, baada ya Kuku kuipoteza sindano ya Mwewe, yeye huwapoteza vifaranga wake kwa Mwewe. Taharuki ipo kwa sababu hatujui iwapo siku itawadia ambapo Kuku ataipata sindano ya Mwewe. Iwapo kuku hataipata sindano hiyo, basi Mwewe naye hataacha kuwavamia vifaranga wa kuku.

**HADITHI YA SUNGURA NA BUIBUI.**

Hadithi hii, kama ilivyo katika sura ya tatu, inaeleza ni kwa nini sungura ana masikio marefu. Mbinu kadha za usanaa zinajitokeza katika hadithi hiyo kama vile:-

CHUKU

Kulingana na hadithi ya Sungura na Buibui, ni wazi kabisa kuwa jambo la kiumbe kama vile Sungura kuteremshwa kutoka mbinguni kwa nyuzi haliwezekani. Pia haiwezekani kwa mdudu kama Buibui kuweza kufika mbinguni kwa kutumia utandabui wake.

TANAKALI - SAUTI:

Yasemekana katika hadithi hiyo kuwa, mara tu Sungura alipoachwa mbinguni na Buibui, alianza kulia kwa masikitiko kwani hakujua jinsi ya kurudi Ulimwenguni. Basi hapo, mzee mmoja alijitolea kumsaidia Sungura na aliwaambia watu wafume nyuzi ambazo zingetumiwa katika kumteremsha Sungura chini. Sungura alipofungwa nyuzi hizo kwenye masikio, aliambiwa kuwa azitingishe alipoweza kufika duniani ili kuwaarifu watu wa mbinguni kuwa alikuwa amefika. Sungura aliweza kufanya hivyo kiajali kabla ya kufika duniani, na basi watu wa mbinguni waliweza kuziachilia nyuzi.

Yasemekana kuwa mara Sungura alianguka chini kwa nguvu puh! puh!. Tanakali - sauti katika kisa hiki yaonyesha uzito au nguvu alizoanguka nazo Sungura.

TAHARUKI

Hadithi ya Sungura na Buibui inadhihirisha taharuki kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hii ni kwa sababu hadhira, katika huisikiza hadithi hiyo, itakuwa na hamu ya kutaka kujua hatua Buibui aliyoichukua baada ya kupotezewa wapenzi au wachumba na Sungura. Aidha hadhira inaweza kuwa na hamu ya kutaka kujua jinsi Buibui na Sungura walivyoweza kufika mbinguni, na jinsi Sungura alivyoweza kurudi ulimwenguni baada ya kuachwa na Buibui.

KIJEMBE

Katika hadithi hiyo Sungura na Buibui, mbinu ya kijembe inajitokeza wazi kabisa. Kijembe ni usemi wa mzunguko; ni usemi wa kifumbo na humsema mtu kwa ubaya. Yasemekana kuwa Sungura aliwafitini wachumba wa Buibui kwa kuzungumza mambo mabaya kumhusu Buibui. Sungura kila mara aliweza kuwaambia wachumba wa Buibui kuwa, iwapo wangekubali kuolewa naye Buibui, wao wangeweza kuchoka sana, kwa kuteka mitungi mingi ya maji. Sungura pia aliwadanganya wapenzi wake Buibui kuwa, yeye (Buibui) alitumia mtungi mmoja wa maji kuoshea mguu wake mmoja kila siku. Sungura, bila shaka, alitumia kijembe kuwaonyesha wachumba wa Buibui kuwa Buibui hakustahili kuwaoa. Kijembe cha Sungura kilimfanya Buibui awakose wasichana wengi aliowapenda. Kijembe katika kisa hiki kinaonekana kwa sababu Sungura anawaeleza wachumba wa Buibui sifa mbaya kumhusu Buibui, na hivyo Buibui anakataliwa na wachumba wengi.

TASHIHISI

Mbinu hii ya usanaa inajitokeza wazi katika hadithi hiyo. Tashihisi inadhihirika tunapozingatia jinsi Sungura na Buibui wanavyopewa sifa za kibinadamu. Yasemekana kuwa Sungura na Buibui walikuwa marafiki wakubwa na, aidha, kwamba walitembeleana sana na kuzungumza. Sifa ya kuweza kuzungumza, inawafanya wanyama hao waweze kuwasiliana kama wanadamu. Pia, kuna vitendo wanavyoshiriki Buibui na Sungura ambavyo mara nyingi huwa vya wanadamu. Kwa mfano, kitendo

cha Buibui kubeba mtungi wa maji, na kuelekea mtoni kuteka maji ni jambo la kawaida miongoni mwa wanadamu. Kwa hivyo, Buibui na Sungura wamepewa dhima na sifa za wanadamu.

**HADITHI YA NYOKA NA TANDU**

Katika sura ya tatu, kuna hadithi inayoeleza sababu ya nyoka kuwa hana miguu. Pia hadithi hiyo inaeleza sababu ya tandu kuwa hana macho. Hadithi hiyo ina mbinu kadha za usanaa kama vile:-

CHUKU:

Katika hadithi hiyo ya Nyoka na Tandu, kitendo cha Nyoka kuitoa miguu yake na kumpa Tandu; naye Tandu kuyang'oa macho yake na kumpa Nyoka ni chuku tupu. Haiwezekani kamwe kiumbe yeyote yule, isipokuwa binadamu, aweze kung'oa viungo fulani vya mwili wake na kuvipachika kwenye mwili wa kiumbe kingine.

TASHIHISI

Mbinu ya tashihisi inadhihirika wazi kabisa katika hadithi hiyo. Uwezo wa kuzumgumza waliopewa Nyoka na Tandu, ni wa kibinadamu. Wanyama hao wanatembeleana, wanajadiliana na hata wanaazimana viungo vya miili yao. Bila shaka hata kitendo cha kutoa kiungo cha mnyama mmoja, na kukipachika kwa mnyama mwingine, ni kitendo kinachofanywa tu na binadamu. Binadamu siku hizi, kupitia kwa ujuzi wa kisayansi, huweza kutoa kiungo au viungo fulani kutoka kwa mtu mmoja na kukipachika au kuvipachika kwa mtu mwingine.

**HADITHI YA ASILI YA UHUNZI:**

Hadithi inayoeleza asili ya uhunzi miongoni mwa Wakikuyu imeelezwa katika sura ya tatu. Katika hadithi hiyo, mbinu za usanaa zilizojitokeza ni:-

TAHARUKI

Hadithi ya asili ya uhunzi imeeleza jinsi, baada ya wanyama kutoroka kutoka kwa wanawake, wanaume walivyoona ni heri wamwendee Mungu na kumwuliza jinsi walivyopaswa kuwachinja wanyama hao. Katika kusikiza hadithi hiyo, labda hadhira

huweza kukumbwa na taharuki katika kutaka kujua yale yalioelezwa na Mungu na pia jinsi binadamu alivyopewa mawaidha ya uhunzi. Hatua mbalimbali za ufuaji wa chuma, kama zilivyoelezwa na Mungu, bila shaka zinasababisha taharuki; kwani baada ya hatua moja, hadhira huwa na hamu ya kutaka kujua hatua inayofuata. Hiyo hamu ina jukumu la kuifanya hadhira imakinike kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kisa kwa kutaka kutosheleza hamu iliyopo.

TASHIHISI

Yasemekana katika hadithi hiyo kuwa, Mungu aliwagawia wanaume na wanawake wanyama mbalimbali. Wanyama waliomilikiwa na wanawake walihisi uchungu mwingi wakati na kuchinjwa, kwani wanawake walitumia vifaa butu katika kuwachinja wanyama hao. Yasemekana kuwa wanyama hao walikutana, wakazungumza na kupanga njama ya kutoroka. Wanyama hao walifaulu na basi kukawa na wanyama wa mwituni na wa nyumbani. Wanyama wa mwituni ni wale waliotoroka, nao wa nyumbani ni hao waliosalia, na hasa waliomilikiwa na wanaume.

Wanyama katika hadithi hii wamepewa sifa za kibinadamu kwa kuweza kuzungumza, na kupanga mipango.

DHIHAKA

Katika hadithi hiyo, yasemekana kuwa baada ya wanyama waliomilikiwa na wanawake kutoroka, wanawake walijaribu sana kuwapata wanyama hao. Wanawake waliposhindwa kuwarudisha wanyama wao, walimwendea Mungu na kumuomba msaada. Mungu aliwadhihaki wanawake kutokana na vitendo vyao vibaya na akakataa katakata kuwasaidia katika kuwapata wanyama wao. Dhihaka ya Mungu kwa wanawake ilidhihirika wazi baada ya Mungu kuwapatia wanaume ujuzi wa kufua chuma. Hata hivyo Mungu aliwaambia wanaume wawafunze wanawake ujuzi huo.

## HADITHI YA MCHWA NA CHAWA

Kama ilivyo katika sura ya tatu, hadithi ya Mchwa na Chawa inaeleza sababu ya Mchwa kuwa na kiuno chembamba na aidha, sababu ya kuharibika kwa pua ya Chawa. Hadithi hii inadhihirisha mbinu za usanaa kama vile:-

## CHUKU:

Katika hadithi hiyo ya Mchwa na Chawa, vitendo vya Mchwa kujifunga mshipi hadi kiuno chake kikakaribia kukatika na aidha Chawa alivyoweza kucheka kwa nguvu sana hadi pua yake ikapasuka vyaonyesha chuku. Tunajua wazi kuwa haiwezekani kwa kicheko kusababisha jambo kama kupasuka kwa pua. Aidha ni wazi kuwa kitendo cha mshipi kukaribia kukikata kiuno cha Mchwa alipokuwa anajitayarisha kuelekea karamuni ni habari zinazosisimua sana lakini si za kweli. Kisa hicho, kwa hivyo, kimejaa chuku ili kufanikisha maudhui. Kama tulivyotangulia kueleza, kisa hicho kinaeleza ni kwa nini Mchwa hana pua na pia ni kwa nini mchwa ana kiuno chembamba. Ili kuweza kutosheleza mahitaji ya kisa chenyewe, yaani kutoa maelezo fulani kuhusiana na maumbile ya wadudu hao, inakuwa ni muhimu kutoa maelezo hayo na pia kubuni matukio kisanaa.

## UCHESHI

Ingawa lengo kuu la hadithi hiyo yamkini ni kutoa sababu za maumbile ya wadudu hao, ndani yake mna ucheshi mwingi. Jinsi wadudu hao walivyokuwa wamejitahidi vilivyo kujitayarisha kwenda karamuni, na yaliyotokea, yote yanachekesha mno. Kwa mfano, kitendo cha Mchwa kujikaza sana mshipi kiunoni na kukaribia kukata kiuno chake, na aidha kitendo cha Chawa kumcheka Mchwa hadi pua yake ikapasuka, bila shaka vinaburudisha vilivyo. Matumizi ya ucheshi huweza kuifanya hadhira imakinike na aidha huiongezea hamu ya kutaka kusikiliza hadithi au kisa hadi mwisho.

## TASHIHISI

Katika hadithi ya Chawa na Mchwa, wadudu hao wamepewa sifa za kibinadamu. Wao wanaweza kuzungumza, na ni katika majadiliano yao ndipo wanapoelezana kuhusu mwaliko wa kuhudhuria sherehe za harusi. Wadudu hao wanakumbwa na mikasa iliyowapata baada ya kuzungumza na kuelewana. Hapo basi

katika matayarisho yao, mchwa anakaribia kujikata kiuno ilihali Chawa anamcheka hadi pua yake (Chawa) inapopasuka.

## HADITHI YA FISI, NJIWA NA KUNGURU

Hadithi hii ipo katika sura ya tatu, na inaeleza ni kwa nini Fisi huwa na miguu mifupi ya nyuma.. Aidha, hadithi hii inaeleza ni kwa nini kunguru huwa na sehemu nyeupe shingoni. Hadithi hii ina mbinu kadha za usanaa.

### TASHIHISI

Katika kisaasili hiki, twaona kuwa Njiwa, Kunguru na Fisi wote wanapewa sifa za kibinadamu hata ijapo kwa kawaida tunajua kuwa ndege na wanyama hawazungumzi. Hata hivyo, ili maudhui ya kisaasili hiki ipate kujitokeza vizuri na kueleweka kwa urahisi, twaona viumbe hawa wakiwasiliana kwa mazungumzo.

### TANAKALI - SAUTI

Hadithi hiyo ina matumizi ya tanakali-sauti. Yasemekana kuwa baada ya Fisi wote kuhadaiwa na Kunguru na wakakubali kumfuata kuelekea mawinguni, Kunguru alijitahidi sana kuhakikisha kuwa manyoya yake yamenyoyoka. Baada ya manyoya hayo kunyonyoka, Fisi wote walianguka chini kwa kasi sana kwani walikuwa wameyashika manyoya hayo. Fisi hao wote, kwa hivyo, walianguka chini puh! na kufa. Tanakali-sauti hiyo yaonyesha, bila shaka yoyote, kuwa walianguka kwa Nguvu sana na hivyo basi wakafa.

### UCHESHI

Hadithi ya Fisi, Kunguru na Njiwa inaonyesha hali ya ucheshi. Jambo kama lile la fisi kuamua kufumwa sehemu yake ya makalio ili utamu wa asali usimtoke linachekesha sana. Aidha, mpangilio wa matukio tangu Fisi alipofumwa, alipofumuliwa, na matokeo yake, na aidha kisasi alicholipizwa na Kunguru, waonyesha dhahiri kuwa kisaasili hicho kimejaa uchesi kwa vile tu lengo lake ni kuburudisha hadhira.

TASIFIDA

Tamathali hii husisitiza matumizi ya lugha kwa "adabu" ama kwa "kuficha" maneno makali. Katika hadithi hiyo, mbinu ya tasifida imetumika hasa tunapoona maneno kama vile:

- Fisi alifumwa sehemu yake ya nyuma au ya makalio.
- Fisi alipatwa na maumivu baada ya kushindwa kujisaidia au kwenda haja.
- Kunguru alifunikwa na kinyesi cha Fisi mara tu yeye (Kunguru) alipomfumua Fisi.

CHUKU

Hadithi hiyo inadhihirisha chuku, hasa tunapoelezwa mkasa uliowapata Fisi. Kitendo cha Fisi wote kukamatana mikia huku wakiwa wameyashikilia manyoya ya Kunguru ni chuku. Ni jambo lisilowezekana, kwa mfano, kwa Fisi wote waliokuwepo kuweza kubebwa na Kunguru ambaye ni ndege mdogo tu. Chuku imetumika katika hadithi hiyo ili iweze kukamilisha maudhui ya hadithi vilivyo.

DHIHAKA

Katika hadithi hiyo, mbinu ya dhihaka inaonekana wazi hasa kupitia kwa mhusika Kunguru, ambaye, baada ya kuchafuliwa na kinyesi cha Fisi, aliamua kulipiza kisasi. Kunguru aliwadhihaki Fisi wote na hivyo basi aliamua kuwadhuru wote. Dhihaka ndiyo iliyowafanya Fisi wote wafe kwani kama Kunguru hangewadhihaki, yeye pengine angemwadhibu tu yule Fisi mmoja aliyekuwa na kisasi naye. Dhihaka ndiyo iliyofanya maumbile ya Fisi yabadilike.

## 4.3 HITIMISHO:

Katika sura hii, tumejaribu kuonyesha usanaa uliopo katika utanzu wa visaasili. Kutokana na mifano na maelezo tuliyotoa, bila shaka tumedhihirisha kuwa utanzu huo una haki ya kuwa na mbinu za usanaa kama tanzu nyingine za Fasihi Simulizi.

Mafanikio ya fanani katika utambaji yanategemea mafanikio yake katika kukuza fikra, na kuuangalia Ulimwengu na kuutafsiri, kupanua akili, hisia za hadhira na kujifunza kutoka kwa wengine au katika kazi yake. Hivyo basi, mbinu za usanaa zinapatikana katika tanzu tofauti tofauti za Fasihi Simulizi na fanani huwa na nafasi kubwa sana katika kufanikisha usanaa uliopo. Hii ni kwa sababu kuna mbinu nyingine ambazo hueleweka vizuri sana kulingana na uwezo wa fanani, kwa mfano mbinu za matumizi ya ucheshi na takriri. Kwa hivyo, ili usanaa wowote ule uweze kufanikiwa, ni sharti fanani naye awe amefaulu katika hali yake ya utambaji.

Inasemekana kuwa binadamu huzaliwa na silika ya kuigiza sherehe, ngoma, na vitendo vya wahenga ambavyo ndivyo chanzo cha usanaa. Hata hivyo, sanaa za maonyesho zilipotengana na dini na harakati nyingine za matambiko, fikra na tabia za binadamu zilichukua sehemu kubwa katika mipango ya sanaa hiyo.

Katika utambaji hadithi, mwigizaji hujionyesha katika sauti na vitendo vya utambaji akitenganisha watu mbalimbali, wanyama mbalimbali au vitendo mbalimbali. Mtambaji huchukua mafunzo yake kutokana na maisha na kuijenga sanaa yake kutokana na tabia, fikra na vitendo vya watu Ulimwenguni.

Mtambaji wa hadithi anaweza kuiathiri hadhira yake kutokana na hisia, fikra na pia vitendo vyake. Hii ni kwa sababu sanaa, kwa ujumla, ni njia ya mawasiliano inayokuza maisha; maarifa na fikra za watu. Misingi na matokeo ya sanaa huwa yameambatana sana na jamii, na nia ya mwisho ya sanaa hiyo huwa ni kudhihirisha na kueleza yale yanayothaminiwa na jamii.

Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa mtendaji au fanani huwa na nafasi ya kukuza fikra za hadhira kulingana na vile anavyoitoa sanaa kwa hadhira hiyo. Mbinu za kisanaa, vile vile, hupata mashiko zaidi iwapo zitawasilishwa vilivyo na fanani au mtambaji, kwani akishindwa kufanya hivyo, mbinu hizo zitakuwa hazina manufaa yoyote kwa hadhira na jamii kwa jumla.

# SURA YA TANO

## 5.1 MUHTASARI

Tasnifu hii imejishughulisha na utanzu wa visaasili, na hasa kuzingatia vipengele vya maana, matumizi na mbinu za usanaa katika jamii ya Wakikuyu. Mbali na kuonyesha sifa mbalimbali zinazotambulisha visaasili kama utanzu wa Fasihi Simulizi, tumevichambua visaasili vya Wakikuyu na kuonyesha matumizi yake katika jamii hiyo na aidha mbinu za usanaa zilizo katika visaasili vya jamii hiyo.

Katika sura ya kwanza, tunapata msingi ambao tasnifu hii imejengeka. Miongoni mwa mambo muhimu ambayo yameshughulikiwa katika sura ya kwanza ni pamoja na somo la utafiti, madhumuni na sababu za kuichagua mada, upeo wa tasnifu, njia zilizotumiwa katika utafiti, pamoja na nadharia ambayo imetumika kuvichambua visaasili katika tasnifu hii. Jambo jingine ambalo limepewa umuhimu mkubwa katika sura hii ni masuala mbalimbali ambayo yamekwisha kuandikwa kuhusiana na utanzu wa visaasili na ambayo yana uhusiano kwa namna moja ama nyingine na mada ya tasnifu hii.

Katika sura ya pili, mambo muhimu kuhusiana na utanzu wa hadithi kwa ujumla yameshughulikiwa. Tumeeleza maana ya tanzu mbalimbali za hadithi kama vile mighani, epiki, visaasili, hekaya, hurafa na kuonyesha uhusiano uliopo katika tanzu hizo unaowakanganya wengi.

Aidha, katika sura ya pili, tumeeleza mambo muhimu katika utambaji hadithi miongoni mwa Wakikuyu kama vile wakati na mahali pa utambaji. Vile vile, sheria zinazowaongoza watambaji na hadhira katika utambaji zimetolewa maelezo.

Katika sura ya tatu, tumeingilia swala la kuonyesha matumizi ya utanzu wa visaasili katika jamii ya Wakikuyu. Tulivichambua baadhi ya visaasili vya Wakikiyu na kuvitoa kama mifano katika vitengo mbalimbali vinavyoeleza matumizi hayo Matumizi hayo ni kama vile kuelimisha jamii, kutawala jamii, kutoa maadili katika jamii,

kuonyesha ufundi miongoni mwa Wakikiyu, na vile vile kuburudisha au kuwastarehesha watu katika jamii hiyo.

Katika sura ya nne, tumeonyesha mbinu za usanaa uliopo katika utanzu wa visaasili huku tukitoa mifano ya visaasili vya Wakikuyu tulivyochambua. Sura hii imenuia kuonyesha dhahiri kuwa, utanzu wa visaasili una matumizi mengi ya mbinu za usanaa, jinsi tanzu nyingine za Fasihi Simulizi zilivyo. Aidha katika sura hii tumetoa maelezo ya kijumla kuhusiana na sanaa, usanaa na msanii au fanani na umuhimu wake katika kufanikisha sanaa katika utambaji. Miongoni mwa mbinu za usanaa tulizoeleza na kutoa mifano ni kama vile taharuki, chuku, ucheshi, takriri, tanakali-sauti na tashihisi au uhaishaji. Kwa jumla, tasnifu hii imejaribu kuonyesha kwamba, visaasili ni utanzu ulio na umuhimu mkubwa sana katika jamii kwa kuwa unaelimisha, kufahamisha, kuburudisha na kustarehesha watu.

## 5.2 <u>MATOKEO YA UTAFITI</u>

Katika kuvichunguza visaasili vya jamii ya Wakikuyu, imebainika kuwa visaasili ni utanzu wa kifasihi ulio na mbinu za kisanii na ubunifu.

Kuhusu matumizi ya visaasili, jambo ambalo limebainika ni kwamba jamii hazioni visaasili kama utanzu usio na maana bali kama amali inayothaminiwa sana. Visaasili hufunza wanajamii mambo mbalimbali ya kimaisha na jinsi wanavyokabiliana na Ulimwengu unaowazunguka.

Visaasili hufunza, sio tu jinsi wanadamu walivyo ama watakiwavyo kuwa, bali pia mambo na vitu vinavyowazunguka na jinsi wanavyokabiliana na mambo na vitu hivyo. Visaasili hufunza na kuelimisha. Katika miaka ya nyuma ya akina babu zetu, hakukuwapo mashule wala vyuo kama tunavyovifahamu hii leo. Njia bora na mwafaka iliyokuwapo kuifunza jamii mambo mbalimbali kuhusu maisha na mazingira ilikuwa matumizi ya mbinu mbali mbali kama vile utanzu wa visaasili.

Utanzu wa visaasili katika jamii ya Wakikuyu ulitekeleza wajibu muhimu sana sio tu kufunza sayansi ya maumbile ya vitu au mambo mbalimbali, bali pia utamaduni wa jamii; na kwa kufanya hivyo, ulitoa mwelekeo wa maisha kwa wanajamii. Visaasili

hufunza mienendo na kanuni zinazokubalika katika jamii na mfano mzima wa jamii. Kwa kufanya hivyo, visaasili huwa havitumiki tu kurithisha amali na utamaduni wa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine, bali pia huhalalisha mfano na matendo ya jamii kuhusiana na asili ya mambo mbalimbali. Wanajamii wanapojifunza sababu za kuwepo mambo fulani katika visaasili yanayokubalika na kuthaminiwa na jamii, utamaduni wa jamii huwa unahifadhiwa na kuendelezwa katika vizazi mbalimbali.

Hali kadhalika, visaasili hutumika kama tasjili za kihistoria na kuwa kumbukumbu ya mambo na matendo ambayo huenda yamebadilika ama kuachwa nyuma na wakati. Mambo mbalimbali ambayo huaminiwa kuwa yalitokea katika jamii ya Wakikuyu, kisha baadaye yakabadilika, kwa mfano mfumo wa utawala, huweza kufunzwa kwa vizazi vya baadaye ambavyo huenda havikushuhudia matukio hayo.

Wajibu wa kufurahisha na kustarehesha pia ulikuwa muhimu sana katika visaasili. Huo ndio uasili wa tanzu mbalimbali za fasihi. Ilikuwa ni katika mazingira ya burudani kama hayo ambamo mafunzo mbalimbali yalitolewa. Hali kama hiyo ya starehe na burudani iliwezesha ujumbe uliokusudiwa kwenye visaasili kukolea na kuwanata washiriki.

Vikao vya utambaji hadithi, vikiwemo visaasili, viliruhusiwa nyakati za jioni, baada ya kazi nyingi za mchana kutwa. Mbali na kuwa utambaji uliwapumzisha na kuwastarehesha wanajamii baada ya kazi, utambaji huo uliweza pia kuwaelekeza wanajamii kwa kuwapa shughuli muhimu ya kufanya na kuwaepusha na maovu katika jamii.

Visaasili pia vilisaidia kukuza na kuzoeza maarifa miongoni mwa watu. Visaasili ni visa ambavyo huwa na mafunzo mbalimbali, na katika kuvisikiliza, mtu huhitajika kufikiria akilini mwake ili aweze kung'amua funzo lililomo. Kwa njia hii, ile hali ya kufikiria kwa makini huwa na madhumuni ya kukuza ubongo au fikra za mtu.

Vile vile, uhodari na ustadi wa fanani uliweza kugezwa katika vikao vya utambaji. Jambo hilo liliweza kuwatia motisha watu mbali mbali katika jamii

wajishughulishe na visaasili. Ugwiji wa fanani yeyote yule ungeweza kutokana na uwezo wake wa kuigiza maelezo yake na aidha kutumia, kwa njia mwafaka, mbinu za usanaa zinazohusika. Utambaji huo ungeweza kuwakuza vilivyo watambaji katika jamii na hivyo kusaidia katika uhifadhi sio tu wa visa-husika bali pia katika uhifadhi wa fanani katika jamii.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Inafaa tafiti nyingi zifanywe ili nafasi ya visaasili iweze kutambuliwa na pengine kutoa mchango wake katika ukuaji wa jamii. Bila shaka utafiti utakaofanywa, katika kuchambuliwa visaasili na kubainisha matumizi katika jamii mbalimbali utakuwa na maana sana kuliko pengine ukusanyaji tu wa visaasili usioweza kusaidia hadhira ya wasomaji kuvielewa visaasili vinavyohusika.

Jambo jingine ambalo lahitaji sana kufanyiwa utafiti pia ni kuonyesha usanaa uliopo katika visaasili. Miktadha ya kiasili iliyoruhusu vikao vya utambaji hadithi kwa ujumla imebadilika, na pengine visaasili ambavyo tutaendelea kuwa navyo ni vile vinavyopatikana katika maandishi. Utafiti unaweza kubainisha ni kwa namna gani visaasili, ambavyo vimeandikwa na havipo katika miktadha ya kiasili, vinaweza kutumiwa kwa manufaa ya wanajamii wote.

Mfumo wa elimu haujatambua umuhimu wa tanzu za Fasihi-Simulizi na kuzithamini kwa mchango unaoweza kufidisha elimu na mafunzo kwa wanajamii. Inafaa tanzu hizi zipewe umuhimu zaidi kwa kuzifanya ziwe miongoni mwa kazi muhimu ama za lazima katika vyuo na mashule. Masomo yatakayojengeka kwenye misingi ya kitamaduni, na kuendeleza mbinu za kiasili za kuelimisha kama vile visaasili, yatapata msingi thabiti na kuwapa wanajamii mwongozo mwema na mwelekeo utakaowanufaisha katika maisha yao.

Vyombo vya habari kama vile redio, magazeti, majarida, na vinginevyo pia vyapaswa kusaidia katika usambazi wa utanzu wa Fasihi Simulizi kwa asasi za elimu. Ni muhimu iwapo vyombo kama vile redio na magazeti vitakuwa na vipindi vingi au

sehemu kubwa ambamo tanzu za Fasihi Simulizi na umuhimu wake katika jamii utaweza kusisitizwa ipasavyo.

Vyuo vya mafunzo ya walimu aidha vitasaidia vilivyo iwapo vitawasajili walimu wengi wa somo la Fasihi Simulizi. Hii ni kwa sababu shule nyingi huwa na tatizo kubwa la upungufu wa walimu wa Fasihi Simulizi, jambo ambalo huwafanya wanafunzi kukosa fursa ya kulisoma somo hilo lililo muhimu sana maishani mwao.

Makampuni ya uchapishaji wa vitabu yanafaa kuwatia moyo waandishi chipukizi wa vitabu vya Fasihi Simulizi. Kwa kuchapisha vitabu vingi vya Fasihi Simulizi, makampuni hayo yatawamotisha watu kuandika zaidi, na hivyo basi tatizo la ukosefu wa vitabu vya Fasihi Simulizi litaweza kutatuliwa.

## MAREJELEO:


Abrahamson, M. (1978). Functionalism. Prentice Hall Inc.; New Jersey, Prentice Hall Inc.

Akivaga, K. na Odaga, B. (1982). Oral Literature : A School Certificate Course Heinemann Educational Books; Nairobi.

Bahemuka, J. M. (1982). Our Religious Heritage. Thomas Nelson and Sons Ltd; Edinburg.

Bascom, W. R. (1965). ''Four Functions of Folklore" Katika Alan Dundes (Mhariri), The Study Of Folkore Prentice - Hall, Inc, Englewood Cliffs; New Jersey.

Beuchat, P. D. (1965)."Riddles In Bantu" Katika Alan Dundes (Mhariri) The Study Of Folklore: Prentice - Hall, Inc, Englewood Cliffs; New Jersey.

Biebuyck, D. na, Mateene, C. (Ed) (1971). The Mwindo Epic. University of California Press; Berkeley.

___________ (1979)."The African Heroic Epic" University of California Press; Berkeley.

Bottignole, S. (1984). Kikuyu Traditional Culture And Christianity Heinemann Educational Books; Nairobi.

Brown, R. A. (1935). On the Concepts of Functions in Social Sciences American Anthropologists; New Jersey.

Carol, R. E. na Luin, M. E. (1973). Anthropology. Prentice- Hall, Inc.; New York.

Campbell, J. Makala "The need for New Myths" Katika jarida la Time January 17, 1972.

Cunnigham, A. (1973). The Theory of Myth. Sheed and Ward Ltd.; London.

Chacha, D.M. (1991). "Kitendawili" cha Vitendawili : Maana na Matumizi Katika Jamii ya Wakuria; Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Doke, E.M. (1947). "Bantu Wisdom Lore" African Studies: Toleo 6, Nambari 3.

Eliade, M. (1957), Myths, Dreams and Mysteries. Harper and Row Publishers; New Jersey.

Esenwein, J. B. (1909). "Writing the Short Story ". A Practical Handbook on the Rise, Writing and Sale of Modern Short Story Nobe and Eldredge; New York.

Finnegan, R. (1970). Oral Literature in Africa. Oxford University Press; Nairobi.

Gakuo, K. (1992). Nyumba Ya Mumbi. The Gikuyu Creation Myth Jacaranda Designs Ltd. ; Nairobi.

Haji, A. I. 1982). "Fasihi Ni Nini?" Katika A.I. Haji na Wenziwe (Wahariri). Misingi Ya Nadharia Ya Fasihi. ; Taasisi Ya Kiswahili Na lugha za Kigeni; Zanzibar.

Hamilton, E. (1953). Mythology. Cambridge University Press; London.

Herskovits, S. F. na Melvile, J. (1958). Dahomean Narrative. North Western University Press; Evanston.

Isajiw, W. W. (1968). Causation and Functionalism in Sociology. Routledge and Kegan Paul Ltd; London.

Jahadhmy, A. A. (1975). Kusanyiko La Mashairi. Anthology Of Swahili Poetry : Heinemann Educational Books; Nairobi.

Jones, E. D. (1988). Oral and Written Poetry in African Literature Today. James Currey Ltd; London.

Kabira, M. W. (1980). Gikuyu Oral Narratives. Heinemann Educational Books; Nairobi.

__________ (1983). The Oral Artist. Heinemann Educational Books; Nairobi.

Kenyatta, J. (1938). Facing Mt. Kenya. Heinemann Educational Books; Nairobi.

Kerenyi, C. na Jung, C. C (1951). Introducation to A Science Of Mythology. Routledge and Kegan Paul Ltd; London.

Kipury, N. (1983). Oral Literature Of The Maasai : Heinemann Educational books; Nairobi.

Kirumbi, P. S. (1975). Misingi Ya Fasihi Simulizi. Shungwaya Publishers; Nairobi.

Knappert, J. (1971). Myths And Legends Of The Congo. Cox and Wymann Ltd; London.

Lusweti, B. M. (1984). The Hyena And The Rock: A Handbook Of Oral Literature For Schools. Basingstoke, Macmillan Publishers; London.

Malinowski, B. (1926). Myth in Primitive Psychology. Norton Library; New York.

Mbele, J. M. (1977). "Sundiata. The Epic as an Ideological Weapon. "(Mimeo) Chuo Kikuu Cha Dar - es- Salaam, Idara ya Fasihi; T.U.K.I.

Mlama, P. (1981). Makala Ya Semina Ya Fasihi Simulizi.Chuo Kikuu cha Dar -es- Salaam, T . U . K . I.

Msokile, M. (1992). Misingi Ya Hadithi Fupi. Dar -es- Salaam University Press, Dar -es- Salaam.

__________(1993), Misingi Ya Uhakiki wa Fasihi. East African Educational Publishers; Nairobi.

Muhando, P. na Balisidya, N. (1976). Fasihi na Sanaa za Maonyesho. Tanzania Publishing House; Dar- es-Salaam.

Mwangi, R.(1976). Kikuyu Folktales. East African Educational Publishers; Nairobi.

Njau, R. na Mulaki, C. (1984). Kenya Women Heroes. Heinemann Educational Books; Nairobi.

Njururi, N. (1966). Agikuyu Folktales. Oxford University Press; London.

__________(1977),Tales From Mount Kenya. Transafrica Publications; Nairobi.

Odaga, B. O. (1984). Yesterday's Today. Lake Publishers and Enterprises; Kisumu.

Oinas, F. J. (Ed) (1978a). Heroic Epic and Saga. Indiana University Press, Bloomington; London.

Okpewho, I.(1977)."Does the Epic Exist in Africa: Some Formal Considerations". Research In African Literatures. University of Texas Vol 8. No.8. Texas.

______________ (1979). Epic In Africa. Colombia University Press; New York.

______________ (1983),Myth In Africa. Cambridge University Press; London.

Okombo, O. na Nandwa, J. (1982). Reflections on Theories and Methods of Oral Literature. K.O.L.A; Nairobi.

Olela, H. (1981). From Ancient Africa to Ancient Greece; An Introduction to the History of Philosophy. The Select Publishing Corporation; London.

__________ (1988). Philosophy Of Education Kenyatta University Faculty of Education and University of London Institute of Education.

Omari,CK. na Wenziwe(Wahariri) (1975). Misemo na Methali Toka Tanzania. E . A. L . B ; Nairobi.

Onyango, O. na Roscoe, A. A. (1974). Keep My Words. East African Publishing House; Nairobi.

Pick, V. M.(1973). Ndai na Gicandi. (Kikuyu Enigmas) Editria Misionaria Italiana; Bologna.

Robertson, S. (1889). Religion Of The Semites. Edinburg.

Ruthven, K. K. (1976). Myth, The Critical Idiom. Harper and Row Publishers; London.

Sankan. S. S. (1971). The Maasai. Kenya Literature Bureau; Nairobi.

Senkoro, F.E.M.K. (1982). Fasihi. Dar - es - Salaam Press and Publicity; Dar-es-Salaam.

Soyinka, W. (1976). Myth, Literature and the African World. Cambridge University Press; London.

Stewart, R.J. (1989). The Creation Myth. Element Book Ltd; Dorset.

Syambo, B. na Mazrui, A. (1992). Uchambuzi wa Fasihi. East African Educational Publishers; Nairobi.

Taban Lo Lyong (1972). Popular Culture Of East Africa. Longman (K) Ltd; Nairobi.

Vansina, J. (1985). Oral Tradition as History. Heinemann Educational Books; Nairobi.

Warner, A. (1968). Myths and Legends of the Bantu. Francass Co. Ltd; London.

Wellek, R. na Warren, A. (1949). Theory of Literature. Cox and Wymann Ltd; London.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY